

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Hamsini na Nne – Tarehe 18 Juni, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Mkutano wa Tatu,  
Kikao cha Hamsini na Nne.

Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

Na. 445

**Mifuko ya Uvezeshaji Wananchi Kiuchumi**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza: -

Je, ni kwa kiasi gani mifuko ya uvezeshaji kiuchumi  
iliyoanzishwa kwa lengo la kuwaondelea wananchi umasikini  
na kuwajengea uwezo wa kiuchumi imenufaisha wanawake  
wa kitanzania kutoka mikoa ya nje ya Dar es Salaam?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA  
NA AJIRA (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nitumie fursa hii adhimu kulishukuru Bunge lako la Jamhuri ya Muungano kwa kuwapa ruhusa Wabunge kujumuika nasi pale Mwanza katika tukio kubwa la Kitaifa la mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alikuwa akikutana na vijana na changamoto zote za vijana zilizungumzwa na kujadiliwa. Lakini pia alitoa mwelekeo mzuri wa Kitaifa wa namna gani tutakavyoenda kutatua changamoto hizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge lakini pamoja na hilo sambamba Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuratibu vizuri shughuli hiyo lakini sambamba na hilo tunaenda kwa kweli kupitia Waheshimiwa Wabunge hawa kuwasaidia vijana wote nchi nzima hasa kwa kuwasikiliza, kuwapokea na kutatua changamoto zao katika maeneo mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi katika kufanya hivyo kwa kweli tutahakikisha kwamba vijana hawa wanapewa kila wanachostahili kwa Serikali kutengeneza mazingira wezeshi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa muda huo lakini pia sasa nitumie fursa hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Desemba, 2020, mifuko na programu za uvezeshaji zimetoa mikopo, ruzuku na dhamana yenye thamani ya shilingi trilioni 4.34 kwa wajasiriamali 6,037,462. Kati ya hao, wanawake ni 3,079,105 sawa na asilimia 51 na wanaume ni 2,958,357 sawa na asilimia 49. Aidha, jumla ya ajira 10,844,589 zimetengenezwa kupitia uvezeshaji huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya wanawake 3,079,105 walionufaika na mikopo, ruzuku na dhamana kupitia mifuko na Programu za Uvezeshaji, wanawake 1,046,896 sawa na asilimia 34 wametokea Mkoa wa Dar es Salaam na

wanawake 2,032,209 sawa na asilimia 66 wametokea katika mikoa mingine nje ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi litaendelea kuweka mikakati ambayo itaimarisha utendaji wa mifuko na programu hizi ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi na tija.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Neema Lugangira swali la nyongeza!

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nashukuru sana Serikali kwa majibu mazuri. Sasa nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni ipo haja ya kufanya tathmini ya mifuko hili ya uwezeshaji kwa kuzingatia muda mfuko ulipoanzishwa, jumla ya mikopo iliyotolewa, ruzuku na dhamana pamoja na hali ya marejesho. Na tathmini hii pia iangalie hasara na faida ili kwa kufanya hivyo, Serikali iweze kuja na mikakati ya kuimarisha utendaji wake na iwe na tija kwa maendeleo ya wanawake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili ni kutokana na changamoto kubwa za ajira kwa vijana, je, Serikali haioni ipo haja sasa ya kuweka vipaumbele vyta kutoa *startup capital* kwa wahitimu wa vyuo maana mara nyingi vijana hawa wanakuwa na *bankable ideas* lakini wanashindwa namna ya kupata mikopo, ruzuku na dhamana zenyе riba na vigezo nafuu? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana kwa sababu amekuwa mfuatiliaji kwa wakati wote katika masuala haya yanayohusu maendeleo ya vijana lakini pia wanawake na Watoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna haja kubwa ya kufanya tathmini ya muda kuhusiana na masuala ya ruzuku na dhamana ambazo zimekuwa zikitolewa kila wakati ili kuangalia kama inaleta tija. Katika hatua hiyo, Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa tayari tumekwishakuanza kufanya zoezi hilo ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya mifuko yote 54 na ile mitatu ambayo ipo chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tayari tumekwisha kuanza kufanya zoezi hilo ili kuweza kuangalia namna gani ambavyo itakuwa na tija zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ambayo baadhi ya hayo ambayo tumeyabaini, ukiacha kazi ya timu ambayo bado inaendelea, tumebaini kwamba katika fedha hizi nyingi zinatolewa wakati mwingine vikundi vinakuwa havijaunganishwa vizuri zaidi na tumeenda kwenye hatua ya kuona kwamba lazima sasa kuwe na tija ya kutoa mafunzo kabla ya kutoa mikopo hii. Vilevile kuweza kufanya na kuangalia yale maandiko ya mpango kazi au mpango wa biashara kwa maana ya zile *business writeups* ambazo zinazletwa kwa ajili ya wao kufanya hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hatua nyingine pia tunaangalia namna ya kuweza kutanua wigo wa kutoa mikopo hii au fedha hizi na uwezeshwaji huu kwa makundi mengi zaidi na kuona jinsi gani ambavyo inaweza ikaenda kwa mtawanyo kwa maana ya uwiano mzuri katika mikoa lakini pia katika Majimbo na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tumebaini jambo jingine ambalo katika mikopo hii ambayo imekuwa ikitolewa, na tutakubaliana kwamba fedha hizi zimekuwa zikitolewa katika mifumo mbalimbali. Ukiangalia kwenye Halmashauri kuna ile 4:4:2 kwa maana ya fedha ambazo ni asilimia 4 kwa wanawake, 4 kwa vijana na 2 kwa

watu wenye ulemavu. Fedha hizi zimekuwa zikitolewa nchi nzima lakini kwa sehemu kubwa utaona kwamba marejesho yamekuwa ni hafifu sana. Kwa hiyo, tulitegemea kwamba fedha hizi zikitolewa, vijana hawa waweze kuzifanya kazi na wa-graduate waende kwenye hatua ambayo watawaachia wengine waweze kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaenda kwenye hatua nyingine ambayo bado ipo katika hatua ya mashauriano kuona kama tutaweza kutoa asilimia 50 ya vifaa na 50 iwe fedha kwa ajili ya *operational cost* kwa sababu ili tuweze kama ikitokea wameshindwa kulipa, tumewapa trekta au mashine za kushona nguo ama tumewapa vifaa vitendea kazi labda mashine za kufyatua tofali na ilikuwa mkopo labda wa milioni 10; tukawapa milioni 5 gharama za mashine na milioni 5 nyingine wakapewa kama fedha taslimu maana yake ni kwamba hata wakishindwa kurejesha walau tunaweza tukarejesha ile mashine ya kufyatua tofali ikawasaki die vijana wengine kuliko sasa hivi mfumo wa *returns* umekuwa mgumu na halmashauri zimekuwa zikhangaika wakati mwingine kulazimika kuwapeleka mahakaman. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la Mheshimiwa la kuona namna gani ambavyo tunaweza tukatengeneza *startup capital* kwa wanafunzi wahitimu wa vyuo vikuu ni pamoja na mpango mzuri ambao tumekuwa nao katika Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu...

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri utajibu hapo kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ni pamoja na mpango huu ambao tumeanza kuona bado lipo katika kuona namna gani ambavyo vijana wa vyuo vikuu tutawaingiza kwa programu tatu ambazo zipo. Kwa sasa tumeanza na programu ya uanagenzi ambayo kimsingi inatumika kwa wale ambao hawajamaliza chuo kikuu lakini tuna programu maalum ya *internship* ambayo

tayari tunawachukua vijana hawa na kuwaunganisha kwenye maeneo ya ajira. Sambamba na hilo, tunatoa mafunzo pia na kuwasaidia kuweza kupata mikopo kwenye maeneo ya halmashauri lakini pia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana unaotolewa na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo pia tumelichukua na tutalifanyia kazi, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana. Sasa tunakwenda Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Namuita Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakatwe aulize swali lake.

Na. 446

### **Ujenzi wa Daraja Barabara ya Kishanda B –Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Daraja katika barabara ya Kishanda B limefunkwa na maji, hivyo kukatisha mawasiliano ya Wananchi wa kata za Nyaruzumbura, Nyakatuntu, Kakanja, Kikukuru, Mabila na Kitwe Wilayani Kyerwa.

Je, ni lini Serikali itajenga Daraja katika barabara hiyo ili kuwarejeshea mawasiliano wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALLI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa, Innocent Sebba Bilakwate Mbunge wa Jimbo la Kyerwa kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kishanda B ni sehemu ya barabara ya Nyaruzumbura –Kishanda yenye jumla ya

kilomita 3.4 na eneo korofi kwa maana ya tinga tinga lina urefu wa mita 300. Barabara hii ni muhimu kwa wananchi wa Wilaya ya Kyerwa kwa sababu inaunganisha Makao Makuu ya Wilaya na Kata za Nyaruzumbura, Nyakatuntu, Kikukuru, Mabira na Kitwe katika Wilaya ya Kyerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na jiografia ya Wilaya ya Kyerwa kuwa na maeneo mengi yenye tinga tinga (*swamp areas*) Serikali kuititia Mfuko wa Barabara (*Road Fund*) imekuwa ikitenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya ukarabati wa maeneo korofi ambapo kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 hadi 2020/2021 shilingi milioni 862.54 zimetumika katika maeneo korofi kwa maana ya tinga tinga Wilayani Kyerwa katika barabara za Omukigando-Mkalinzi kilometra 0.18, Isingiro-Ishaka-Ibare kilometra 7.8, Nyabishenge-Nyakakoni kilometra 10, Kamuli-Mtagata-Kigorogoro (*Omukagoye swamp*) na barabara ya Rwabwere-Karongo kilometra 10 na utekelezaji wa barabara hii unandelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi milioni 33 kwa ajili ya ujenzi wa maboksi kalvati manne ili kusaidia kuitisha maji katika eneo la Kishanda B. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya barabara na madaraja nchini ikiwemo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakatwe swalii la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza niishukuru Serikali kwa kazi inayofanyika kwa upande wa barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kyerwa ni miongoni mwa Wilaya ambazo zina vipindi virefu vya mvua, barabara zake zinatengenezwa kwa udongo, sasa Serikali ina mpango gani wa kuongeza bajeti ili barabara hizi ambazo

hazipitiki kipindi cha mvua ziweze kutengewa bajeti ya changarawe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; niishukuru Serikali kwa ombi langu lla kujenga lami katika Mji wa Nkwenda, kazi ambayo tayari imekamilika lakini nililetu ombi kwa sababu ya umuhimu wa ule Mji wa Nkwenda kuweka taa pale. Je, Serikali imefikia wapi ombi ambalo nimelileta kwenu kuweka lami katika Mji wa Nkwenda? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKLIA ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anaomba tu, amejaribu ni ombi vilevile ni ushauri, upi ni mpango wa Serikali wa kuongeza bajeti. Nafikiri baada ya Wabunge wengi kuzungumza ndani, Serikali katika bajeti kuu imekuja na mpango wa kuongeza fedha kwa *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuseme tu kwa ongezeko hilo la fedha ambalo Bunge lako Tukufu likiwapendeza wakapitisha, basi tutaongeza bajeti katika halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Kyerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili; ameshukuru kwamba Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa lami katika eneo la Mji wa Nkwenda na hiyo lami imeshakamilika lakini sasa hivi aliletu ombi Serikalini na nimhakikishie tu kwamba ombi lake linatekelezwa na Serikali kwa sababu mkandarasi ameshapatikana, yupo *site* na taa zitawekwa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kawaambie wananchi wa Kyerwa katika Mji wa Nkenda kwamba ombi ulilolileta basi linaanza kutekelezwa; hivi niavyozungumza mkandarasi amekwenda *site*, ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 447

### **Vitambulisho vya Wajasiriamali**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA K.n.y. MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza: -

Suala la Vitambulisho vya ujasiriamali limekuwa ni changamoto hasa kwa Wafanyabiashara ambao wana mitaji midogo.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha au kufuta vitambulisho hivyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Machi 2019, Serikali kwa kuwathamini na kuwajali wajasiriamali na watoa huduma wadogo ilianzisha utaratibu wa vitambulisho ili kuwawezesha kufanya biashara katika mazingira bora na tulivu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba kweli kuna changamoto zilizojitokeza katika utoaji wa vitambulisho kwa wajasiriamali na watoa huduma wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais -TAMISEMI imefanya tathmini ya zoezi zima la ugawaji, usajili na matumizi ya vitambulisho vya wwasiriamali na watoa huduma wadogo katika mikoa na hal mashauri ili kubaini changamoto zilizopo na kufanya maboresho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2021 vitambulisho hivyo vimefanyiwa maboresho kadhaa ikiwemo kuwekwa picha na jina la mjasiriamali mdogo aliyepatiwa kitambulisho pamoja na ukomo wa muda wa kutumika kitambulisho hicho ambao ni mwaka mmoja tangu tarehe ya kupatiwa kitambulisho badala ya mwaka wa kalenda kama ilivyokuwa awali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza; nataka kujua pesa hizo za vitambulisho ambavyo wajasiriamali wanavitoa huwa zinaingia akaunti gani na mahesabu yake ni yapi, swali la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; wanaonaje wakaweka utaratibu hasa wafanyabiashara wa mbogamboga na mama ntilie ambao mitaji yao ni midogo wakahakikisha kwamba chaji yao inakuwa moja kwa nchi nzima badala ya bei inakuwa juu zaidi kwa sababu wengi mitaji yao ni midogo, ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKLI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza ametaka kujua tu fedha za wajasiriamali wadogowadogo zinaingia katika mfuko gani, ni kwamba zinaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, huko ndiko ambako fedha zinakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili alikuwa tu anataka kujua ukomo. Nieleze tu kwamba wakati Serikali

inapanga ukomo wa shilingi 20,000 ilikuwa imezingatia vipato vyta wananchi wetu na ndio maana awali hawa wakina mama ntile, wafanyabiashara wadogowadogo walikuwa wanalipa fedha nyangi zaidi kwa kuchangia kidogokidogo kila siku lakini ilipowekwa shilingi 20,000 maana yake tulikuwa tumewasaidia kupunguza hiko kiwango. Kwa hiyo, hiki kiwango ambacho kipo kwa sasa bado kinazingatia hali halisi iliyopo lakini sisi tutalipokea ombi lako na tutaendelea kulizingatia kwa kadri ya mahitaji ya wafanyabiashara wetu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunakwenda Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, namuita Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba aulize swali lake.

Na. 448

### **Kuhuisha Miundo ya Utumishi kwa Kada Mbalimbali**

**MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaondoa changamoto ya kukaimu muda mrefu kwa watumishi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Sekretarieti za Mikoa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua changamoto ya uwepo wa Watumishi wanaokaimu nafasi za uongozi kwa muda mrefu na uchambuzi uliofanyika unaonesha kuwa, watumishi 1,496 wanakaimu nafasi za uongozi katika Taasisi mbalimbali zikiwemo Halmashauri za Wilaya na Sekretarieti za Mikoa. Kati ya hao, watumishi 332 wanakaimu nafasi zao wakiwa na vibali halali kutoka kwa

Katibu Mkuu Utumishi na Watumishi 1,164 wanakaimu nafasi zao bila ya kuwa na vibali kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi, Aidha, Kati ya watumishi hawa 1,164 ambaa wanakaimu nafasi bila vibali vya Katibu Mkuu Utumishi, jumla ya watumishi 543 hawana %ifa za kukaimu nafasi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lengo la kutatua changamoto hii, ofisi yangu imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kukusanya taarifa za maafýsa Waandamizi na Wakuu 7,008 katika Utumishi wa Umma wakiwemo watumishi wanaokaimu nafasi hizo ili wafanyiwe upekuzi kwa ajili ya kujaza nafasi wazi za uongozi na zinazokaimwa kwa muda mrefu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Mtemvu swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Swali la kwanza; kwa kuwa majibu ya Serikali yanathibitisha kuwepo kwa watumishi 332 kukaimu wakiwa na sifa lakini zaidi ya watumishi 1,164 wanakaimu bila sifa yaani hawana kibali cha Katibu Mkuu Utumishi. Sasa na ni ukweli kuwepo kwa viongozi wengi wanaokaimu kunazorotesha utendaji kazi na hivyo kutofikia malengo tarajiwa. Je, ni ipi sasa *commitment* ya Serikali kuwathibitisha au kuwaondoa watumishi wenye kukaimu zaidi ya miezi sita? (*Makof!*)

Swali la pili; kwa kuwa mchakato wa uteuzi unachukua muda mrefu sana hata zaidi ya miaka kumi na mfano upo, Katibu Tawala Msaidizi upande wa uchumi na uzalishaji Mkoo wa Kilimanjaro Ofisi ya Mkoo wa Mkoo anakaimu mwaka wa tisa toka 2012. Je, Serikali ipo tayari kutengeneza kanzidata au *database* ya wale watumishi waliofanyiwa *vetting* wengi kwa ujumla wao ili waweze kusaidia kupunguza muda ule wa watumishi kukaimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Issa Mtemvu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la kwanza tumekuta kuna changamoto kubwa sana ya waajiri kukaimisha watu wasiokuwa na sifa bila ya kupata kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi kama mwongozo unavyotaka, matokeo yake mtu anakaa kwenye nafasi muda mrefu anakuwa hafanyiwi upekuzi na hivyo kufanya mtu kukaa kwenye nafasi hiyo kwa miaka mingi. Sasa tayari tulishawaagiza waajiri wote mapema mwaka huu kuleta majina yote ya watu wanaokamimu nafasi zao kwa zaidi ya miaka mitatu ili tuweze kupitia na kuangalia ni wapi wenye sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, ni kwamba tayari tumegundua kuna watumishi 1,164 wasiokuwa na sifa na tunazidi kuwaomba waajiri waweze kuhakikisha wanakaimisha watu wenye sifa lakini vilevile kwa kibali cha Katibu Mkuu Utumishi. Waache kukaimisha kwa sababu anamtaka fulani au fulani mimi naweza nikafanya nae kazi na kumburuza, bali wakaimishe mtu kwa sababu ndie anayetakiwa kuwepo kwenye nafasi hiyo na hiyo itasaidia sana katika upekuzi na kuweza kuwathhibitisha watumishi ndani ya miezi sita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la pili la nyongeza Mheshimiwa ameuliza kama tuna kanzidata, sasa tayari tumeshaanza kukusanya taarifa na tumeshapeleka majina zaidi ya 2,300 kwa ajili ya upekuzi ili yawepo na wiki hii tunapeleka tena majina 2,400 kwa ajili ya upekuzi ili tuweze kuwa tuna watu katika kanzidata yetu wenye sifa. Tunapoona mwajiri amekuweka mtu asiye na sifa, Utumishi tutam-*post* moja kwa moja mwenye sifa ili akashike nafasi hiyo na aweze kuifanya kwa weledi na kuweza kufanya maamuzi. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Wabunge na watumishi

wote wale wenye sifa muda si mrefu mtaanza kuwaona na tatizo hili la kukaimu litaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Deo Ndejembie kwa majibu mazuri sana. Nimekuona Mheshimiwa Nape Moses Nnauye.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa tatizo hili limekuwa kubwa na kwa miaka sasa linazungumzwa na hoja ni hizi hizi na majibu ni haya haya, Serikali haioni umefika wakati wa kutunga sheria iwe ni kosa kumkaimisha mtu kwa muda mrefu. Kwamba tutunge sheria ifikie ukomo kwamba mwisho wa kukaimu ni hapa na baada ya hapa mtu akipitiliza tuchukue hatua ili tuondokane na hili mtu anakaimu miaka Tisa na hakuna mtu anachukuliwa hatua. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nape Moses Nnauye kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishesema awali tatizo hilli tunalifahamu na tayari tukishakuwa na kanzidata ya watu wenye sifa hii changamoto inaenda kuisha kwa sababu tutaanza ku-*post* moja kwa moja watu kwenye nafasi hizi zilizo wazi. *Commitment* yetu ni kwamba tutaendelea kulifanya kazi na kuhakikisha kwamba nafasi zote zinazokaimwa zinakuwa na watu wenye sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilihakikishie Bunge lako kwamba muda si mrefu tutakuwa tayari tuna watu wenye sifa kwenye nafasi zao. Vilevile, nichukue fursa hii

kuwaasa na kuwaagiza watumishi wote nchi nzima kuhakikisha ifikapo mwisho wa mwezi huu, walete majina yote ya watu ambao wanakaimu nafasi zao bila kibali cha Katibu Mkuu Utumishi. Vilevile, ifikapo tarehe 30 ya mwezi huu, walete majina ya wote wanaokaimu kwa vibali vyta Katibu Mkuu Utumishi ili tuweze kuwafanyia upekuzi na kama wao wanafaa kuwa kwenye nafasi hizo, basi tuwaache hapohapo kwenye nafasi hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, nafikiri ikifanyiwa kazi jambo hili litasaidia sana hata kujenga *morale* kwa watumishi wetu. (*Makofii*)

Tunakwenda Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, namwita Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga aulize swali lake.

Na. 449

**Ujenzi wa Barabara ya Tanga – Mabokweni – Maramba –  
Daluni – Bombo hadi Korogwe**

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Tanga – Mabokweni – Maramba – Daluni – Mtoni – Bombo – Magoma hadi Korogwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG.  
GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Tanga – Mabokweni – Maramba – Daluni – Bombo Mtoni – Korogwe yenye urefu wa kilometa 127.69 ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*). Aidha, Sehemu ya barabara ya Tanga – Mabokweni yenye urefu wa kilometa 11.2 tayari imejengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kiuchumi wa barabara ya Tanga – Mabokweni – Maramba – Daluni – Bombo – Korogwe kwa wananchi wa maeneo ya Mashewa, Mabokweni, Maramba, Bombomtoni, Magoma na Daluni. Kwa kutambua umuhimu huo, Wizara imetenga fedha katika bajeti ya mwaka wa fedha ujao 2021/2022 kiasi cha shilingi milioni 1,275.4 ambayo ni sawa na bilioni 1.2754 ili kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii. Mara baada ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamilika, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii. Aidha, barabara hii itaendelea kufanyiwa matengenezo mbalimbali ili iweze kupitika majira yote ya mwaka. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Muuliza swali naona ameridhika, Mheshimiwa Kitandula swali la nyongeza.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii imekuwa ikiahidiwa na Marais watatu walipita. Je, Serikali haionti kwamba kutotekelezwa kwa ahadi za Marais wetu watatu ni kipindi kirefu sana? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; tunaishukuru Serikali kwamba kwa kipindi hiki sasa imetenga bilioni moja kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu. Je, Serikali inatuhakikishia kwamba kazi hii itaenda kufanyika na kukamilika kwa kiasi hiki cha fedha? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba barabara hii imeahidiwa na Marais watatu kama alivyosema na ni kweli ni muda mrefu, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Mkinga na wananchi wa Mkinga kwamba wawe na imani na Serikali na ndio maana hata fedha tumeonesha kiasi ambacho tumekitenga ili kutimiza ahadi hizo za Marais na awe na imani sana na Awamu hii ya Sita inayoongozwa na Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Naomba nimhakikishie kwamba itatekelezwa kama tulivyoahidi na tulivyopanga kwenye bajeti. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; nimhakikishie kwamba bajeti iliyotengwa kwa maana ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina itatosha kufanya kazi hii na kama iliyopangwa kazi hii ya usanifu na upembuzi yakinifu itakamilika, ahsante. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florent Kyombo, swalii la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, viongozi wetu wa Kitaifa kwa nyakati mbalimbali wamefanya ziara ndani ya Wilaya ya Miseni na kuahidi ujenzi wa barabara za lami. Barabara ya Mutukula kwenda Minziro lakini vilevile barabara kutoka Kadieli Kata ya Ishozi mpaka Gela njia panda. Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi za viongozi wetu wapendwa? Ahsante. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Mheshimiwa Kasekenya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba

kujibu swalı la nyongeza la Mheshimiwa Florent Kyombo, Mbunge wa Misenyi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara ya Mtukula hadi Minziro iliahidiwa na anakubaliana na mimi kwamba kuna kazi tayari imeshanza. Baada ya kukamilisha kwa kiwango cha changarawe na kuifungua basi tutafanya kazi ya pili itakuwa ni kuisanifu kwa ajili ya kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja ya pili ni barabara ambayo tayari ameshakuja mara kadhaa ofisini ni barabara ambayo ilikuwa inahudumiwa na Wakala wa Barabara (*TARURA*) na tayari tunafanya mawasiliano na wenzetu ili tuone namna ya kuipandisha hadhi lakini itategemea na wao watakavyoleta mapendekezo yao ili barabara hiyo kwa umuhimu wake iweze kuchukuliwa na *TANROADS* kama itakuwa imekidhi vigezo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swalı la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi niweze kuuliza swalı dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa kuna ahadi ya muda mrefu ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara inayotoka Karatu – Kilimapunda – Mbulu, ahadi hii imekuwa ni ya muda mrefu sana.

Je, ni lini sasa Serikali mtatekeleza ahadi hiyo kwa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalı la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara aliyoitaja ya kuanzia Karatu kuja Mbulu ni ahadi ya muda mrefu, lakini nataka nimhakikishie kwamba katika bajeti ijayo lakini hata mwaka huu barabara hii itatangazwa mara moja kuanzia kipande cha Mbulu kwenda Haydom ambayo ni sehemu ya barabara hiyo. Kwa hiyo, tayari Serikali imeanza kutekeleza hiyo ahadi. Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa majibu mazuri Mheshimiwa Naibu Waziri, na nina kimemo hapa cha Mheshimiwa Mbunge Daniel Awack Tlemai akisisitiza jambo hilo hilo. Kwa hiyo, kwa majibu hayo nafikiri na yeye Mbunge wa Karatu amelipokea jibu hilo ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, namuita Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati aullize swali lake.

Na. 450

**Chombo Kinachosaidia Abiria Kupata Haki Zao  
Wanapopata Ajali**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je ni chombo gani kinasaidia abiria kupata haki yake pindi abiria anapopata ajali safarini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge Wa Viti Maalumu kutoka Iringa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu au watu wanaopata ajali au madhara kutokana na chombo cha moto ambacho fidia yake inasimamiwa na Sheria ya Bima wanapaswa kulipwa fidia ya madhara waliyoyapata ama kwa kuumia

au kifo kutoka kwenye kampuni ya bima ambayo chombo hicho cha moto kimekatia bima yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ajali kutokea tukio hukaguliwa na Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani na wahanga wa ajali hupatiwa fomu ya matibabu. Taarifa ya ajali fomu hii hupelekwa ofisi za bima husika na kwa mmiliki wa chombo cha moto kilichopata ajali. Kisha shauri la ajali hupelekwa mahakamani na kesi ikimalizika fomu namba 115 hutolewa kuonyesha matokeo ya kesi (*Final Case Report*). Ndipo wahanga wa ajali au ndugu huchukua nyaraka za ramani ya tukio la ajali, fomu ya matibabu, fomu ya taarifa ya ajali, fomu ya matokeo ya kesi, fomu ya ukaguzi wa chombo kilichofanya ajali, taarifa ya uchunguzi wa marehemu, kama mhanga amefariki na nakala ya bima ya gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyaraka zote hizo hupelekwa kwenye kampuni ya bima ambayo chombo cha moto kilichohusika na ajali kimekatia bima yake na wahanga hufidiwa kutokana na ukubwa wa madhara waliyoyapata. Kwa ufupi Jeshi la Polisi linathibitisha kutokea kwa ajali, Mahakama inatafsiri sheria kuhusu tukio, Daktari anathibitisha madhara waliyopata wahanga na kampuni ya bima inalipa fidia. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la yongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ajali inapotokea wamiliki wa vyombo vya moto hupewa mara moja bima yao wanapokwenda kudai chombo kama imeharibika, lakini hawa waathirika ambao ni abiria wanaopata ajali wamepoteza maisha au viungo wamekuwa wakisumbuliwa sana na hawa bima.

Je, nini kauli ya Serikali kutokana na usumbufu mkubwa sana wanaopata abiria wanaopata ajali barabarani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa abiria wengi sana wanaotumia vyombo vyा moto wanapopata ajali wanakuwa hawana uelewa wa kutosha na mara nyingi sana sasa hivi tumetumia *electronic ticketing* yaani kule nyuma hakuna elimu yoyote.

Je, sasa Serikali haioni ni wakati sasa wa kuhakikisha kwamba katika vituo vyा kusubiria abiria kuwepo na mabango na matangazo ili kutoa elimu ya kutosha kwa abiria wanapopata ajali nini wafanye? Ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Iringa.

Kwanza nataka nichukue fursa hii nimpongeze sana kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika Mkoa wake. Mheshimiwa Ritta amefika hatua ya kukarabati Kituo cha Polisi na ujenzi wa kumalizia Kituo cha Polisi katika Kata ya Semtema. Hakika amefanya kazi kubwa, kwa hili nampongeza sana lakini na wengine pia watusaidie kufanya hiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe kujibu maswali mawili. Inapotokea ajali ni kweli mmiliki wa chombo anapata fidia kama amejiunga ama amejihuisha na bima, lakini je vipi kuhusu sasa hawa abiria. Ni kweli hii ni changamoto na bado kuna changamoto nyingine kwa upande wa wananchi. Hapo nataka niwaambie kitu kwamba changamoto ya kwanza wanapopata ajali wanakuwa hawajui namna bora ya uandishi wa barua za kuombea zile fidia zao, kitu ambacho mwisho wa siku kinakuja kuwafanya wao aidha kuchelewa au kukosa kabisa kuweza kupata zile fidia kutoka bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine kwa kweli ipo kwenye upelelezi kwamba wale watu wa bima hawawezi kutoa zile fedha za fidia *unless* mpaka wahakikishe kwamba wamepata *attachment* ya upelelezi kutoka Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, hapo nataka nitoe wito pia kwa Jeshi la Polisi kwamba wahakikishe wanafanya haraka kupeleka ripoti za upelelezi kwa hawa wananchi ambao wanapata ajali ili sasa waweze kupata fidia zao kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kikubwa zaidi uelewa mdogo wa hii taaluma ya bima. Hapa natala nitoe agizo kwa Jeshi la Polisi, kwamba pamoja na kazi nzuri ya utoaji wa elimu kwa wananchi juu ya namna bora ya utumiaji wa barabara, lakini suala la elimu hii ya bima ya kuweza kupata mafao iendelee na kazi ifanyike vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine alikuwa anauliza je, sasa tuna mpango gani wa kuweka haya mabango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabango yapo, kazi imeanza na inaendelea, lakini kingine tunaendeleza taaluma ambazo kuitia mabango, vyombo vya habari, vijiwe vya bodaboda, shule pamoja na kuitia kila mahala; tunawaelewesha watu namna bora ya kutumia barabara na kuepuka na ajali. Kikubwa zaidi tumeshaweka ishara na alama za barabarani ambazo pia zinasaidia watu kuweza kujua namna ya kuepuka hizi ajali za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri tunakwenda Wizara ya Maji namwita Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa aulize swalii lake.

Na. 451

**Mradi wa Kutoa Maji Mto Simba hadi Longido**

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA** aliuliza: -

Je, ni lini Tarafa ya Enduimet pamoja na Vijiji vya ELerai, Tingatinga na Sinya vitaunganishwa na mradi wa maji kutoka Mto Simba hadi Longido ambao umepita katika maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Mbunge wa Jimbo la Longido kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji Longido kutoka chanzo cha Maji Mto Simba kulingana na miundombinu iliyopo unazalisha lita 2,160,000. Mradi huo kwa sasa unahudumia Mji wa Longido na Vijiji vya jirani vya Ranchi, Orbomba, Tingatinga pamoja na Mji mdogo wa Namanga na vijiji vya Kimokouwa na Eworendeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya maji kwa vijiji vya Tingatinga, na Sinya ni zaidi ya lita 500,000 kwa siku, na vinapata huduma ya maji kupitia miradi ya Magadini, Makiwaro na visima virefu vitatu 3 vilivypo maeneo ya Donyomali, Idonyo na Sinya. Vijiji vingine vya Tarafa ya Enduimet vinapata huduma ya maji kupitia skimu za maji ya Mtiririko ya Tingatinga Ngereyani, Larang'wa na Kamwanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2021/2022, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya kuboresha huduma ya maji katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido. Aidha, lengo la muda mrefu ni kutumia vyanzo vya uhakika vya maji ikiwemo kufanya upanuzi wa mradi wa kutoa maji Mto Simba hadi Longido.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kiruswa Mbunge wa Longido swali la nyongeza kwa ufupi.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo

mawili ya nyongeza. Lakini kabla ya maswali yangu niweke hii kumbukumbu kwa usahihi kabisa, kwamba kwanza nashukuru Serikali kwa kutapatia jamii ya Longido maji safi na salama kutoka Mto Simba ambayo mpaka sasa yamekuwa toshelevu katika Mji wa Longido ambako ni Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pia kwa sababu kazi inaendelea kuelekea Kimokouwa, Eworendeke na Namanga, na ni mradi ambao bado haujakamilika. Nashukuru pia kwa kuwa imefika Engikaret, lakini bado hayajafikiwa Kiserian na baadhi ya maeneo yaliyokusudiwa kama kitongoji cha Wasinyai na Yambaluwa Yambalua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza la nyongeza. Kwa kuwa mradi huu bado una hayo mapungufu ya kufikisha maji katika maeneo hayo;

Je, ni lini Serikali itakwenda kukamilisha huo mradi wa kufikia maji maeneo yote yaliyolengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa wananchi waliopitiwa na bomba hilo kutoka kule chanzo chake, waliopo kitongoji cha Emotong, ni kitongoji kikubwa sana ile *scheme* nyingine inayokwenda mpaka Larang'wa na Kamwanga haipitiki huko kabisa;

Je, ni lini watu wa Emotong, Tingatinga, a Engerian ambao nao waliahidiwa kwamba watapata matawi ya haya maji na bado hawajayapata watapata hayo maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Engineer Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nami nipende kupokea shukrani zake kwa sababu amekiri kazi kubwa ambayo Wizara tumeendelea kufanya katika jimbo lake; na huo tu ni mwanzo wa mageuzi makubwa ambayo wizara inaendelea kuyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa miradi hii tunatarajia kadri pesa tunavyoendelea kupata, na mwaka ujao wa fedha tutaendelea kuhakikisha hii miradi inakamilika. Hii ni kwa sababu lengo la Wizara ni kuona kwamba miradi inakamilika na wananchi wanapata maji safi na salama ya kutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitongoji cha Tingatinga na maeneo hayo mengine vilevile wao pia wapo kwenye Mpango Mkakati wa Wizara kuona nao wao pia wanakwenda kunufaka na maji safi na salama. Hivyo nikutoe hofu Mheshimiwa Mbunge kama ulivyoona kazi imeweza kufanyika kwenye maeneo mengine na maeneo haya pia kazi itakuja kufanyika na maji bombani yatapatikana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Wizara ya Maji, sasa namwita Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, Mbunge wa Kiteto aulize swali lake.

Na. 452

**Maji Safi na Salama Kupatikana kwa Asilimia 95 Vijijini na Mijini Kufikia Mwaka 2025**

**MHE. EDWARD O. KISAU** aliuliza: -

Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kuwa Wananchi wa Jimbo la Kiteto wananaufaika na Miradi ya Maji safi na salama ili waweze kufikia azma ya asilimia 85 na asilimia 95 Vijijini na Mijini ifikapo Mwaka 2025?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** aliibju: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita Mbunge wa Kiteto kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkao wa Manyara ni miongoni mwa maeneo kame nchini ambayo chanzo kikuu cha maji ni maji chini ya ardhi. Huduma ya maji ya uhakika katika Wilaya Kiteto kwa upande wa vijiji inapatikana vijiji 35 kati ya 63, sawa na asilimia 53 kwa mijini ni asilimia 44.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vijiji, Serikali imepanga kutekeleza miradi mitano au zaidi kila mwaka ili huduma ya maji ifike katika vijiji vyote 63 na kufikia lengo la asilimia 85 au zaidi. Kwa upande wa Mji wa Kibaya kwa mwaka 2021/2022, Serikali imepanga kutekeleza mradi ambaao utahusisha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji ambapo huduma ya maji itakayopatikana itakidhi mahitaji ya wananchi wa Kibaya kwa asilimia 95 au zaidi ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha huduma ya maji katika maeneo kame, Serikali itatekeleza mpango wa ujenzi wa mabwawa madogo na makubwa na ukubwa wa kati kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua na kuongeza uhakika wa upatikanaji wa maji wakati wote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Olelekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninashukuru sana kwa majibu mazuri sana ya Serikali; na nishukuru juzi tu wakati wa Mbio za Mwenge tulizindua miradi ya Wezamtima na kutembelea miradi mingine ya maji kule Nchinila. Pamoja na haya ninashukuru sana kwa majibu haya ambayo wananchi wangu wa Kibaya pale, na nniafurahi kusema watakuwa wamesikia majibu haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, ni lini sasa Serikali itajenga Bwawa la Dongo ambalo lipo kwenye mpango wa Mwaka huu wa Fedha 2021/2022. Lakini wakati huo huo pale pale Dongo tuna Miima Njoge unatiririsha maji; na kwa kuwa tanki ambalo limejengwa ni zamani sana, ni la mwaka 1965, na katika Vijiji vya Dongo na Chang'ombe wananchi wameongeza; ni nini kauli ya Serikali kuhusu kujenga tanki kubwa la maji; pengine la lita laki moja, laki mbili ili wananchi hawa waendelee kunufaika wakati wanasubiria bwawa hili la Dongo ambalo tunasuburia kwa hamu sana? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu wa Maji *Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mbunge wa Kiteto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipende kukushukuru kwa kukiri kazi kubwa ambayo imefanyika na hata Mwenge wetu wa uhuru umeweza kuzindua miradi ile. Lakini vilevile nipende kukujibu swali lako, kwamba ni lini bwawa la Dongo litafanyikwa kazi. Umeshajibu wewe mwenyewe kwamba mwaka ujao wa fedha tayari mpango mkakati umeuona uko pale hivyo tusubiri muda. Na kadri fedha itakavyokuja ndivyo kasi ya ujenzi wa lile bwawa itakuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuhusiana na hili bwawa lililojengwa miaka ya 1965 tunafahamu ongezeko la wananchi ni kubwa. Tayari tuna mikakati ya kuja kukarabati tanki hilo, lakini vile vile kuongeza matanki mengine kadri fedha tutakavyopata, na mwaka ujao wa fedha naamini tutakuja kufanya hizi zote. Lengo ni kuona wananchi wanapata maji safi na salama ya kutosheleza na wananchi wote wapate maji bombani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka swali la nyongeza.

**MHE: ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi nipate kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru Serikali kwa kutupatia fedha kwa ajili ya maji ya Mji wa Liwale. Hata hivyo mpaka leo *DDCA* wametutia changa la macho, ni mwezi wa sita huu hawajaja; na Mheshimiwa Waziri ameniambia kwamba kuna uwezekano tukachukua watu binafsi wakaanza kuchimba pale. Lakini nimewasiliana na Mhandisi anasema asilimia 30 ya fedha hizo tayari *DDCA* walishachukua na walishaingia mitini.

Je, ni lini *DDCA* watakuja kutuchimbia maji Wilaya ya Liwale?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuberi Kuchauka Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zuberi ni jana tu tumeongea na Mheshimiwa Waziri amekupa hayo maelekezo. Kwa hiyo nipende tu kuongeza pale alipoongea bosi wangu kama alivyokuhakikishia, pale *DDCA* wanapozidhiwa kazi basi watu binafsi tutawapa vibali ili waweze kuja kuchimba hivi visima. Na visima hivi mwaka ujao wa fedha ninaamini vitachimbwa na mambo yatakan vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na fedha iliyochukuliwa na *DDCA* fedha ikichukuliwa maana yake ni lazima kazi ije ifanyike. Kwa hiyo kwa ile asilimia ambayo wamechukua lazima watakuja kufanya hiyo kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi naomba kuuliza swali la

nyongeza. Kwa kuwa Mji Mdogo wa Matui Wilaya ya Kiteto una wakazi wengi na unaendelea kukua kwa kasi.

Nini kauli ya Serikali juu ya upatikanaji wa uhakika wa maji safi na salama kwa wananchi wa Matui pamoja na viunga vyake?

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa swali fupi, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia Mbunge wa Viti Maalum vijana kama ifuatayyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya ya Matui huko Kiteto nayyo ni mionganoni mwa maeneo ambayo Wizara imetoa jicho la kipekee kabisa. Tunafahamu kuwa ni maeneo ambayo watu wameongezeka sana, hivyo mwaka ujao wa fedha kila eneo tutalitupia jicho, na kwa eneo hili la Matui pia tutalipa kipaumbele.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa majibu. Sasa tunahamia Wizara ya Nishati, namwita Mheshimiwa Oran Manase Njeza Mbunge wa Mbeya vijijiini aulize swali lake.

Na. 453

### **Hitaji la Umeme wa REA - Mbeya Vijijiini**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

(a) Je, ni Vijiji vingapi vya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya vimepata umeme wa *REA II*, *Densification* na *REA III*?

(b) Je, ni lini vijiji vilivyobaki vitapatiwa umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijiji lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mbeya Vijiji ina jumla ya vijiji 140. vijiji 101 vina umeme ambao umepatikana kupitia miradi mbalimbali kama ifuatavyo;

*REA II* Vijiji 21; ujazilizi (*Densification*) vijiji 24; na mradi wa *REA* awamu ya tatu mzunguko wa kwanza vijiji 45. Vijiji 11 vimepatiwa umeme kupitia miradi inayotekelzwa na Shirika la Umeme nchini (*TANESCO*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kupeleka umeme katika vijiji 39 vilivyobaki ilianza mwezi Mei, 2021 na kazi hiyo, itakamilika ifikapo Disemba, 2022. Gharama ya mradi ni shilingi billioni 8.05.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Njeza swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipa swali la nyongeza; lakini vile vile, naomba niishukuru sana Serikali kwa kweli kwa kazi kubwa iliyofanya ya kusambaza umeme vijiji. Ninashukuru sana ya kwamba vijiji 39 vya mwisho sasa navyo kazi imeshaanza ili kukamilisha vijiji vyote vya Wilaya yetu ya Mbeya, Halmashauri ya Mbeya Jimbo la Mbeya Vijiji kupata umeme, nashukuru sana kwa hilo; ingawaje mkandarasi alipewa vijiji 32 kwa hiyo nitamuomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia ili kuoanisha hayo mahesabu yake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa mradi mkubwa wa Tanzania Zambia *Inter-Conektor* ambao unapita kwenye vijiji vya kata nane za Wilaya ya Mbeya Jimbo la Mbeya Vijiji. Inapita katika Kata za Ulenje, Inyala

Maendeleo, Itewe, Swaya, Igale, Iwindi na Bonde la Songwe. Wananchi waliopisha ujenzi wa *line* hii waliahidiwa kupatiwa fidia tangu mwaka 2018, lakini mpaka leo hii wanasubiria hakuna kinachoendelea, na imekuwa kero kwa vile waliambiwa wasifanye ujenzi wala maendeleo yoyote. Sasa ni lini wananchi hawa watapata fidia yao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kama unavyojuua kupeleka umeme vijijini ni kuchochaea uchumi, lakini kumekuwa na mkanganyiko wa tozo katika wateja wa *line* ya *three phase* na wateja wa *line ya single phase*. Wateja wa *line ya three phase* wanatozwa na TANESCO Shilingi 918,000 ambapo REA wanawatoza 139,000.

Je, Serikali ina mpango wa kuoanisha hizo tozo mbili ili kuchochaea huo uchumi vijijini na wananchi waweze kulipia laki moja na thelathini na tisa badala ya laki tisa na kumi na mbili? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Manase Oran Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake na shukrani alizozitoa kwa Serikali, na mimi kwa niaba yake nizipokee, kwamba Serikali imejitahidi sana kuhakikisha inapeleka umeme vijijini na katika maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nimuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba vijiji 39 ambavyo anavyo vyote vitapata umeme pamoja na kwamba inawezekana mkandarasi alipewa 32 vya kwanza. Pia niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba hata kama mkandarasi alipewa vijiji pungufu ya vile ambavyo uhalisia vimebaki, katika *survey* hii ambayo tumewatuma wakandarasi wafanye kwenye maeneo yetu watahakikisha

na vile vijiji vingine ambavyo vilibaki au viliachwa vinachukuliwa katika kazi zao na katika *adendum* za nyongeza za kazi tutakazo wapatia, watavichukua vijiji vyote na kuvifanyia kazi. kwa hiyo nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ufuatiliaji wake umefanikiwa na wengine pia umeme utapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swalii la fidia itakayolipwa kwenye mradi mkubwa wa kuunganisha umeme wa *grid* kutoka Iringa kwenda Mbeya, Tunduma mpaka Sumbawanga, takribani kilomita kama 622, kazi hiyo ya umbembuzi yakinifu imefanyika imekamilika na sasa makabrasha ya ulipaji wa fidia ndiyo yanawasilishwa sasa kwenye ofisi zetu kwa ajili ya uhakiki na kuweza kulipa fidia hiyo. Kwa hiyo bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri aliwasilisha hapa juzi imetenga kiasi cha kuanzia, zaidi shilingi bilioni moja kwa ajilli ya malipo ya fidia ya eneo hilo, na tutaanza kulipa fedha hiyo kuanzia kwenye mwezi wa kumi na kuendelea kwa ajilli ya kupisha sasa ujenzi wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swalii la pili, niombi kutoa maelezo na maelekezo kwa watumishi wenzetu. Serikali imesikia kilio cha Watanzania na tayari ilielekeza kwamba umeme katika maeneo yote utaunganishwa kwa shilingi 27 kwa umeme mdogo. Kwenye maeneo yetu ya vijiji Serikali imetoa msamaha wa kuunganisha *lineya* nguvu kubwa *three phase* kwa gharama ya shilingi 139,000 tu. Kwa hiyo, ninawaelekeza watumishi wenzetu wa *TANESCO* kwamba maeneo yote ya vijijini ambapo eitherni *TANESCO* kapeleka umeme au *REA* imapeleka umeme, gharama ya kuunganisha umeme wa *three phase* ni shilingi 139,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo shilingi 912,000/= ni kwenye maeneo mengine ya mijini ambapo mradi wa *REA* wowote ule haujafika. Kwa hiyo ielewewe wazi kabisa, waheshimiwa Wabunge tunaomba tusaidiane katika usimamizi wa hili. *TANESCO* akiwa analeta umeme au *REA* analeta umeme mkubwa gharama yake ni shilingi 132,000 kwenye maeneo yetu ya vijijini. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Sasa namuita Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga Mbunge wa Makambako aulize swali lake.

Na. 454

**Wananchi Kulipwa Fidia Eneo la Umeme wa  
Upepo Makambako**

**MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Je, ni lini wananchi wa Makambako watalipwa fidia baada ya maeneo yao kuchukuliwa na Serikali kwa ajili yakuzalisha umeme wa upepo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Byabato, karibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudzi za kuongeza upatikanaji wa umeme nchini kupitia vyanzo mbalimbali, eneo la Kijiji cha Majengo Jijini Makambako, limebainika kuwa na uwezo wa kuwekewa miundombinu ya kuzalisha umeme kupitia nishati ya upepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakamilisha taratibu za kuingia Mkataba wa uzalishaji wa umeme wa upepo na Mwekezaji Binafsi aitwaye *Sin Tan*. Kwa mujibu wa Mkataba huo, fidia kwa wananchi wa maeneo yatakayotumika kuzalisha umeme huo, italipwa na mwekezaji huyo, katika kipindi cha kuanzia mwezi Agosti, 2021 na Julai, 2022 ambacho ni kipindi kinachotarajiwa kutekelezwa kwa mradi huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Nina maswali madogo mawili. Swali la kwanza; pamoja na majibu mazuri ya Serikali yenye kutia matumaini, kwa wananchi wanaopitiwa na mradi huo, wananchi wa eneo la Kivavi na eneo la Majengo na kwa sababu, wamesubiri kwa muda mrefu sana zaidi ya miaka saba na huu sasa tunakwenda mwaka wa nane. Je, Serikali itakuwa tayari kusimamia kama ambavyo wamesema hapa, ndani ya mwaka 2021/2022 na kuhakikisha kwamba, wananchi hawa watalipwa kama ambavyo amesema kwenye jibu la msingi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali itasimamia namna ya kuwalipa fidia wakati wa kuwalipa utakapofika? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Byabato, karibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, kwa pamoja, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudzi za Serikali za kuhakikisha inaongeza wigo wa umeme, tunazalisha umeme kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na maji, mafuta na gesi ambayo imezoleka. Hata hivyo, tunafanya vitu vinavyoitwa *energy mix*, ambavyo ni vile vyanzo jadidifu tunaviita *renewables* ambayo kuna upepo, jua na ile wanayoita joto ardhi. Sasa, kwenye eneo la Makambako imeonekana tunaweza tukapatata pale, umeme kwa kutumia upepo katika hicho Kijiji cha Majengo tulichokisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatarajia kupata kama megawati 1,179 kutoka kwenye hizo *renewables*. Sasa, tumewakaribisha wawekezaji binafsi ili waweze kuwekeza katika eneo hilo ili isaidiane na Serikali katika kupatikana kwa

umeme huo. Huo mkataba nilioutaja unaelekeza kwamba, yule mwekezaji binafsi anayekuja kuwekeza katika eneo hilo, ye ye ndiye ata-*acquire* ardhi na kuweza kulipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, nipende kutoa *commitment* ya Serikali, Mheshimiwa Deo amefuatilia sana kwa muda mrefu madai haya na malipo haya, nimhakikishie kwamba, tumefikia mwisho wa makubaliano na kutafuta wawekezaji katika eneo hili na Serikali itasimamia kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuhakikisha kwamba, mkataba unaingiwa katika kipindi hicho kilichotajwa. Pili, kuhakikisha kwamba, kila yule anayetakiwa kulipwa fidia analipwa fidia stahiki katika eneo lake, kulingana na hali halisi na sheria inavyoelekeza katika maeneo hayo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Deo kwamba, wananchi wa Makambako wamefanikiwa na naendelea kuwasimamia vyema na kile wanachokistahili kukipata, watakipata kwa wakati. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Tunawashukuru Waheshimiwa Mawaziri kwa majibu mazuri. (*Makof!*)

Sasa, hapa nina matangazo pamoja na kukaribisha baadhi ya wageni.

Wageni waliopo jukwaa la Spika, wa kwanza ni Mtaalam wa Mawasiliano kutoka *UNICEF* na Mratibu wa Ushirikiano kati ya Bunge na *UNICEF*, Ndugu Sia Ledama Nkoma. Karibu sana, Mratibu wetu wa Mawasiliano. (*Makof!*)

Pili, wapo wageni 56 wa Mheshimiwa Naibu Spika, amba ni Wenyeviti wa Umoja wa Vijana wa CCM wa Wilaya mbalimbali nchini, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM Dodoma Mjini, Ndugu Said Kasote; Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM Mbeya Mjini, Ndugu Ramadhan Shekaoneka; na Mwenyekiti wa Umoja

wa Vijana wa CCM, Ndugu Masaga Paul. Wenyeviti wetu wa Umoja wa Vijana wa CCM, karibuni sana kwenye Bunge letu. Nyinyi ndio jeshi la kuhimiza na kusimamia maendeleo kwenye maeneo yenu, lakini mkiwa mnasimamia ajenda ya kusaidia vijana wa nchi hii. (*Makofi*)

Pia, tunao wageni wengine 42 wa Mheshimiwa Naibu Spika, Wanambeya Afya Kwanza *Jogging Club* wakiongozwa na Ndugu Jacob Madeje. Karibuni sana Dodoma, karibuni sana Bungeni. Mheshimiwa Mbunge wenu, Naibu Spika wetu, anaendelea kuchapa kazi. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Wapo wageni wengine 45 wa Mheshimiwa Spika, ambaao ni Jumuiya ya Utoto Mtakatifu kutoka Jijini Dodoma, wakiongozwa na Ndugu Leticia Masuka. Karibuni sana vijana wetu, watoto wetu. (*Makofi*)

Wageni sita ni wa Mheshimiwa *Engineer Msonge Kasekenya*, Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Ndugu Joseph Mkude. Karibu sana. Karibu sana Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na timu yako. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Mussa Zungu, kutoka Ilala Dar es Salaam, Ndugu Salehe Omary. Ahsante Mheshimiwa Omari. (*Makofi*)

Wageni 20 wa Mheshimiwa John Sallu Mbunge, ambaao ni Wanachama wa Mkata *Fitness Club* kutoka Handeni Vijijini, wakiongozwa na Ndugu Husein Saguti. Wageni wa Mheshimiwa Sallu, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 10 wa Mheshimiwa Rashidi Shangazi, Mbunge ambaao ni *Wana-jogging* kutoka Mkoa wa Tanga, wakiongozwa na Ndugu Hassan Shedaffa. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Shangazi, Katibu wetu hapa Bungeni wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Tunao wageni saba wa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kagera, ambaao ni Wenyeviti wa Umoja wa Vijana

wa CCM, Mkoa wa Kagera, wakiongozwa na Ndugu Ferdinand Banyenzaki, karibuni sana Umoja wa Vijana wa CCM kutoka Kagera. Tunasikilia faraja kuwa nanyi hapa ndani leo. (*Makofii*)

Tunao pia wageni 38 wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) na wenyehi wa Wilaya ya Arumeru, Mkoani Arusha. Karibuni sana, vijana wetu na Dkt. Pallangyo yuko anajenga hoja, kwa ajili ya maendeleo ya watu wa Arumeru Mashariki. (*Makofii*)

Tunao wageni 24 wa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, ambao ni Madiwani wa Iringa, wakiongozwa na Mstahiki Meya, Ndugu Ibrahim Ngwada. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani wetu kutoka kwenye ardhii ya Mkwawa, mwendelee kujifunza kwenye Bunge letu. (*Makofii*)

Pia, tunaye Mgeni wa Mheshimiwa Yustina Rahhi, Mbunge kutoka Manispaa ya Dodoma, Dkt. Bertha Lyimo. Karibu sana Dkt. (*Makofii*)

Tunao wageni 58 wa Mheshimiwa Jerry Silaa, Mbunge ambao ni wanafunzi na Walimu wa Shule ya St. James ya Ukonga Jijini Dar es Salaam, wakiongozwa na Meneja wa Shule, Ndugu Mercy Mrisho. Tunafurahi kuwa nanyi hapa Bungeni, tunaamini mtajifunza na kesho nyie ndio mtakaa kwenye viti hivi. (*Makofii*)

Wageni 11 wa Mheshimiwa Jacqueline Kainja ambao ni wajasiriamali yaani (Malkia wa Nguvu) kutoka Jijini Dodoma, wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu Timina Sawe. Karibuni sana Malkia wa Nguvu, si mmewaona (Malkia wa Nguvu)? (*Makofii*)

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, ambaye ni binti yake kutoka Kibaha Mkoani Pwani, Ndugu Vanessa David. Karibu sana Dodoma binti yetu. (*Makofii*)

Mgeni wa Mheshimiwa Agness Hokororo, Mbunge ambaye ni Mkurugenzi wa Taasisi ya *Anuflo* Ndugu, Flora Njelekela. Ameshasimama ndio yule pale, karibu sana. (*Makofii*)

Wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, ni wanafunzi 60 na Walimu watano kutoka Shule ya Nala ya Jijini Dodoma, ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake, wakiongozwa na Mwalimu Hadija Kapombe. Karibuni sana Dodoma, kwenye Bunge letu. (*Makofii*)

Pia, tunao wageni wa Mama Shally Raymond, ambao ni Nelfin Msia Raymond ambaye ni binti yake na Ali Othman Mohamed kijana wa rafiki yake. Karibuni sana. (*Makofii*)

Pia, kuna matangazo kutoka kwa Katibu. Moja, Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa kushiriki matembezi ya Hedhi Salama, yatakayofanyika siku ya Jumamosi tarehe 19 Juni, 2021, kuanzia saa 1.30 asubuhi, matembezi yataanzia katika Viwanja vyta Bunge kuelekea Nyerere Square. Mgeni Rasmi atakuwa ni Mheshimiwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano Tanzania, Dkt. Tulia Ackson, ambaye nafikiri na nyote leo mmewwona hata vazi lake rasmi zuri kabisa, kapendeza kweli kweli. Kwa hiyo, tunaomba m jitokeze kwa wingi siku hiyo. (*Makofii/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge wanawake, vile vile mnajulishwa kuwa kesho tarehe 19 Juni, 2021 saa 4.00 asubuhi, kutakuwa na semina kwa Wabunge wanawake wote. Semina hiyo itafanyika katika Ukumbi wa Takwimu, wote mnaombwa kuhudhuria. Tangazo hili ni la Mwenyekiti wa Wabunge Wanawake. Kwa hiyo, naamini pengine maandalizi yote yameshakamilika yanawasubiri nyie ili muweze kushiriki hiyo kesho. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kwamba, Jumamosi tarehe 19 Juni, saa 10.00 jioni, kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, kutakuwa na mechi za kirafiki za mpira wa miguu na pete, kati ya Bunge *Sports Club* dhidi ya Chama

cha Waandishi wa Habari Tanzania (*TASWA*). Kwa hiyo, mnaombwa Wabunge na watumishi wote kujitokeza kwa wingi, kwa ajili ya pambano hilo na huwa mara nyingi Wabunge huwa tunashinda, ndio utaratibu wetu. (*Makofii*)

Ninalo tangazo hapa kutoka kwa Mheshimiwa Japhet Hasunga, ambaye anaomba tuwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wenye Taaluma ya Uhasibu kwamba, leo Ijumaa saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao kifupi cha kujadili masuala mahususi sehemu ya *Canteen*. Kwa hiyo, Wabunge wote wenye taaluma hiyo, waweze kufika.

Pia, kuna wageni 15 wa Mheshimiwa Mavunde Anthony Peter, ambaao ni *Mothers Club*, naomba tuwatambue na tuwakaribishe. (*Makofii*)

Vile vile kuna wageni 60 wa Mheshimiwa Rashid Abdalla na Mheshimiwa Mariam Azan kama wapo hapa pia. Ahsanteni sana. (*Makofii*)

Sasa tumefika mwisho wa kipindi chetu cha awali. Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Hapa ninayo orodha, mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, wakati huo Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo na Mheshimiwa Ameir Abdallah wanajiandaa.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchukua nafasi hii kwanza, kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi. Pili, kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kuamka salama na kuanza kufanya kazi za kutumikia tena Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya yote nitoe pongezi maalum za sura ya bajeti. Nasema za sura ya bajeti kwa sababu, kwa hakika bajeti hii imetudhihirishia mambo mawili makubwa. Kwanza, imetudhihirishia kwamba, Serikali hii ya CCM ni Serikali sikivu. Pili, imetudhihirishia kwamba, Serikali inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wetu ni Serikali ambayo imekusudia kabisa kazi iendelee. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sifa hizi hazipatikani kwa kusema tu, zinapatikana kwa mambo tunayoyaona kwa sababu, Serikali sikivu inazo sifa zifuatazo: Moja ni Serikali inayowasikiliza wananchi; Pili, Serikali inayowasikiliza Wabunge; Tatu, Serikali inayoshaurika; Nne, Serikali ambayo ipo tayari kujikosoa; na Tano, Serikali inayotekeleza mambo kwa wakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya mambo yakiwepo ndio unasema hii Serikali sikivu na katika bajeti hii unaweza ukayaona haya mambo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kitendo cha kupunguza faini za makosa ya barabarani kwa bajaji na bodaboda, kutoka Sh.30,000/= mpaka Sh.10,000/= ni kuwa Serikali hii ni sikivu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kitendo cha kuhakikisha kwamba, katika bajeti hii posho za Waheshimiwa Madiwani, ambao ni wasaidizi wa karibu wa sisi Wabunge, zitakuwa zinalipwa sasa kutoka TAMISEMI badala ya Halmashauri zao. Hiki kitendo kinaonyesha Serikali hii ni sikivu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kitendo cha kuweka posho maalum kwa Watendaji wa Kata na Makatibu Tarafa,

ili waweze kupata uwezo wa kuzifanya kazi zao vizuri, kinaonyesha Serikali hii ni sikuvi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kitendo cha kuyatafutia ufumbuzi matatizo ya barabara zetu zinazosimamiwa na TARURA, maji na kushughulika na maboma ya shule zetu, haya yote yanaonyesha Serikali hii ni sikuvi na kwamba, lazima tutoe pongezi maalum kwa Rais wetu na Serikali kwa ujumla, kuonyesha kweli kazi inaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, ningependa kuwatoa wasiwasi Wabunge wenzangu, hasa ambao wamekuwa na wasiwasi au wakiwa na maoni tofauti kuhusu kodi ya majengo, kwamba, itozwe wapi na mahali gani? Nataka niipongeze kabisa Serikali wamelenga, wametafuta mahali pazuri ambapo kodi itapatikana na ambapo hapawezhi kuwa na maumivu kwa mtu mmoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri katika hili tukafahamu kwamba, kodi zote na hasa zilizo nyingi, lazima mwisho wake zilipwe na mtumiaji, maana hata ukisikia kodi imewekwa kwenye mafuta, unaweba ukafikiri analipa mwenye gari, si kweli hiyo. Mwenye gari ataenda kununua mafuta tu, lakini baadaye abiria akipanda gari hilo atalipa hiyo kodi ya mafuta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kodi zote hatimaye hulipwa na mtumiaji kwa hiyo, kama nyumba imejengwa na mwenye nyumba yupo, aidha, anakaa kwenye nyumba hiyo ina umeme au hakai kwenye nyumba hiyo kuna mtu mwingine anakaa na huyo ndiye anayelipa kodi hiyo ya majengo, iko sahihi, wala hakuna tatizo lolote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni niliungana na Rais wetu, kushuhudia utiaji saini wa mikataba mitano kule Mwanza ya ujenzi wa meli ambazo zitatoa huduma na kuchochea uchumi katika Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi katika Ziwa Tanganyika ni wanufaika, maana kuna meli mbili; moja ya abiria ambayo itabeba abiria 600 na mizigo 400 ipo katika mkataba huu ambayo itaanza kujengwa; na nyingine ni ya mizigo. Hapa narudia kuipongeza Serikali, maana nimesema hapa Bungeni katika Mpango na hata katika Wizara mbalimbali ikiwemo Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, nilisema kuhusu suala la kuhakikisha tunachangamkia fursa ya soko kubwa la *DRC Congo*. Kwa hiyo, meli hizi zitakuwa kichocheo kikubwa cha uchumi cha kufungua mlango na kuongeza wigo mkubwa wa biashara baina ya sisi na *DRC Congo*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mniruhusu vile vile baada ya kusema Serikali hii Sikivu, niwakumbushe mambo ambayo hamjayasikia vizuri. Maana ingekuwa ni binadamu ungeweza ukasema, kama mtu ana masikio mawili labda ungesemea siklo la kushoto, la kulia labda liliinglia maji hakusikia vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia haya mambo, nimeshayasema na sasa nataka niyarudie. Uchumi wa nchi yetu unategemea sana uimara wa sekta binafsi. Sekta binafsi sasa hivi imebeba mizigo mikubwa miwili; tukiitua mizigo hii sekta binafsi itatusaidia sana katika kukuza uchumi. Mzigo wa kwanza ni riba za mabenki. Maana ilisababisha hapa mpaka nijiteue mwenyewe kuwa balozi wa kutetea riba za mabenki. Riba za mabenki endeleeni kulitazama jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzigo wa pili ni ulipaji wa madeni ya Serikali kwa wakandarasi wa ndani. Nataka nikwambie, hali ni mbaya. Kuna watu sasa hivi hapa wakipiga simu napata shida kupokea. Mmojawapo ni mpiga kura wangu mmoja anaitwa Raymond Dabiegese, yupo kule Kigoma, anaidai *TBA* (*Tanzania Building Agency*). Amewa-supply vifaa, duka lenye thamani ya mtaji kama wa shilingi milioni 100, unakwenda kuchukua vifaa vyaa shilingi milioni 40, halafu unafika mahali miaka miwili hujalipa. Unamuua huyu mtu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa kupitia nafasi hii niseme, tumesaini mikataba na hawa wakandarasi kwa ajili kutengeneza meli hizi. Naiomba Serikali ichukue tahadari sana katika kuwasimamia hao wakandarasi kufanya kazi zetu. Najua Serikali kabla ya kutoa kazi, inafanya kitu kinaitwa *due diligence*, kuangalia uwezo wa kitaaluma na kifedha wa haya makampuni kufanya kazi zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa tunalo tatizo, kampuni iliyopewa kandarasi ya reli yetu ya kisasa, inakabiliwa na madeni makubwa ya wazabuni wa ndani wadogo iliyowapa kazi. Sijui hili kama mnalijua! Serikali inawalipa wao kwa wakati, lakini wao wale watu waliowa-*sub-contract* kazi ndogo ndogo hawawalipi. Sasa hivi wanadaiwa zaidi ya shilingi bilioni 14. Baadhi ya wadeni walikuwa hapa niliwaunganisha na Naibu Waziri wa Ujenzi ili waone jinsi ya kuwasialdia. Ndugu zangu imetokea baadhi ya makampuni haya yamefanya kazi kwenye nchi nyingine yakamaliza mikataba yake, yakamaliza miradi, yakawaacha watu wa nchi hizo, Wakandarasi wadogo wadogo wa nchi hiyo, wazabuni wadogo wadogo wanadai madeni; nchi mojawapo ni Ethiopia. Wametekeleza miradi lakini wameacha makovu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali na hasa Hazina mnapotoa fedha, ikiwezekana hata katika mikataba yenu, hawa wakandarasi wa kutoka nje mnapowapa kazi, waoneshe wao wanaingia mikataba na wazabuni wadogo wadogo wa ndani ya nchi; mikataba ile mwenayo na mjue kama wale wazabuni wanaowapa, wanalipwa kwa wakati. Vinginevyo ninyi mnawalipa lakini wao hawawalipi. Hilo jambo litafika mahali litasaidia miradi kutekelezwa lakini litarudi tena kuwabebesha mizigo watu wa sekta binafsi katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla nataka niseme kwamba sisi Wabunge naamini kama nilivyowasikia wenzangu wengi wanasema, tumeridhishwa sana na bajeti hii na kwa kweli napenda kutamka rasmi kwamba naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwita Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema ambaye amenipa afya njema na kuweza kusimama kwenye hili Bunge Tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Fedha pamoja na viongozi wote wa Wizara kwa namna ambavyo wameiongoza na kusimamia bajeti hii ya Taifa letu la Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu ambaye ni mwanamke wa kwanza kuwa Rais katika Taifa letu hili la Tanzania. Mheshimiwa Rais wetu ni mama msikivu, mwenye busara, ana hekima, ni mama ambaye anastahili sifa zote. Napenda kuwashukuru Watanzania wote kwamba wamemkubali sana mama tangu pale ambapo ameapishwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia bajeti hii na kuipongeza sana vile ambavyo imeandalisha hasa kwenye kipengele cha vijana wetu wa bodaboda. Naipongeza sana kwani wameondola mzigo mkubwa sana maana faini ya shilingi 30,000/= ilikuwa ni kubwa sana. Pamoja na kuipongeza kwa kazi nzuri hii waliyoifanya, napenda sana kuishauri pia Serikali, vijana ni nguvu kazi ya Taifa, tunawategemea sana na tunawapenda. Napongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwani ilifanya utaratibu wa kuondoa viroba ambavyo viliendelea kulinda uhai wa vijana wetu wa bodaboda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali kwa yafuatayo: kuhusu watu wa Usalama wa Barabarani, nilikuwa napenda kusimamia haya. Vijana wetu wa bodaboda kama nilivyoanza kwa kusema tunawapenda, hatutaki kuwapoteza. Naomba sana ufuatiliaji wa sheria na

taratibu za kupita barabarani hizi bodaboda zetu. Bodaboda zilizo nyingi zinapita barabarani zikiwa hazina taa ya breki ya nyuma ambayo inaonesha kwamba ile ni bodaboda inapita. Pia usiku wakati fulani unapishana na bodaboda haina taa yoyote, ukizingatia zenyewe hazina sehemu ya kuweka *reflector*. Sasa hiyo ni hatari sana ambayo inaweza kupoteza uhai wa vijana wetu hawa wa bodaboda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Jeshi la Usalama wa Barabarani kuwaita vijana wa bodaboda kuweka vikao na wao kuwaelimisha, kuwapa semina, namna ambavyo sheria za barabarani zinavyotakiwa kuwa. Naliongea hili maana kipindi cha kwanza bodaboda zilivyokuwa zinaanza, kulikuwa na utaratibu; wanakuja wilaya kwa wilaya, wanakalishwa vikao vijana wa bodaboda kuwapa elimu. Hapa katikati bodaboda zimeingia kwa wingi sana, sijawahi kuona semina inafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naomba tuzijali sana afya za hawa watoto wetu. Hawa vijana hawavai sana *helmet* ambayo inazua kupasuka kwa kichwa endapo watapata ajali. Pia kuna kitu kinaitwa *chest coat* la kuziba kifua, havijazingatiwa kabisa. Vijana wengi wanaendesha bodaboda bila kukinga kifua. Sasa imeanza kuleta athari ambapo hofu yangu tutapoteza vijana wengi katika Taifa letu hili Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewashuhudia vijana wanne ambao waliathirika na mapafu. Wengine walifanyiwa upasuaji wakapona, lakini wawili walipoteza maisha. Sasa hapo ni hao nimefanikiwa kuwaona, ambao hatujawaona! Hili nalionna ni tatizo kubwa sana ambalo tunatakiwa tuwasimamie vijana wetu wa Taifa hili la Tanzania. Pia napenda kuishauri Serikali, naipongeza kwamba wamepunguza hizo faini, lakini vituo vingi vya Polisi vina bodaboda nyingi sana. Nilikuwa naomba sana Serikali yetu hii ni sikivu, hao watu ambao bodaboda zao zimekamatwa wawaruhusu kwenda kufuata bodaboda zao ambazo hazina makosa ya jinai wakalipe faini ya hiyo hiyo shilingi 10,000/=.

(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, wakati fulani nilikuwa nimechangia kuhusu elimu kwa ajili ya mlipa kodi wa Tanzania. Naomba sana, narudia kusema, elimu ya mlipa kodi wa Tanzania ni muhimu sana. Naomba kwa mara nyingine, elimu itolewe kuanzia Shule za Msingi, Sekondari, Vyuo na Vyuo Vikuu ili vijana hawa wanapokua siku zinavyozidi kwenda, inakuwa inawajenga kwamba kulipa kodi ndiyo uendeshaji wa Taifa letu ya Tanzania. Hivyo napenda sana kuliombea hili lizingatiwe. Naomba sana hawa viongozi wa *TRA* kuweka mikutano na vikao na wafanyabiashara kuwapa elimu na semina ili wasione kwamba wanaonewa katika kulipa kodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongee lifuatalo; kipindi cha Awamu ya Tano, naomba sana mpango na hali ile ya Awamu ya Tano iendelee hata hii Awamu ya Sita. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan. Sisi ni wanawake, naomba sana kasi ile ile iliyokuwa ya Awamu ya Tano iwe ni hiyo hiyo mpaka kipindi hiki cha Awamu ya Sita. Ofisi zote za Umma za Serikali zinaongozwa kwa kutumia llani ya Chama cha Mapinduzi na ofisi zote zinazo. Naomba Watumishi wa Umma tusilegelege, ile kasi na mori ya kufanya kazi kama ilivyokuwa Awamu ya Tano iwe hivyo hivyo na awamu hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi baada ya Bunge la Bajeti hili kwisha narudi Mbeya, naomba ofisi vile ambavyo alikuwa akijituma akijihimu asubuhi kwenda kazini na iwe hivyo. Nitapita maofisini kuangalia kama mambo yanakwenda sawa. Naomba sana, vile ilivyokuwa, mtu kama hajafika ofisini kwa wakati, maana yake kipindi cha nyuma ilikuwa tukifika unasubiri, mtu anaambiwa bosi sasa hivi ametoka amekwenda *breakfast*. Unasubiri, ikifika saa 5.00 anasema hajarudi, basi nifanye kazi mbili tatu, unarudi saa 8.00, wanasema ooh, amekwenda *lunch*. Naomba hilo lisirudiwe tena . Vile ilivyokuwa Awamu ya Tano na iwe hivyo mpaka sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba sana; amani na upendo uliokuwepo Awamu ya Tano uendelee na sasa.

Maana tumesikia sasa vibaka wanaanza, wizi wizi unaanza. Tanzania inajengwa na sisi wenyele Watanzania. Haya ninayoongea ninamaanisha. Nalipenda sana Taifa letu la Tanzania, nawapenda sana Watanzania wote na ninaomba amani. Utendaji kazi ndiyo iwe ngao yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir na wakati huo huo Mheshimiwa Maryam Omar Said, Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, wanajandaa.

**MHE. AMEIR ABDALLA AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba Mbingu na Ardhi, ambaye leo ameniwezesha kupata afya njema nami kuwa mionganini mwa Wabunge watakaochangia hotuba hii ya bajeti ya mwaka 2021/2022. Napenda kumpungeza sana Rais, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan pamoja na Waziri wa Fedha na Naibu wake, kwa bajeti hii ambayo imeweza kupanga matumizi yake kwa kuyapa kipaumbele maeneo muhimu ambayo yanakwenda kukuza uchumi wa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo, bajeti hii haijaacha pengo hata moja. Hii ni bajeti ya wananchi, kwa maslahi ya wananchi na kwa neema ya wananchi wa Tanzania wote. Bajeti hii imegusa wananchi wote; imegusa wakulima, wavuvi, wajasiliamali, watu wa makundi maalum, walimu, waendesha bodaboda, akina mama kwa asilimia kubwa sana, mama ntilie na kadhalika. Kwa hiyo, naipongeza sana bajeti hii kwa asilimia kubwa sana na Inshaallah Mungu atatuweza kwamba Taifa letu la Tanzania litapiga hatua kubwa katika maendeleo ya uchumi katika sekta mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nitachangia katika maeneo machache sana kwa sababu maeneo mengi Waheshimiwa Wabunge wameyazungumza kwa ufanuzi

mzuri na kutoa mapendekezo mazuri, na ushauri mzuri ambao una manufaa makubwa kwa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mimi nitatoa ushauri nikijikita zaidi kwenye ongezeko la kodi katika suala zima la utalii wa watu wenye mahitaji maalum; vile vile nitaongea kuhusu suala la umuhimu wa kuwekeza viwanda vyetu hususan katika suala la mbolea na jambo lingine ni suala la ajira kupitia lugha sanifu ya Kiswahili na mwisho nitazungumzia kuhusu mahusiano mazuri baina ya sekta ya kilimo na sekta ya viwanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya utalii kuna jambo hatujaligusa kwa undani zaidi na tumeliacha kidogo, lakini kama Serikali italitilia mkazo na kulipa kipaumbele suala hili basi litasaidia sana kuongeza thamani na ongezeko la mapato katika utalii wetu. Nalo ni suala la kujikita katika utalii wa watu wenye mahitaji maalum. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wenye mahitaji maalum sasa hivi duniani wanafika takriban bilioni tatu. Ni robo tatu nzima ya *population* ya watu duniani. Kwa maana hiyo, Serikali kama tutajikita zaidi huku, basi Tanzania itakuwa ni nchi ambayo inapokea watalii mbalimbali duniani katika kundi hili na kwa asilimia kubwa itaongeza thamani kubwa ya pato la nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kukibidhaisha na kufanya lugha ya Kiswahili kama ni sehemu ya ajira. Kiswahili kinapaa duniani; Kiswahili kinasomeshwa katika Vyuo Vikuu mbalimbali duniani hivi sasa, lakini cha kushangaza maeneo mengine, Wazungu kwa Wazungu ndio wanafundisha hicho Kiswahili kwa sababu sisi hatujapanua zile fursa za kufika katika hayo maeneo mbalimbali tukakieneza Kiswahili na walimu wetu ambao wanemosha Kiswahili Tanzania kule Zanzibar na Tanzania Bara wakapata fursa hii kwa undani. Kwa hili sasa, namwomba sana Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi (ameshageuka) ambaye ni Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, atutengenezee mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sana, nimekosea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Waziri anahusiana na mambo ya Nje, aweze kututengenezea mazingira kupitia balozi zetu ambazo zinatuwakilisha nchi za nje. Kila balozi atengeneze fursa za lugha ya kishwahili kwa watanzania jamani, naomba sana tusaidie sana kwa kila balozi hata kama hakuna mazinga hayo lakini atengeneze kuhakikisha kwamba walimu wanaofundisha kiswahili Tanzania wanapata fursa katika balozi zetu hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine napenda kuhangia katika sekta ya maendeleo ya kilimo na viwanda, hatuwezi kuendelea katika sekta ya viwanda bila ya kufanya mageuzi na mapinduzi ya sekta ya kilimo. Bajeti hii inakuja na mageuzi hayo, bajeti hii imeelekeza wakulima wazilishe kwa wingi mazao ya biashara na mazao ya chakula, tukizalisha kwa wingi mazao ya chakula kwa wingi, maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba tutaongeza *population* ya idadi ya watu, na tukiongeza *population* na idadi ya watu maana yake tutakuwa na soko la uhakika la ndani ya nchi na bidhaa zetu zitauza ndani ya nchi na nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nilizungumzie katika suala la kuwekeza katika viwanda vya mbolea. Tanzania tumejaaliwa kuwa na aina ya madini fulani ambayo yanatumika katika kutengenezea hizi mbolea ambazo nchi nyengine hakuna, na madini haya tukiyatumiwa viwili ambayo yanatumiwa katika mikoa miwili tu, basi ni vyema tukawa na madini haya ambayo yanatuwezesha kuzalisha mbolea zetu sisi wenyewe, na kuondoa ule utegemezi mkubwa wa kuzalisha au kuagiza mbolea kutoka nchi za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na mbolea zetu wenyewe hapa nchini, basi sekta ya kilimo itakuwa na kuimarika kwa hali ya juu zaidi. Lingine niipongeze sana bajeti hii na Serikali kwa ujumla, kwa kuondoa tozo ya nyasi bandia, jambo hili linaisababishia nchi yetu kukuza sekta ya michezo, hususan mchezo wa mpira wa miguu, na leo hii nataka *declare interest*, kwamba mimi ni mfuasi wa Simba tangu miaka 12. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa bajeti hii ya kaka yangu Mwigulu Nchomba, bajeti ya wananchi, kwa maslahi ya wananchi, kwa ajili ya wananchi, natangaza rasmi ni mwana Yanga rasmi. Natangaza rasmi kwamba i leo ni mwana Yanga rasmi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwamba, aah! Ukitoa taarifa unanitatiza kidogo niache. Eneo lingine ni kwamba tuna miradi ya kimkakati na nashukuru kwamba mama bajeti imetuhakikishia kwamba hakuna mradi wa kimkakati hata mmoja utakaosita, miradi yote ya kimkakati itaendelezwa, namshukuru mama na naishukuru bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri hapa katika miradi ya kimkakati, tuwekeze rasilimali watu ambao wataweza kulendesha vizuri miradi hii, lazima tuhakikishe tunasomesha vijana wetu, na tunasomesha raia wetu wa Tanzania katika zile sekta au taaluma ambazo zina ugumu ndani yake, ili kupunguza utegemezi wa kuajiri wataalam kutoka nje ya nchi mara kwa mara, na tuwe na waalamu wetu kwa asilimia zote ikiwezekana kama siyo asilimia 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naipongeza sana naiunga mkono bajeti hii na ninaimani leo na mimi nitaalikwa chako ni chako, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, namuita Mheshimiwa Maryam Omar Said.

**MHE. MARYAM OMAR SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia bajeti iliyopo Mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniamsha mzima wa afya na kuweza kusimama hapa leo. Pia niipongeze Serikali kwa kuleta bajeti nzuri ila bado ninahofu na wasi wasi mkubwa, kila

ninapoisoma bajeti hii nikiangalia na bajeti zilizopita, kiukweli Napatwa na wasi wasi mkubwa mno, kwa sababu ni tayari mara nyingi sana wananchi kubwa wanadolalamikia ni kuitisha bajeti zetu, ikisha baadaye zikatushinda njia tukawa hatufikii kile kiwango. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nitachangia katika maeneo mawili makubwa. Niishukuru bajeti hii ama nimshukuru mama yetu Samia, kwa kutufanyia kazi kubwa katika sehemu ya VAT ya Jamhuri wa Muungano ya Tanzania. Kiukweli tulikuwa katika hali mbaya sana kule Zanzibar kiasi ambacho ilifika hatuwezi kuutaja Muungano kabisa, ilikuwa tukiutaja Muungano kwa mwananchi wa kawaida anavyokuja juu, unashindwa unafikia hadi unanyamaza kimya. Tumefikia hatua nzuri lakini bado, ni wakati muafaka sasa wa kwenda kumaliza zile kero za Muungano zilizobaki hususan kwenye VAT. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazanzibari tunataka tukitoa bidhaa zetu kutoka Zanzibar kuja Tanzania bara basi tusiwe na vikwazo kama vile tunavyotoa Tanzania bara tukapeleka Zanzibar. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nije katika sensa. Naishukuru bajeti hii imezungumzia vizuri na imetenga pesa ya bajeti kwa ajili ya sensa. Nitakacho kiomba hapa ama nitakachoshauri hapa, ni Serikali kuzipeleka haraka fedha za bajeti ya sensa ya watu na makaazi kwa sababu, mara nyingi sana tunapokwenda kwenye sensa kutekeleza majukumu ya sensa changamoto moja tunayokutana nayo ni elimu ndogo, inafika hadi siku mdau anakwenda kukamilisha yale mahesabu ya sensa unatakiwa uanze na elimu kwanza, unamkuta mwananchi hakuna elimu yoyote aliyopatiwa juu ya sensa, vinginevyo analilingiza suala la sensa katika masuala ya dini na tamaduni, jambo ambalo haliko sawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali tujitahidi sana kuzifanyia kazi pesa za bajeti ya sensa zipatikane haraka na elimu ifike kwa usahihi kwa walengwa wahusika zaidi

hususan kwa upande wetu wa Zanzibar. Kule kuna changamoto mnajua fika dini iliviotanda kule Zanzibar, kwa hiyo kila kitu kinaingizwa katika dini, ni wakati muafaka Serikali kutoa elimu kabla ya kwenda kufanya mahesabu ya sensa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo mawili niipongeze tena Serikali kwa kuleta bajeti nzuri hii, nimuombe kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, nataka uwe mfano Bunge hili la Kumi na Mbili, tukitoka tutoke na kipaumbele kizuri bajeti yetu ifikie kiwango, kile ambacho kwamba tumekipanga. Naamini kabla ya kuitisha hii bajeti ulishazungusa jicho lako Tanzania nzima na ukajua fedha ya bajeti itatokea wapi. Sitaki kwamba nikupe twakimu za kilimo za wizara moja moja hapana, ninachokiomba nataka utuwekee historia ndani ya Bunge hili la Kumi na Mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii iende ikakamilike kwa asilimia 100, tukirudi kule majimboni tuwe tunatemebea vifua Mbele kwa ajili ya bajeti hii. Sikupi pongezi nikupongeza niatakaporu Mungu akiniweka hai, baada ya mwaka huu mmoja nikaiona bajeti hii imefikia wapi, hapo nitakuja kuleta pongezi kwa kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas.

**MHE. TARIMBA G. ABbas:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nivunje utaratibu kidogo, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Ameir Mohammed, kwa uamuza wake wa busara, kwa leo kutamka ndani ya Bunge lako tukufu, kwamba anakuwa mwananchi na hii ifungue milango kwa waheshimiwa wabunge wengine waweze kufuata mfano mzuri kama huu na namuombea Mwenyezi Mungu majaze busara zaidi Mheshimiwa Ameir Mohammed. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo...

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Taarifa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Rashid Shangazi.

## TAARIFA

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayezungumza hapa ndio Mwenyekiti wa wabunge wa Simba hapa mjengoni, na katika makabrasha yetu hatujawahi kuwa na mwanachama anayeitwa Ameir Abdalla Ameir, ahsante. (*Makof/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tarimba taarifa unaipokea.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ananipotezea muda na naomba uulinde muda wangu ndio kwanza naanza, sasa ndio naanza. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ambayo nitaitumia vizuri, katika kuhakikisha nachangia vizuri katika hotuba hii ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, na ninaweza kusema katika historia ya hotuba za bajeti, hotuba ambayo imewagusa wananchi kwa kiasi kikubwa sana ni hotuba hii, imejaa ubunifu na inanipelekea nimuombe Mwenyezi Mungu amjaalie Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan, yeye na timu yake. Mawaziri hawa wakiwemo ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na wengine wote wanaomsaidia, Mwenyezi Mungu awajaalie afya, uzima na akili nydingi sana za kuwa wabunifu kama walivyofanya safari hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia katika eneo moja, na eneo lenyewe ni sera na mikakati ya kuongeza mapato na kama ilivyo katika Ibara ya 25 ya hotuba, kwa wale ambao wanacho hicho kitabu naomba wapeleke hapo macho yao. Na nkipata muda nitagusia jimboni kwangu Kinondoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda kuchangia nawaombeni siku ya Jumanne, wabunge wote tuwemo

ndani ya Bunge hili tui pigie kura ya ndio bajeti hii. Kama alivyosema ndugu yangu Mheshimiwa Shangazi kwamba Wabunge wote wawemo ndani ya ukumbi, siku ya Jumanne basi Mwenyezi Mungu awajaalie wote wawepo humu ndani, ili bajeti hii ipate kupigia kura ya ndio pamoja na wenzetu walio upande ule kule walio wachache. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najaribu kusoma azma ya Serikali ya kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa kuweka mazingira rafiki kwa mlipa kodi, ili wawavutie wawekezaji na vile vile kundi la wafanyabiashara wadogo na wakati, ili waweze kupanua wigo wa kodi ni jambo zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naisoma hii pamoja na ile azma nyengine ya kujenga uchimu shindani wa viwanda kwa maeneleo ya watu. Haya ni madhima mawili makubwa sana ambayo Serikali lazima iangalie kwa macho ya uangavu kabisa. Kwa sabau gani, kwa sababu hivi vitu vinakinzana na hali ya sheria zilizopo nchini pamoja na sheria za kodi hazionekani kabisa kuipa *support* hiyo azma ya Serikali ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa ajili ya maendeo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niwape mifano miwili mikubwa kabisa, na hii inahusu watanzania ambao wamejaribu kujenga viwanda vya madawa hapa Tanzania, changamoto zao wanazozipata ukilinganisha na dawa zile ambazo zinazotengenezwa nje na kuletwa nchini, sasa hivi hapa Tanzania dawa ambazo tunazitegemea sana ni dawa zinazotoka nje, na kulifanya utafiti August mwaka 2019, yupo bwana Dikson Pius Wande na wenzake, walifanya utafiti juu ya mahitaji ya dawa katika nchi hii, na wakaona kwamba katika mwaka 2021, dawa ambazo zinakwenda kuingizwa Tanzania ni karibu zenye dhamani ya dola milioni 906, sawa na katibu triliioni 2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hiyo utakuta hizi ni dawa zinazoletwa na *private sector* peke yake, achilia zile dawa ambazo zinaletwa na Serikali. Sasa ukiangalia utakuta

kwamba wanaojenga viwanda vya madawa nchini, wao wanapata misukosuko mikubwa sana kwa kuwa hali ya sheria za kodi haimpi nafuu mjengaji wa viawanda vya madawa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii utashangaa *cough syrup*, juzi nimenunua *cough syrup* kutoka Bangladesh shilingi 3,000 lakini *cough syrup* hiyo hiyo, ya *in gradients* hizo hizo ya Tanzania ni zaidi ya shilingi 3,000. Kwa kuwa tuna kasumba ya kuona kwamba dawa za nje ndio nzuri tunakimbilia kununua zile ambazo ni nafuu vile vile. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikwambie kitu kimoja, kwamba watafiti wale wanasema, katika mwaka mmoja unaokuja mahitaji ya dawa yataongezeka kwa asilima 28, maanda yake tunawasaidia wenyewe viwanda vya nje na wafanya biashara wa nje, kuendelea kuvuna fedha za Tanzania, wakati Tanzania tunaweza kutoa tukatoa unafuu mkubwa kwa wajengaji wetu wa viwanda, ili hata ile azma ya Serikali inayosema kwamba watu wajenge Tanzania ya viwanda iweze kutimia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo mtu ambaye anatengeneza *cough syrup* Tanzania, pengine atahitaji kuleta zile chupa, angalia hapo akiletu ile chupa anaambiwa lazima aweke na *label*/moja kwa moja huko inakotoka, *label* zenyewe ni za karatasi, zikija hapa zinaingiwa katika mifumo ya kusafisha chupa zile, lebo zinaharibika, na wanaambiwa hivyo ili wapate msamaha wa VATlazima watimize masharti kama hayo, sasa masharti gani hayo, tuweke masharti ambayo yataidia viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Mheshimiwa Dkt. Mwigulu yupo katika Serikali ambayo ni Sikivu, na wewe bahati nzuri Mwenyezi mungu amekujaalia kuwa mwananchi, na wananchi ni wasikivu. Hebu sikiliza kilio cha wananchi ambao wanajenga viwanda Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba twende sehemu nyengine, katika masuala yanayohusiana na unafuu wa

kufanya biashara, wafanya biashara hasa upande wa *TRA*. Hebu angalieni *dispute resolution* ya makodi haya, Kamishna anapoandikiwa kwenye *dispute resolution* kama ilivyo kwenye sheria ya *TAA* katika *part 7*, utakuta kwamba kuna mlolongo mkubwa sana wa kuondoa haya matatizo ambayo yanatokana na *decisions* zinazofanywa na Kamishna, na zenyewe zinasababisha mashauri yazidi kule kwenye *tax board appeal/inafanya* tukose kupata fedha za Serikali kwa sababu mashauri hayaendi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningekuomba katika hili Serikali ifanye utafiti iweze ikaangalia sheria zile kinzani ambazo hazitupi manufaa katika sera yetu ya Tanzania ya viwanda uzifanyie marekebisho, na hazi ni sheria zote mifumo ya *licenses*, mifumo ya usimamizi na mifumo ya kodi inahitaji kuangaliwa vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende Kinondoni. Nataka niseme kwamba bajeti hii imetufanyia kazi kubwa sana, na namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuja na bajeti ambayo wabunge wengi wameisifia, hasa upande pale tulivyopewa shilingi milioni 500 kwa kila Jimbo. Nataka niwaambie milioni 500 kwangu hazitajenga lami lakini kuna barabara nyingi ambazo nitakwenda kuzitengeneza kwa kiwango cha changarawe, ili ziweze kupidika. Wananchi wa Kinondoni wanaoniskiliza, barabara ya Wibu, barabara ya Ufipa, barabara ya Chogo, barabara ya Wakulima, barabara ya Gulwe, Mkalama, Lalago, Sekenke, Mkunguni, Kiwanjani, Mapera kote huko tunakwenda kuzijenga hizi, angalieni bajeti ya wananchi inavyo kwenda ufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupongeze wewe pamoja na Serikali, kwa kuliona suala la kulitengeneza mto Msimbazi ambaao ni kero kubwa sana, Dar es Salaam, na nataka niwambie kwa kutengeneza mto msimbazi sio tu Kinondoni inakwenda kufaidika Dar es Salaam nzima inakwenda kufaidika, kwa sababu mto Msimbazi ukifurika magari hayapiti Morogoro *road*, sasa hivi magari yatakuwa na nafasi ya kwenda kupita, daraja itajengwa, wananchi wa Kigogo,

Mzimuni, Magomeni wote wanakwenda kupata nafuu ya jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni fedha nyingi sana ambazo Serikali imeziweka, kutohana na hili nataka niwaambie wananchi wa Kinondoni kwamba wamuombee Mheshimiwa Rais, wamuombee Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwiguli pamoja na Serikali nziama, kwa sababu tayari..

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante!

**MHE. TARIMBA G. ABNAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aaah! Unanitoa raha lakini nikushukuru sana na naunge mkono hoja hii, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Sasa namuita Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, wakati huo Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko na Mhehsimiwa Mohammed Maulid Ali ajiandae.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuweza kunipa fursa hii kuweza kuchangia katika bajeti hii ya Serikali ya mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subhana Wataalaah* kwa kuweza kutujaalia uzima na kuweza kuendelea na bajeti katika kipindi hiki cha lala salama. Hali kadhalika ningeomba vile vile kumpongeza sana sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wa Wizara ya Fedha wakiongozwa na Komandoo Katibu Mkuu Tutuba kwa kazi nzuri ya ukweli ambayo wameweza kuifanya. Kwa kweli, bajeti bajeti hii kama ambavyo wenzangu wamezungumza imezingatia hoja za Wajumbe wa Bunge hili Tukufu na ndiyo maana imekuja kuwa ni bajeti kielelezo, bajeti ya mfano, bajeti ya mkakati ambayo inakwenda kutuvusha katika uchumi ule wa kiwango

cha chini tunakwenda katika daraja la juu sasa uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeanza tu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Alhamis tarehe 10 wakati anawasilisha bajeti *speech* yake hapa siku ile ile kama nchi tano zilikuwa zikiwasilisha bajeti zao zile za nchi za Afrika Mashariki. Sambamba na hilo pia Zanzibar, siku ileile Alhamisi tarehe 10 iliwasilisha bajeti yake, Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sasa Mheshimiwa Waziri nikuombe hapa kabla sijaenda kwenye michango ya moja kwa moja kwamba ukimaliza bajeti hii tukimaliza Bunge hili, ningekuomba sana ukae na Waziri wa Fedha wa Tanzania Visiwani (Zanzibar) pamoja na Waziri anayeshughulikia masuala ya Muungano kule Zanzibar, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, muweze kukaa kuangalia vipaumbele vyta bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambavyo vina mnasaba wa kuangalia ushirikiano ambaa unahitajika kwa upande wa Muungano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hili kwa sababu mara nydingi bajeti ya Zanzibar kuna maeneo ambayo kwa kweli kama haikupata msukumo wa Waziri wa Fedha pamoja na Sekta za Muungano huku Tanzania Bara basi bajeti ile inakuwa ina kasoro na mambo mengi yanakuwa hayawezi kutekelezeka vyema. Kwa hiyo, naomba tu Mheshimiwa Waziri hili ukali-*note* ukimaliza usisubiri upate mualiko, mtafute mwenzako Waziri wa Fedha muweze kukaa kitako pamoja muangalie vipaumbele ambavyo vinahitaji ushirikiano muweze kuvitekeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala muhimu ambalo pia ningependa kuligusia. Wakati Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano Hayati Magufui Mungu amrehemu anazindua Bunge la 12, alisisitiza sana ushirikiano wake kwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hili kwa kweli mimi siiti ile ni hotuba ya kulizindua Bunge, naiita ni hotuba ya kutuusia kwa sababu kama alijua kwamba anaondoka basi niwausie au niwaase viyi Watanzania wakati naondoka waishi viyi hasa katika masuala ya Muungano. Hali kadhalika wakati anamuapisha Waziri Mkuu kule Chamwino pia

alimkaribisha Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kuweza kueleza machache na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar alitumia muda mwingu kuweza kuomba ushirikiano na kuungwa mkono na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, ningependa tuzidiske kuziunga mkono zile sekta na taasisi za Zanzibar katika masuala ambayo yanahitaji ushirikiano wa Kimuungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kuna Sekta ya Kilimo na Mifugo. Sekta hii siyo ya Muungano lakini kuna changamoto kama wenzetu wa Mambo ya Ndani hawakuisaidia, basi wananchi wataendelea kupoteza nguvu zao bure na tija ya kilimo na mifugo haitaweza kupatikana Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa kipindi kirefu na hata Rais wa Zanzibar wakati ananadi sera za Chama cha Mapinduzi aliahidi hili kwamba atajitahidi kuhakikisha kwamba kero za wizi wa mazao ya kilimo na mifugo inapungua. Kwa kweli, kwa tatizo kubwa la wizi wa mifugo na mazao ya kilimo Zanzibar na hata nafikiri Mheshimiwa Abdallah Mwinyi ni shahidi. Jimboni kwake kule kuna mwannachi wake mmoja alipoteza maisha kwa kulinda nazi. Amelinda nazi wakati mtu yuko juu kwenye mnazi anaangua basi yeye wakati analinda kuna mwizi mwagine akaja akampiga kisu na kumuua hapo hapo. Sasa kwa kweli ningeomba tu katika bajeti inayokuja Wizara ya Mambo ya Ndani ije ituambie mkakati ambao imeutumia katika kipindi hiki kuondoa tatizo la wizi wa mazao ya kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wameondokana kabisa na suala zima la ufugaji Zanzibar. Mtu alikuwa na mbuzi au ng'ombe wake watano, kule ufugaji wetu sio mkubwa sana lakini zizi zima limeenda kuchukuliwa wakachinjwa hapo hapo. Sasa nataka kuwauliza, hivi Jeshi la Polisi liko wapi? wakati watu wanajitahidi kulima wewe shamba lako zima unaenda asubuhi limeshavunwa lote, kama muhogo umeshavunwa wote. Kama viazi vimeshavunwa zote, kama nazi zimeshaanguliwa zote. Kwa hiyo, *ina-disappoint* au inakatisha tamaa wakulima kwa upande mmoja. Kwa hiyo,

Wizara ya Mambo ya Ndani lazima tuje na mkakati tatalisaidiaje hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kwenda Misri, wenzetu kule ukitembea ndani ya dakika moja utakutana na Askari kwa sababu wanafahamu hali yao. Sasa na sisi Zanzibar Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani lazima uje na mkakati wa kulisaidia hili. Ni mionganoni mwa kero ambazo Mheshimiwa Rais wa Zanzibar ameahidi kwenda kuzifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Donge, nafikiri kama ningekuwa Tanzania Bara tungeweka mionganoni mwa Mikoa mitano ambayo inalisha nchi. Jimbo la Donge ni mionganoni mwa Jimbo ambayo Mungu kayajaalia kuyapa rutuba ni mionganoni mwa maeneo ambayo ni *big fertile land* lakini kwa kweli kumekithiri wizi kiasi kwamba hata ukilima basi huna uhakika wa kuvuna. Mazao yanavunwa usiku, yanavunwa machanga kiasi kwamba tija ya kilimo na mifugo haionekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nazungumzia hilo, ningependa vile vile kuzungumzia suala jingine la kuzishika mkono Sekta za Zanzibar. Zanzibar tuna miundombinu ya barabara ambazo ni *main road* hazizidi kilometra 700, Zanzibar nzima yaani hiyo. yaani ukitoka Mjini Zanzibar kwenda Nungwi, Mjini Zanzibar kwenda Makunduchi, Mjini Zanzibar kwenda Chwaka na ukitoka Wete kwenda Mkoani, Wete kwenda Makangale, Wete kwenda Micheweni ni kilometra zisizozidi 700. Lakini tumekuwa tukihangaika na barabara hizi kwa miaka sasa hivi, toka mapinduzi hatujaweza kumaliza kwa sababu hali ya Zanzibar kama hatukuishika mkono kuweza kuikamilisha vizuri ile miradi ya kimkakati ni ngumu.

Kwa hiyo, ningeomba sana hii miradi ya wahisani ambayo inapitia katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuiangalie sana Zanzibar kwa sababu kinyume chake ina-*disappoint* maendeleo ya Zanzibar kwa asilimia kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Kwanza aliisaidia Zanzibar kuipa eneo Makurunge kule. Lile eneo akasema chukueni fugeni ng'ombe ili Zanzibar iondokane na matatizo ya nyama ya ng'ombe na maziwa. Ile ni *spirit* ambayo sisi hivi sasa lazima tuiige. Kwa hiyo, naomba Mawaziri na uongozi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivi sasa tuige *spirit* ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Kwanza ya kupenda kuisaidia Zanzibar kuwa ni kama *economic hub* kwa *East Africa*. Tukiitengeneza Zanzibar ikawa ni *economic hub* itakwenda kuisaidia Tanzania Bara vilevile. Lakini matatizo ya Zanzibar vilevile yatakwenda kuhatarisha na kuongeza changamoto za Muungano vilevile. Kwa hiyo, ningependa tukalisaidia hili nalo kwa sababu lina umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Waziri wa Fedha amesaidia zile pesa za Majimbo zile Milioni Mia Tano ukisaidia Zanzibar hutapoteza kitu kwa sababu ndiyo ile *spirit* Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Kwanza ameifanya kwa kuipa Zanzibar ardhi ndani ya Tanzania Bara. Wewe ukipeleka zile fedha Milioni Mia Tano ni ile ile *spirit* ambayo ameifanya Mwalimu Nyerere kipindi hicho kwa kuipa Zanzibar ardhi huku.

Kwa hiyo, utakuwa hujafanya kosa kubwa Mheshimiwa, iga huo mfano ili na wewe uache *legacy* ambayo Zanzibar itakukumbuka miaka 50 inayokuja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumalizia kuhusu fedha za mifuko. Nimeshukuru sana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa hii nami kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Msalala kuchangia juu ya bajeti hii ya Wizara ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita katika maeneo matatu kama muda utaniruhusu, na nianze moja kwa moja kwa kujikita katika suala zima eneo la madini. Lakini nianze kwa kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika Taifa letu la Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitachukua nafasi hii kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa ajili ya kuniamini mimi na kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Msalala lakini pia kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya. Tumeona Katibu Mkuu na Sekretarieti nzima ikzunguka kwa ajili ya kuinadi na kuisimamia Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Mawaziri na wafanyakazi wote wa Wizara ya Madini. Pia nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia fedha kiasi cha shilingi 500,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa kilometra Moja barabara ya lami katika Kata ya Bulyanhulu. Kwa hiyo, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuona namna gani sasa wananchi wa Bulyanhulu wanasumbuliwa na vumbi na kutupatia kiasi cha shilingi 500,000,000 walau tuweke kilometra moja ya lami katika eneo lile ili tuweze kupunguza vumbi lile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. Lakini pia niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutupatia shule moja ya sekondari ambayo tunaenda kuijenga katika Kata ya Ikinda ambayo itapunguza adha ya ukosefu wa shule katika Kata ile ya Ikinda. Lakini niendelee kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais na Wizara kwa kutupatia kiasi cha shilingi 1,000,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali yetu ya wilaya. Hivyo hivyo, nimpongeze Mheshimiwa Rais

tena kwa kutupatia kiasi cha shilingi 750,000,000 kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la utawala katika Wilaya yangu ya Msalala. Nimpongeze pia kwa kutupatia kiasi cha shilingi 500,000,000 katika ujenzi wa kituo cha afya kinachoendelea katika Kata ya Isaka. Mambo mengi Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ametutendea katika jimbo langu la Msalala. Hivyo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Msalala ninamshukuru na tunamshukuru kwa dhati Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kututendea wema huu katika Jimbo langu la Msalala. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa moja kwa moja kuchangia katika Sekta hii ya Madini. Sekta ya Madini kama mnavyofahamu imetembea katika misuko suko mikubwa sana mpaka hapa ilipofikia. Sekta ya Madini imekabiliwa na changamoto nyingi, nimshukuru Waziri wa Madini kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya kuhakikisha kwamba sekta hii ya Madini inasimama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kuchangia nimeona hapa kwenye bajeti hii kuna tozo ambayo inaenda kuanzishwa kwa wachimbaji wa madini wadogo wadogo na hii Mheshimiwa Waziri nikuambie ukweli, hii tunayoenda nayo kwa sasa ambayo inawataka wachimbaji wadogo wadogo wenye makusanyo yasiyo zidi milioni mia moja kwenda kulipa tozo ambazo zimeorodheshwa hapa. Hii kiukweli tunaenda kuua Sekta hii ya Madini. Sekta ya Madini Mheshimiwa Waziri nikuambie ukweli, Sekta ya Madini kwa sasa tunaona kabisa kwamba Wizara zingine zote, Sekta ya Madini wameiona sasa kama ni Sekta ambayo ya kwenda kukusanya fedha. Sekta ya Madini tunakabiliwa na changamoto nyingi sana hasa za kikodi. Kuna kodi nyingi sana katika Sekta ya Madini na ili Sekta hii iende ikasimame ni lazima tuone namna gani tunaenda kuisaidia sekta hii katika kupunguza gharama na tozo mbalimbali zilizoko hapa.

Mheshimiwa Waziri, leo hii tunakwenda kumwambia mchimbaji mdogo mdogo anapokwenda kuuza madini yake katika soko la dhahabu aende akakatwe tozo ya zuio la ajira.

Leo hii tutambue Mheshimiwa Waziri, huyu mchimbaji mdogo mdogo kwanza hana maeneo ya kuchimba ambayo ni rasi na utaratibu unaotumika kule ni kwamba mtu anayemiliki leseni ni tofauti kabisa na mchimbaji mdogo mdogo anayechimba katika leseni ile. Sasa, baada tu ya huyu mchimbaji mdogo mdogo kuchimba madini yake kunakuwa na migao mingi ambayo kimsingi inaenda kufanyika pale kabla hata ya kwenda sokoni kuuza dhahabu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wachimbaji wadogo wadogo hawajaajiri watu, wanapochimba mathalani mchimbaji ametoa mifuko 100 kwenye shimo lake, hapo hapo anakatwa mifuko kwa ajili ya mmiliki wa leseni mifuko ishirini na zaidi. Hapo hapo anakatwa kwa ajili ya ulinzi, hapo hapo anakatwa kwa ajili ya wafanyakazi, hapo hapo wanamalizana. Maana yake ni kwamba mtu anapotoka na dhahabu yake mchimbaji mdogo mdogo huyu kwenda sokoni ameshamalizana na mambo mengine yote huku. Unaendaje kumkata tena fedha pale kwenye soko la dhahabu anapouza kwa ajili ya kulipa zuio la ajira? Mheshimiwa Waziri nikuombe hebu nendeni makapitie upya mapendekezo haya mliyoyaleta yanaenda kuua Sekta ya Madini. Sisi kama wachimbaji wadogo wadogo tuko radhi kuhakikisha ya kwamba tunalipa kodi. Lengo la kuanzishwa masoko haya ni kudhibiti utoroshwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kodi hizi zinazoendelea kuwekwa hapa inaenda kufungua tena milango ya kuhakikisha kwamba utoroshaji wa dhahabu unaendelea. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, nenda kapitie upya. Hili suala haliwezekani, wachimbaji wadogo wadogo hawa wasiopitia mauzo ya chini ya milioni 100 hawawezi wakalipa mambo yote hapa, hapa yamewekwa kuna kodi inakatwa asilimia tatu ambayo kodi hii tayari ameshailipa kule mifuko. Imewekwa hapa anatakiwa akatwe kodi ya mapato ya ajira, huyu anamuajiri nani mchimbaji mdogo? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nikuombe chonde chonde twendeni tuhakikishe ya kwamba tunaenda kuondoa kodi hizi ili kumrahisishia mchimbaji

mdogo mdogo. Lakini pia niiombe Wizara badala ya kujikita kuongeza kodi hizi tujikite katika kuhakikisha ya kwamba tunaenda kuwajengea uwezo wachimbaji wetu hawa wadogo wadogo. Leo wachimbaji wadogo wadogo wanahangaika na ukosefu wa mitaji, wanahangaika na ukosefu wa maeneo sahihi ya uchimbaji, tafiti hazitolewi kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo hawa ili waweze kuchimba maeneo sahihi, hazitolewi. Leo hii tunaenda kuongeza kodi tena. Mheshimiwa Waziri nikuombe, kuna maeneo mengi ya kwenda kukusanya kodi na siyo maeneo haya. Mheshimiwa Waziri, ukipiria ripoti ya CAG imeonesha kuna kampuni kubwa zipo ambazo kimsingi zinaweza zikachangia ongezeko la kodi na mapato katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Ripoti ya CAG imejieleza hapo. Imetueleza kuna kampuni za Kimatalfa zinafanya kazi hapa na kampuni hizi kwa sasa ukiangalia uwezo wake ukisoma Ripoti ya CAG kuna kampuni zaidi ya 504 ambazo zipo na kampuni hizo ni zaidi ya 116 mpaka 154 hazijafanyiwa ukaguzi. Hebu twendeni tukajikite katika kuhakikisha ya kwamba kampuni hizi zinazoanzisha shughuli hizi za utoroshaji wa mapato twende tukatafute fedha kule tuwaache wachimbaji wadogo wadogo waweze kunufaika na rasilimali za nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nikuombe angalieni namna gani mnaenda kutupatia mitaji. Leo hii tunazungumzia habari ya mitaji kuna fedha zinatolewa asilimia 10, asilimia Nne zinaenda kwa vijana, asilimia Nne zinaenda kwa akina mama. Leo hii mchimbaji mdogo mdogo anayekopeshwa fedha hii anaenda kuchimba, bado hujajua kwamba ametumia gharama kiasi gani katika ku-*invest*, wewe unaenda kukaa katika soko kusubiri sasa umkate tozo ya ajira, umkate kodi mbalimbali bila kuangalia ametumia gharama kiasi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe hebu twende tukapitie upya mapendekezo haya. Mimi siyaungi mkono mapendekezo haya Mheshimiwa Waziri na nitashika shilingi.

Nendeni, ukija hapa Mheshimiwa Waziri njoo na majibu ya namna gani unaenda kutusaidia wachimbaji waodgo wadogo na mkaondoe tozo hizi. Haya masharti ni magumu mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunapozungumza Mheshimiwa Waziri mimi jimbo langu lina mgodi wa Bulyanhulu pale na Bulyanhulu kuna kampuni ambayo imeanzishwa Mheshimiwa Waziri iko pale. Wamezanzisha kampuni mbili kwa ajili, naweza kusema utoroshaji wa fedha. Kuna kampuni moja imeanzishwa ya *TSL* ambayo iko nje huko. Lengo la kampuni hii ni kupata *purchasing activities* ambazo zinaendelea. Lakini pia kuna kampuni nyiningine *TSL* imeanzishwa Dar es Salaam hapa, leo hii mama ambaye analima nyanya Bulyanhulu hawezi akausa nyanya zake pale mgodini inatakiwa aende Dar es Salaam kwenye kampuni hiyo iliyoko kule na nyanya anapouza wale kazi yao ni *ku-maximize profit* tu kuongeza bei na kuhakikisha kwamba wanatorosha fedha katika maeneo yale. Nikuombe Mheshimiwa Waziri chonde chonde, sisi kama wachimbaji Mheshimiwa Waziri tuko tayari kulipa kodi lakini hatuko tayari kulipa kodi za namna hii. Nikuombe, sheria hii na mapendekezo haya yaende yakafutwe, yanaenda kuua Sekta ya Madini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri amenielewa katika Sekta ya Madini. Sasa niende katika kuzungumzia suala zima la biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Tanzania ukiiangalia hapa tumezungukwa na nchi jirani. Mimi nilipata bahati ya kutembea kwenda Dubai nikaona namna gani wanafanya. Kuna maeneo mengi Mheshimiwa Waziri nikuombe, leo hii hapa unaona watu wa kutoka Uganda, Rwanda, kutoka maeneo mbalimbali wanaenda Dubai kwenda kununua magari wanayaleta yanapita hapa na yanaondoka. Hivi, kwanini kama Serikali Tusianzishe utaratibu wa kuwaruhusu watu hawa wanaoingiza magari wafungue *yards* kubwa hapa wasitozwe ushuru kwanza, watozwe tui le kodi ambayo kimsingi mteja akienda kununua gari lake ndiyo atozwe kodi.

Maana yake ni kwamba tutawarahisishia watu wanaotoka Uganda, wanaotoka Burundi na maeneo mengine kuishia hapa nchini kwetu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nikuambie watu wakazi wa Isaka tuko tayari kutoa eneo tuwaite hawa watu ondoeni kodi za magari watu walete hapa magari yao waweke. Mteja akienda pale anaponuna gari lake basi aweze kutozwa kodi na wale wanaotoka nchi jirani wanapokuja kununua magari hapa wasitozwe kodi wapeleke huko, hii itasaidia kuongeza mapato katika nchi yetu hii ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niende kwenye suala zima la kilimo. Tumeona mnajitahidi na nipongeze wakati tunajadili bajeti ya kilimo hapa watu wengi wamezungumzia wallkuwa wanalia kilimo, kilimo, kilimo, lakini mimi nizungumze mambo mawili tu; katika kilimo hapa ni lazima tuone namna gani tunaenda kutengeneza masoko, *issue* sio mbegu, mbegu wananchi tunaweza tukanunua, lakini *issue* ni masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo ninapozungumza hapa kwenye Jimbo langu la Msalala wengi ni wakulima wa mpunga. Ukiangalia Kata ya Mwaruguru, Kata ya Jana, Kata ya Mwananse, Kata ya Kashishi, wote ni wakulima wa mpunga na tunavyozungumza hivi bado wana *stock* ya mwaka jana na bado wana *stock* ya mwaka huu na wameamua baadhi yao kutelekeza mpunga wao mashambani kwa sababu hawana sehemu ya kuupeleka na bei bado iko chini. Kwa hiyo, niwaombe namna gani Wizara inaweza kujikita katika kuhakikisha ya kwamba mnaenda kututafutia soko la kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Serikali imekuwa inakuja pale ambapo wananchi wanavuna ndio inaingia, lakini ni namna gani inamsaidia huyu kutafuta soko na kuhakikisha ya kwamba inamsaidia kwenye kumkopeshia ili aweze kufanikiwa, hakuna. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri na niwaombe Wizara ya Kilimo hebu njooni sasa

mfanye walau *research* katika Jimbo langu la Msalala ili muwasaidie wananchi hawa muone namna gani wanaweza wakauza mpunga wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu leo gunia la mpunga mwananchi anaiza kwa shilingi 36,000 lakini bado kuna matapeli wameibuka humo humo. Leo Serikali imepiga marufuku lumbesa, lakini viwanda vimeibuka sasa kuanza kutengeneza mifuko ambayo inabeba madebe kuanzia nane, wanaenda kumdhulumu mkulima. Niwaombe Wizara na wanaohusika njooni basi katika Jimbo langu la Msalala muone namna gani wakulima hawa tunaweza kuwasaidia ili waweze kuuza mazao yao kwa bei iliyokuwa nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine niseme tu kuna matapeli wamo katika Wizara ya Kilimo na maeneo mengine. Ili tuweze kufanikiwa katika sekta ya kilimo; moja ni tunaweza kutafuta masoko nje ya nchi. Leo hii watu wanatoka nje kuja kufanya biashara ya mazao, kuna watu wanakuja kuwatapeli, *ku-destroy image* ya nchi; Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo uko hapo unanisikia, leo hii kuna watu wamekuja hapa kufanya biashara ya ufuta, Mheshimiwa Naibu Waziri ananisikia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa wamekuja kutuamini hawa wakatoa fedha zao hapa na wametapeliwa, chukueni hatua kwa watu hawa. Kesi hii Mheshimiwa Waziri bado inasumbuliwa, watu hawa wamedhulumiwa zaidi ya dola laki nne watu wamedhulumiwa na wafanyakazi hao wapo kwenye *ma-go down* wanawaleta watu kutoka nje, wanawaleta kuwaonesha kwenye *ma-go down* ya ufuta yale na wanawaambia ufuta huu sisi ndio tunaweza kuuza, wanapewa *advance*, kufanya hivyo ni *ku-destroy image* ya nchi na masoko katika nchi yetu hii Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo uko hapo, hebu ninaomba hili suala lichukulie hatua, limeenda TAKUKURU, limeenda wapi, lakini hakuna majibu watu wanalia kutafuta fedha zao. Huyo aliyechukua fedha hizo Mheshimiwa Waziri mchukulieni hatua arudishe fedha, anaharibu taswira ya nchi Mheshimiwa Waziri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo ninaomba kuunga mkono hoja na ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. ninaomba kutambulisha baadhi ya wageni.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Regina Ndege, wageni wa Mheshimiwa Regina Ndege, ahsante, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wa Mheshimiwa Oscar Kikoyo, ambao ni watalii, ahsante sana, karibuni. (*Makofi*)

Lakini pia tunao wageni wa Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mbunge wa Ukerewe ambao wageni wake ni Philomena Henry pamoja na Jasmin Hussein, ahsante. (*Makofi*)

Lakini pia tunao wageni wa Mheshimiwa Hawa Mwaifunga; ambaye ni Mkurugenzi wa *Mo International Limited*, ahsante. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge nataka pia kukumbusha kwamba sasa hivi tunaendelea na mjadala wa bajeti na kwa mujibu wa Kanuni zetu kifungu cha 122(2) ilikuwa Mheshimiwa Mbunge anaweza kushika shilingi kama kuna jambo amelitazama pale. Sasa hivi tunakoelekea baada ya mjadala huu ni kupiga kura ya wazi kwa mujibu wa kanuni yetu ya 126(2) kwa hiyo, hakutakuwa na fursa ya kushika shilingi. Kwa hiyo, nilitaka nitoe ufanuzi huo ili liweze kuwa *clear*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuweza na mimi kuchangia kwenye mjadala huu muhimu wa bajeti ya Serikali, lakini kabla ya kwenda kwenye mchango wangu moja kwa moja nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania, mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan. Bajeti ambayo

imewasilishwa mbele yetu ni bajeti ambayo imeonesha nia ya dhati ya Mheshimiwa Rais ya kuendeleza kazi ambazo zilikuwa zimeshaanzishwa katika Awamu ya Tano, lakini ya kuweka mkazo katika utekelezaji wa miradi na majukumu mbalimbali ambayo yana tija kwa Watanzania kwa kipindi hiki cha Awamu ya Sita. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Mwigulu Nchomba. Hotuba hii mbali na uwasilishaji wake ulikuwa wa tofauti na hotuba nyengine ambazo nimeshuhudia zikiwasilishwa humu, lakini ni hotuba ambayo imebeba mawazo, maono na michango ya Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wanajadili katika kipindi chote tangu tumekuja kuanza Bunge hili la bajeti. Hii imeleta matumaini, imeleta ari, lakini inatuongezea nguvu kuona namna gani ambavyo tunaweza tukachimbua mambo zaldi kwa ajilli ya kuishauri Serikali kwa imani kwamba haya ambayo tunayazungumza ndani ya Bunge Serikali inachukua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimshukuru na kumpongea sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Masauni; wanafanya kazi nzuri na kwa kweli, *combination* yao watu hawa wawili, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, itatuletea tija na matunda makubwa sana katika kipindi hiki cha Awamu ya Sita. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia Bajeti Kuu ya Serikali; bajeti ambayo ina mambo mawili makubwa, jambo la kwanza ni ukusanyaji wa mapato, lakini jambo la pili ni matumizi ya mapato ambayo yanakusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukusanyaji wa mapato chombo chetu, mamlaka ambayo tunaitumia katika ukusanyaji wa mapato nchini ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), lakini katika michango ya Waheshimiwa Wabunge wengi ambaeo walikuwa wanazungumza tangu mjadala huu umeanza umeonesha kuna upungufu mkubwa wa watumishi *TRA* na hii inawezekana ndio sababu tunasusua katika ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa ushauri kwa Serikali. Kutokana na upungufu huo wa watumishi na taarifa niliyonayo ni kwamba tuna uhitaji wa watumishi 7,406 nchi nzima kwa Mamlaka ya *TRA* peke yake, lakini watumishi walipo ni 4,733 na upungufu ni 2,673, lakini ukiangalia hali halisi ya watumishi kwenye maeneo yetu hususan kwenye Wilaya zetu unakuta Ofisi ya *TRA* ya Wilaya ina mtumishi mmoja kwa maana ya Meneja wa *TRA* wa Wilaya au wawili, ye ye na msaidizi wake jambo ambalo kwa kweli linazorotesha sana ukusanyaji wa mapato kwenye maeneo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wilaya nyiningine ina kata zaidi ya 30, lakini yuko meneja mmoja tu, *I mean* mtumishi ambaye ni Meneja tu wa *TRA*, ndio anafanya kazi ya kutoa elimu, kukagua, kutoa tathmini, kwenda kuhamasisha na kuelimisha watu watumie mashine za *EFD* na kadhalika ili aweze kukusanya mapato. Sasa illi tuweze kusaldia Serikali najua kwamba, hatuna uwezo wa kuwaajiri watu 2,600 *TRA* peke yake kwa wakati mmoja na wala simaanishi kwamba, hao watu wasiajiriwe, lakini nafikiri tunaweza tukaitumia Mamlaka ya Serikali za Mitaa tukaondoa hili ombwe la upungufu wa watumishi katika ukusanyaji wa mapato kwenye maeneo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mfumo wetu wa utawala nchini umeanzia kwa Mjumbe wa Nyumba Kumi, umeenda kwenye Kitongoji, unaenda kwenye Kijiji, unakwenda kwenye Kata mpaka kwenye Wilaya na ngazi ya Taifa. Na huko kote kuna viongozi na watumishi wa Serikali, viongozi ambao wangeweza kutoa taarifa za ukusanyaji wa mapato wakazipeleka kwa Meneja wa *TRA* wa Wilaya akapata taarifa ni duka gani jipya limefunguliwa, ni duka gani limefungwa, ni kwa namna gani watu wanakwepa kodi. Tayari ikawawezesha hawa watumishi wachache wa *TRA* kuweza kufanya kazi yenye ufanisi katika ukusanyaji wa mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ningeishauri sana Serikali tuwatumie watendaji wa kata, tuwatumie watendaji wa vijiji, tuwatumie Wenyeviti wa mitaa, tuwatumie

Wenye viti wa vitongoji na wajumbe wa nyumba kumi-kumi na namna nzuri ya kuwatumia ni kuwatengea kibajeti kidogo tukawawezesha sasa kama ambavyo tumeona kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri kwamba wanakwenda kulipa posho ya madaraka kwa Watendaji wa Kata. Tushuke twende mpaka kwa Mtendaji wa Mtaa au wa Kijiji, twende mpaka kwa Mwenyekiti wa Kijiji na kitongoji watusaidie na tuwa-*task* hii kazi ya kutoa taarifa ya walipa kodi, ili kurahisisha hili suala la ukusanyaji wa mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna ombwe kubwa kati ya Serikali za Mitaa na Mamlaka ya Mapato – *TRA*. Unakuta wanakwenda kufanya ukaguzi eneo hilo hilo moja, pengine duka hilo hilo moja watu wa *TRA*, lakini hawezi kukagua lile jambo ambalo limekuwa *tasked* kwa halmashauri labda ya Wilaya au ya Jiji. Akienda mtu wa jiji ameenda kukagua labda anataka kwenda kukusanya *service levy*, lakini hana muda kabisa wa kuangalia kama je, kodi ya mapato imekwenda *TRA*.

Sasa hawa watu tukiwa-*/link* ikawa mtumishi wa Halmashauri akienda kukagua masuala yanayohusu Halmashauri akapewa na kazi ya kuangalia masuala mengine ya Serikali kwa sababu hawa wote ni watumishi wa Serikali, wote wanalipwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wote wanawajibika kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa nini watengane? Kwa nini wasifanye hizi kazi kwa pamoja kukapatikana mazingira ya ufanisi mwisho wa siku tukapunguza hili ombwe la watumishi katika Mamlaka ya *TRA*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku *TRA* zamani tumezoea, ukimuona mtu anafanya kazi *TRA* utaona ana gari zuri, anaishi kwenye nyumba nzuri, tofauti na mazingira yalivyo sasa. Maeneo ya pembezoni hawa watumishi wa *TRA* wanaishi kwenye mazingira magumu mno, nyumba zimechakaa, hazijakarabatiwa, magari yamechakaa na ndio ambao tunawategemea waende wakakusanye mapato kwa ajili ya Serikali yetu.

Kwa hiyo, ningeomba sana na wao waweze kutizamwa, nyumba zao ziweze kufanyiwa ukarabati maeneo ambayo hamna nyumba waweze kujengewa, ili waweze kufanya kazi hii kwa ufanisi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza leo ni upelekaji wa fedha kwenye maeneo ya matumizi. Huko nyuma palikuwa na maelekezo na ninashukuru kwa kweli ilitekelezwa vizuri kwenye baadhi ya maeneo kwamba ikiwa mradi unajengwa kwenye shule, basi fedha ya mradi hata kama ni ya darasa iende moja kwa moja kwenye shule husika ili kuondoa ile *process* ndefu ya kuweza kutoa fedha kwenda kwenye ngazi moja iende kwingine iende kwingine mpaka ikifika kule inachukua muda mrefu sana. Sasa ili kupunguza hiyo *bureaucracy* hela iende moja kwa moja kwenye eneo la matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumeweza kufanya hivyo kwenye shule, tumeweza kufanya hivyo kwenye zahanati, lakini tuna shida kwenye hela ya matumizi mengineyo (*OC*). Ofisi za Wakuu wa Wilaya hawapelekewi fedha moja kwa moja mpaka ipitie kwa Katibu Tawala wa Mkoa. Fedha yenye unakuta ni milioni tano, milioni sita, milioni mbili, imeshindikana kwenda kwa *Accounting Officer* wa wilaya pale (*DAS*), inapita kwa *Accounting Officer* wa mkoa, ana miradi mingapi ya kuweza ku-manage hiyo fedha? Ana watu wangapi anaokwenda kuwalipa hiyo fedha? Lakini hiyo fedha ingeenda moja kwa moja ingerahisisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Niliwahi kuuliza humu swali pia kwamba, kuna haja gani ya fedha ya matumizi ya kituo cha polisi, Mkuu wa Polisi wa Wilaya, ipitie kwa Mkuu wa Polisi wa Mkoa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni urasimu ambao kimsingi hauna sababu, kwa sababu yule aliyeko pale kwenye kituo cha kazi akipata ile fedha kwa wakati maana yake ataweba kutatua changamoto zake kwa wakati. Na ndio sababu tunaona maeneo mengine unampigia *OCD* kuna ajali, kuna

janga, kuna nini, anakwambia sina mafuta, mipira ya gari imechakaa, fedha bado haijaja, lakini fedha imepelekwa mkoani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa mujibu wa taratibu za wenzetu hawa huwezi kum-*question* *RPC* kwamba niletee fedha ukiwa wewe ni *OCD* uko chini yake kwa mujibu wa taratibu zao za kijeshi. Sasa ili kuondoa huo urasimu wote ni vyema sasa Mheshimiwa Waziri tuone umuhimu wa kupeleka fedha hizi moja kwa moja kule kwenye maeneo ya matumizi ili kuwasaidia wenzetu kuweza kufanya kazi zao vizuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napongeza pia namna ambavyo mmeamua kupeleka fedha za Maafisa Tarafa na Watendaji wa Kata, lakini Mheshimiwa Waziri nataka nikwambie, sio jambo jipya sana huko nyuma limefanyika, lakini halijafanyika kwa usahili sana kwa sababu zinapitia kwenye ofisi nyingine. Mimi nikiwa *DAS* unanilettea milioni tatu, unaweza kukuta pale umepita mwenge umeniachia deni, wamepita pale viongozi wameniachia deni, sikumbuki kupeleka fedha kwa Afisa Tarafa naitumia palepale Wiayani inaisha, lakini kama mmeipeleka moja kwa moja kwa Afisa Tarafa maana yake ni kwamba, siwezi kwenda kuichukua kule tayari atakuwa amepata ile haki yake na kazi zake zitafanyika vizuri. (*Makof!*)

Kwa hiyo, nashauri sana fedha ziende huko moja kwa moja badala ya kupitia kwenye mamlaka nyingine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo ningependa kulizungumza; siasa, uendeshaji wa nchi kwa akili yangu ya kawaida kabisa kila jambo linakwenda kwa wakati. Siasa yetu ya sasa kwa kauli mbiu ya mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan tunaendeleza kazi ambazo tulizianza katika Awamu ya Tano, lakini kwa namna ambavyo mama anaenda kufanya kazi anataka kuacha *legacy* kama mama wa kwanza kuiongoza nchi hii. (*Makof!*)

Mheshimiwa mwenyekiti, ili aweze kuweka *legacy* lazima tumsaidie katika eneo la maji tufanye vizuri, bajeti ya

maji iende vizuri akamtue mama ndoo kichwani. Lazima tumsaidie katika eneo la afya, vituo vya afya ambavyo vimejengwa vipelekewe vifaa tiba, akinamama waweze kujifungua salama na wajifungue kwa mazingira ambayo yanatakiwa, lakini lazima tupeleke bajeti na ifike ile ambayo inalenga kuwawezesha akinamama kiuchumi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiyafanya haya mambo matatu tutakuwa tumemsaidia mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan, kuacha *legacy* katika nchi hii katika muda wake wote ambao atakuwa amekuwa madarakani. Ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namuita Mheshimiwa Mohamed Maulid Ali, wakati huo wafuatao wanajiandaa; Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mheshimiwa Kabula Enock Shitobel na Mheshimiwa Juma Usonge Hamad.

**MHE. MOHAMED MAULID ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa ruhusa ya kuweza kuchangia siku ya leo Ijumaa, siku tukufu, asubuhi hii.

Kwanza ningependa kutoa shukrani au pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Waziri Mdogo au Naibu Waziri Mheshimiwa Masauni pamoja na timu nzima ambayo imejikita kutengeneza bajeti hii. Kwa kweli, ni bajeti ambayo tunaweza kusema haijawahi kutokea, tunawapongeza sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mchango wangu nianze kwenye *TARURA*. Napenda sana kuwashukuru viongozi wetu, pongezi kwa Serikali ambayo imehusisha vilio vya Wabunge moja kwa moja kuhusu fedha za *TARURA*, hii imetupa faraja kubwa sana. Ningependa kuwatoa hofu wananchi waelewe kwamba fedha ambayo imetengwa kwa ajili ya *TARURA* ambayo inatoka kwenye mafuta inakwenda kutuhusisha sisi kama Wabunge moja kwa moja na kutupa ujiko kule majimboni kwetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningewashauri sana Wabunge wenzangu tusiingilie sana katika kuwaambia wananchi kwamba fedha hii itasumbua katika matumizi au kuongeza gharama, si kweli, *fluctuations* katika pesa za mafuta ni jambo la kawaida kila siku na halileti athari yoyote kwenye matumizi. Kwa hiyo, tujikite zaidi kuwaelimisha wananchi kama Serikali ilivyotusaidia sisi kutuchangia, ili na sisi twende kifua mbele majimboni na sisi tuisaidie kuwaelimisha wananchi kwamba hili jambo litatusaidia sote kwa pamoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilikuwa nataka kuzungumzia suala la ajira 8,000 ambazo Serikali..., samahani ni ajira milioni nane ambazo zimeainishwa kwenye ilani yetu ya uchaguzi. Kwa kupeleka fedha hizi TARURA zile ajira milioni nane ambazo zimezungumzwa katika llani yetu ya Chama cha Mapinduzi sasa nina hakika zitatekelezeka sawasawa. Ndani ya kipindi kifupi tutawenza kuona viwanda vyetu viro tayari, malighafi kule vijijini kwa ajili ya viwanda hivi zitakuwa tayari, lakini hata barabara na viungo kati ya viwanda na upatikanaji wa malighafi zitakuwa tayari. Hongera sana Mama Samia kwa maono ya mbali kwa maslahi ya nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kulizungumza kuhusu fedha shilingi milioni 500 kwenye majimbo yetu. Fedha hizi kwa kweli, zitakwenda kusaidia tena zitakwenda kusaidia sana katika majimbo haya kwa sababu sisi kama Wabunge sasa zitatupa nguvu na zitawenza kutusaidia hata katika chaguzi zinazokuja mbele za mwaka 2025. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana Majimbo yetu yote ya Uchaguzi matatizo yake yanafanana na kilio kikubwa cha wananchi ni barabara kama yalivyo majimbo mengine ye yeyote Tanzania Bara na sisi tuna changamoto hii kule Zanzibar. Ningependa kuwahakikisha kwamba Halmashauri zetu na Manispaa hazina uwezo wa kutengeneza barabara hizi haitapendeka kama tutakuwa huku barabara zake zinaonekana vizuri kwetu kule hakupitiki,

Iakini Mbunge ni yule yule wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama alivyo Mbunge mwingine yejote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tunamwomba sana Mheshimiwa Mwigulu, Rais wetu ni msikiu sana na yeye ni mwelewa na viongozi wetu Mawaziri na hata hao Manaibu Waziri, nao ni wahanga vile vile wa jambo hili, ingawa midomo yao wameipiga zipu, lakini ukweli wote tunaathirika kwa pamoja lazima tuseme ukweli. Ikimpendeza Mheshimiwa Waziri suala hili nasi tuweze kusaidiwa ili twende kifua mbele. Huko majimboni kwetu wananchi wanaafuatilia sana vikao hivi, tena wanavifuatilia kwa nguvu zote, wanatuuliza maswali mengi kuhusu fedha hizi ambazo kwakweli hatuna majibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaamini na wao vile vile majimbo yao yatanufaika, iakini kwa kweli upande wetu ni mgumu kidogo. Nomba Serikali yetu siku chini ya uongozi wa Mama Samia, Waziri Mkuu, Waziri Mwigulu, Manaibu Mawaziri ambao kama nilivyosema baadhi yao ni wahanga wa tatizo hili, watufikirie sisi Wabunge wa Majimbo ya Zanzibar na sisi tuyahudumie majimbo haya ili yaweze kupidika muda wote hasa wakati wa kipindi cha mvua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ningependa kuzungumza...

**MHE. SALUM MOHAMMED SHAIFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Karibu kwa taarifa Mheshimiwa.

**MHE. SALUM MOHAMMED SHAIFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nimpe taarifa mzungumzaji juu ya jambo alilolizungumza, huko Majimboni kwao Zanzibar wananchi wanawauliza maswali na akasema hawana majibu juu ya hii fedha ya shilingi milioni 500 ya kila Jimbo. Naomba nimpe taarifa mzungumzaji majibu ya Majimbo ya Tanzania Bara na Majimbo ya Zanzibar majibu

yake ni mamoja, sote ni Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hakuna Mbunge wa Zanzibar wala wa Bara. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa unapokea taarifa Mheshimiwa Mohammed Ali.

**MHE. MOHAMMED MAULID ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema nimeipokea taarifa hiyo kwa mikono na miguu pamoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie kidogo kuhusu suala la ndugu zetu wa Bodaboda. Kwa kweli kwa nia njema kabisa Serikali imefanya kuwasaidia vijana hawa ili waweze kujikwamua kimaisha. Hii ndio nia njema kabisa ya Serikali ya Mama Samia. Tatizo moja tu ambalo ningependa kutoa tahadhari, kwanza kuna Mbunge mmoja amenifilisi kuhusu hizi bodaboda ambazo hazina makosa ya jinai. Vituo vyetu vya polisi sasa hivi havifagiliki havipitiki, kipindi cha mvua vichafu kwa sababu ya bodaboda hizi. Sasa ikiwezekana kama sheria inaruhusu maana yake siwezi kushindana na sheria...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali.

**MHE. MOHAMMED MAULID ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MHE. SEIF K. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya Serikali. Binafsi napenda kutumia fursa hii kumpongeza Rais Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kuanza vizuri katika uongozi wake wa Awamu ya Sita tunampa pongezi nydingi sana. Pia nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa kuteuliwa kwenye wadhifa huu katika Wizara hii nyeti ya Fedha. Nitoe pia pongezi kwa Mawaziri wote wanaofanya kazi kwenye Serikali hii, wanafanya kazi nzuri, hongereni sana Mawaziri wote pamoja na Manaibu Mawaziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze vile vile Serikali kwenye bajeti yake hii iliyowasilishwa, tumeweza kuona bajeti ambayo inaenda kuendeleza miradi ya kimkakati ambayo tumekwishaianza, tumeweza kuona fedha zikitengwa kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo linakwenda kuzalisha umeme *megawatt* 2,115. Hongera sana Serikali kwa maana bwawa lile mpaka sasa hivi limeshafika zaidi ya asilimia 52 ya ujenzi wake. Kwa hiyo ni hatua nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze kwa kuwekwa fedha kwenye kuendeleza ujenzi wa reli ya kisasa ya umeme kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza ambapo juzi tumekwenda kuzindua kuweka jiwe la msingi ujenzi wa reli kutoka Mwanza kuja Isaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze pia kwenye bajeti hii kutenga fedha za kupeleka umeme vijiji tumeona fedha mlizotenga 1.2 *trillion* kwa ajili ya kusambaza umeme vijiji vyote Tanzania, hongera sana kwa Serikali, inaenda kukamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kuona fedha walizotenga kwa ajili ya kujenga barabara na madaraja katika nchi yetu. Ni bajeti ambayo inakwenda kumkwamua mwananchi na kulisogeza Taifa letu mbele. Kwa kweli ni bajeti ambayo imezingatia viwango, ni bajeti ambayo imekuwa ya kihistoria na ni bajeti ambayo inakwenda kutoa tafsiri katika wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuchangia kwenye bajeti hii; tumeweza kuona katika bajeti hii sehemu zenyе upungufu katika baadhi ya Wizara. Sehemu ambayo napenda kuchagia ni kwa Wizara ya Kilimo. Wizara ya Kilimo imetengewa bilioni 200. Wizara ya Kilimo ni Wizara Mama na ni Wizara ambayo ni uti wa mgongo wa Taifa letu. Tukiwekeza fedha kwenye kilimo tutauinua uchumi wa Taifa letu. Leo tunahangaika kutafuta fedha za kodi mbalimbali kwenye maeneo mbalimbali, lakini tukiwekeza kwenye kilimo, mzunguko utakuwa mkubwa kwenye uchumi wetu. Mfano tu, tumetenga bilioni 200, hizi haziendi kujenga skimu wala

mabwawa, ni maeneo machache sana ambayo tunaweza kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tungeweka trilioni moja kwenye sekta ya kilimo, tukaenda kujenga mabwawa, tukaenda kujenga skimu za umwagiliaji, tutaweza kuzalisha mara mbili ya tunavyozalisha sasa hivi. Tukizalisha mara mbili maana yake tunainua uchumi wa watu wetu na wataweza kufanya biashara. Nataka nitoe mfano, pale Igunga tuna bwawa moja, skimu tulizonazo ni nne. Kata ya skimu hizi nne, tatu zinafanya kazi kwa kutegemea mvua, skimu moja inafanya kazi kutegemea mvua na maji yaliyopo kwenye Bwawa la Mwanzugi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bwawa hili linatusaidia kuzalisha mpunga mara mbili kwa mwaka na uchumi wa Igunga kwa kiwango kikubwa sana pale Mjini tunampunga mwingi ambao watu kutoka Rwanda wamefungua kiwanda pale cha kuchukua mpunga, lakini pia na kuuchakata kupata mchele, wanafanya *packaging* wanapeleka kuuza kwao. Kwa hiyo unaweza kuona kwamba hizi skimu zetu tukiziwekea mabwawa kwenye maeneo yetu sio tu Igunga, maeneo yote nchini, tukajengwa mabwawa, tutalima mara mbili na tutazalisha mara mbili, wananchi wetu watapata fedha na Serikali itapata fedha zitakazoweza kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri bajeti yake ijayo atenge fedha za ujenzi wa mabwawa kama kweli tunataka tuinue au tukomboe uchumi wa wananchi wetu, tujenge mabwawa. Pale Chomachamkola tunahitaji tujenge bwawa kubwa, tuna wakulima, tukienda Ziba kunatakiwa kuwepo na bwawa, Nsimbo panatakiwa pawepo na bwawa na Buwekelo tunatakiwa tuwe na mabwawa. Mabwawa haya tukiyajenga katika maeneo mbalimbali nchini, bajeti ya Mheshimiwa Waziri ita- *shoot*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri bajeti yetu sisi ni trilioni 36, lakini bajeti hii tukilinganisha na nchi jirani kama Kenya ambayo tunahitaji tuwe washindani wetu, ni

mara mbili yake yaani Kenya iko zaidi chukua trillioni 36 mara mbili maana yake wao wao trillioni 70 na ushehe. Kama kweli tunahitaji tushindane katika ukanda wa Afrika Mashariki tuwe *giant* bajeti yetu lazima *i-shoot*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kuchangia upande wa mgao wa fedha tunaopatiwa. Nimeweza kuona kwenye bajeti hii tumekuwa tukipata fedha kwa kila kila Jimbo kupewa wakati mwininge zahanati mbili mbili, kupewa vituo vya afya kimoja kimoja kila Jimbo na sasa hivi tumeona tumepewa milioni 500 kila Jimbo. Nawashukuru sana kwa kutupa hizi fedha, lakini niwaombe, sikatai na sisemi wasiwape lakini wawe wanaangalia mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majimbo ya Vijijini au ya Halmashauri hayalingani na Majimbo ya Mijini. Wanavyotuambila wanatupa milioni 500 sawa na Majimbo ya Mijini hawatutendei haki. Wawape milioni 500 lakini sisi wa vijijini watupe bilioni moja. Wakitupa bilioni moja angalau tutaweza, kwa sababu mijini kuna miradi mikubwa tunaweza tukaiona katika miji na Manispaa, kama vile miradi ambayo inakuja kwa ajili ya kuendeleza miji, lakini kuna mradi ambaou umemalizika ule wa *TSCP*, tumeona mikoa yote barabara za lami zinamwagika, lakini kwenye halmashauri zetu kwenye majimbo yetu hakuna lami za kutosheleza. Kwa hiyo niwaombe Wizara waliangalie hili, safari ijayo kwenye migao yetu wawape lakini sisi watupe Mara mbili ya wanayowapa wao. Kama kwenye afya wakitupa vituo viwili, kila Jimbo au kituo kimoja kila Jimbo, basi majimbo ya vijijini watupe vituo viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu katika Wilaya wana Hospitali ya Wilaya, wana fedha za kuboresha kila kitu, kijijini hospitali ya wilaya hatuna, vituo vya afya hatuna, zahanati tuna maboma, halafu wanatupa mgao wa kufanana na Majimbo ya Makao Makuu ya Wilaya, wanatupa mgao wa kufanana na Manispaa. Hili jambo ni lazima waliangalie vizuri. Kama Serikali inataka kuboresha maisha ya wananchi wa vijijini, lazima iwekeze sana kwenye vijiji vyetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie hata kwenye elimu ni hivyo hivyo na nimeona wanatupa fedha ya kujenga shule moja moja katika kila jimbo kwa nchi nzima. Nawashukuru sana na tunaenda kujenga shule 1,000 nchi nzima.

Naomba mgao huu wauangalie, kuna majimbo ya mjini yenyewe yameshamaliza shule, sasa wanataka wajenge maghorofa wakati kwenye kata zetu tuna kata saba hazina shule kabisa. Kwa maana hiyo, wakitupua shule moja maana yake tutegemee mpaka miaka saba ndio tumalize kujenga hizi shule, haiwezekani! Watupe kulingana na mahitaji, tuna mahitaji makubwa ya ujenzi wa shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi jimboni kwangu Kata nane hazina sekondari za kata. Kwa hiyo wakinipa moja na mwakani wakanipa moja, nahitaji nikae miaka nane humu Bungeni ndio nikamilishe zile shule, wakati tumepata shule 1,000, kwa hiyo watuangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine katika hizi fedha wanazotoa, wanatoa fedha hizi wanatoa pamoja na fedha za kwenda kusimamia mradi wenyewe. Mheshimiwa Ummu nimemwona, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwanza nampongeza dada yangu, anafanya kazi nzuri, ameanza vizuri. Nimeona anafuutilia mapato ya halmashauri, kule na penyewe kuna mchwa, lazima tukubaliane kule kuna mchwa. Tena kula wanatafunu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe mfano, Mheshimiwa Waziri, katika halmashauri zetu, chukulia sisi Wilaya yetu ya Igunga ambapo tumejiwekea tu tukusanye bilioni 3.1, sio fedha nyigi ni Bilioni 3.0 na hizo bilioni 3.0 tukienda tukasema tuzikusanya, asilimia 40 ya bilioni 3.0 tunapeleka kwenye miradi ya maendeleo na asilimia 60 kwenye matumizi mengineyo. Tukidhibiti kwenye matumizi tunaweza tukasimamia miradi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. SEIF K. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabula Enock Shitobelo.

**MHE. KABULA E. SHITOBELO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Bajeti Kuu ya Serikali. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na uhai na leo nipo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa kwenye ushuru wa vitenge vinavyotoka nje ya nchi, ukilinganisha na nchi za jirani zinazotuzunguka. Hapo awali vitenge vilitozwa kodi ya 0.28 kwa yadi moja ambayo nadhani sijui ni mita moja, ambapo tulipata wateja wengi sana kutoka nchi mbalimbali za jirani kama vile Zambia, Comoro, Msumbiji, Kongo, Malawi na Zimbabwe, Kenya na Uganda, kwa sababu kodi hiyo ilikuwa ni Rafiki, ilikuwa inaweza kulipika na hata vile vitenge vikaweza kuuzwa kwa bei nafuu. Baada ya muda nchi yetu au Serikali iliongeza kodi kufikia 0.4 *per yard* ambapo sasa tulikosa tena wanunuzi kutoka nje tukawa na wanunuzi wa kutoka hapa hapa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia kuhusu uchumi, uchumi tunauchangia kwa namna nyingi ambapo huyu M-Comoro alipokuwa akija kuanzia anaposhuka *Airport* au Bandarini au stendi ya basi, anapochukua *taxi*, mnufaika pale ni dereva *taxi* au bodaboda au mwenye bajaji. Akifika hotelini atachukua hoteli atalala, lakini asubuhi akiamka anaweza kula kwa mama ntilie, mama ntilie naye akapata kipato chake. Vile vile anapokuja hapa, atahitaji mawasiliano atanunua labda ni vocha, atatumia. Kwa hiyo Kampuni zetu za simu zitapata mapato na vile vile Serikali itapata kodi pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wateja walivyokuwa wakija, hawanunui vitenge peke yake, bali wameweza kununua na bidhaa nyingine muhimu nyingi. Kwa hiyo ilikuwa ni faida kubwa kwa wao kuja hapa Tanzania.

Sasa naona kodi mwaka jana ilipandishwa mpaka kufikia dola moja kwa yadi moja lakini katika bajeti hii nimeona wameshusha *percent* kufikia 0.5 kwa kitenge cha *polyester* na *cotton* wameweka ushuru kuanzia 0.6 hadi 0.8 ambayo kodi hii haitawezekana kabisa kulipika. Matokeo yake tutaongeza wafanyabiashara ambao watakuwa wanakwepa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao wanunuzi watakwenda kununua nchi jirani, kwa sababu sasa hivi changamoto iliyopo, nchi hizi jirani zote zilizozitaja hapo awali, sasa hivi zinazu vitenge bel rahisi zaidi kuliko Tanzania kwa sababu ushuru wake ni *reasonable*. Kinachotoka sasa wafanyabiashara wanakwenda kununua nchi jirani vitenge, wanatafuta njia za panya, wanaingiza ili waweze kuuza bei nafuu, lakini vile vile kupata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu Tukufu inayoongozwa na Mama yetu mpendwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan, najua mama yetu ni mwema na ni mwelewa aangalie katika hili suala zima la vitenge, kwa sababu vitenge hivi mvaaji wa mwisho ni mama, ni kitenge kama hiki nilichokivaa mimi leo na Waheshimiwa wengi walioko humu wamevaa vitenge hivi. Vile vile wauzaji wakubwa wa vitenge hivi ni akinamama, ndio wanaouza vitenge, kwa hiyo naomba waangalie kwa jicho lingine kwa kum-support mwanamke. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimalizie kwa kusema kwamba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, taarifa.

## TAARIFA

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nilitaka nimpe taarifa mchangiajia anayeendelea kuchangia sasa kwamba kuhusiana na suala la kodi ya vitenge, imepanda kwa asilimia 100. Ilipokuwa asilimia 0.4 vitenge vilikuwa vinalipiwa kwa *container* la 40 *feet* shilingi milioni 128. Sasa hivi imepanda kwa asilimia 100 ina maana Watanzania wataenda kutoa *container* hilo la 40 *feet* kwa shilingi milioni 400 jambo ambalo biashara hii inakwenda kufa pale Kariakoo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabula.

**MHE. KABULA E. SHITOBELO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo nimeipokea kwa mikono miwili. Ni kweli kabisa. Labda niongeze tena kidogo kusema kwamba, pamoja na kwamba tunalinda viwanda vya ndani lakini viwanda vyetu vya ndani kwanza haviwezi kutosheleza soko liliopo. Soko ni kubwa sana na viwanda vya ndani bado havina hiyo *capacity* kubwa kiasi hicho, lakini pia kwenye ubora, tukubali tu kwamba bado ndiyo tunaanza, siyo vibaya, lakini ni vizuri tuwe na *varieties*, yaani tuwe na vitu vingi; vitenge vya aina tofauti. Atakayependa kununua cha Tanzania anunue, atakayependa kununua cha China anunue, atakayependa kununua cha Burundi anunue. Kwa hiyo, naona ni vyema tukaacha soko huria, kila mtu akawenza kuingiza na kuuza; na kila mtu awe na *choice* yake anayotaka kununua.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ehe, taarifa.

## TAARIFA

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba sera ya nchi yetu

ni kulinda viwanda vyetu nya ndani. Suala la kwamba vitenge vyetu labda havina ubora, aishauri Serikali kuboresha na suala la kwamba uzalishaji ni mdogo, aishauri Serikali namna ya kuungeza uzalishaji na siyo ku-*entertain* bidhaa kutoka nje. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unapokea taarifa?

**MHE. KABULA E. SHITOBELO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana, siipokei kabisa kwa sababu hivi vitenge nya kutoka nje siyo kwamba vimezuia au vitamaliza hili soko la vitenge vinavyotengenezwa nchini. Bado nafasi ya kuuza vile vitenge ipo. Kila vitenge vina watu wake wanaoweza kununua. Siyo kwamba kile kitenge cha Tanzania; labda nitoe mfano mmoja. Mheshimiwa Msongozi anaweza akakinunua kwa sababu wanawake wa Kitanzania au wa Kiafrika kwanza wamejaaliwa, ni *mashallah*, wana milli mikubwa na maumbo makubwa, vitenge hivi ni vidogo, havitoshi. Hata kwa kufunga mama wa kisukuma aliyepanda kule kijijini, hakiwezi kumtosha, labda achukue vipande viwili. (*Vicheko/Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa Kabula.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea kuchangia.

**MHE. KABULA E. SHITOBELO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa kitenge nimeshamaliza, meseji imeshafika.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea kuchangia, nakulinda.

**MHE. KABULA E. SHITOBELO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu biashara ya mahotelii. Naomba ni-

*declare interest*; nami ni mdau katika hoteli. Hali ya mahotelii nchini hasa Dar es Salaam na Arusha ni mbaya sana, lakini sijawahi kusikia Mbunge hata mmoja humu anaongelea. Nimekaa kimya, lakini leo nimeona ni vyema niongee kwa sababu hata mimi niko kwenye hiyo sekta. Kwa hiyo, ninaelewa hali halisi, wafanyabiashara wa mahotelii au mahotelia wanachokipitia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa hakuna biashara tena kwenye mahotelii hasa hoteli zilizopo Dar es Salaam na Arusha kama nilivyoongea awali, lakini sababu siyo *Covid 19* kama watu wanavyotafsiri. Hili tatizo limekuwepo muda mrefu kabla ya *Covid 19*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali yangu Tukufu kurudisha tena biashara kwenye sekta binafsi hasa kwenye hoteli. Wajaribu kutuletea tena zile semina, wafanye kazi mbalimbali katika mahotelii yetu ili nasi tuweze kuchangia ushuru katika nchi yetu. Kwa mfano hoteli moja sitaitaja, walikuwa na wafanyakazi 80, lakini hivi ninavyoongea na wewe wana wafanyakazi 15; na waathirika wakubwa waliopunguzwa kwenye kazi hiyo ni wanawake, kwa sababu mahotelia wengi huwa ni wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Serikali hii ijaribu kuangalia ni jinsi gani ita-rescue huu upande wa mahotelii. Kwa kweli hali ni ngumu sana na hatujui hatima yetu ni nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, wakati huo Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mheshimiwa Nape Moses Nnauye na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava wanajiandaa.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa hii nami kuweza kuzungumza

kwenye Bunge lako hili Tukufu. Nitoe pongozi zangu za dhati kwa Waziri Mheshimiwa Mwigulu Nchemba pamoja na Naibu Waziri, rafiki yangu Mheshimiwa Hamad Masauni, bila kuwasahau Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na wataalmu wote wa Wizara hii ya Fedha na Mipango kwa uandaaji na uwasilishaji mzuri wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda, niende moja kwa moja. Kwenye wasilisho langu nitazungumzia zaidi kuhusiana na uchumi. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina uchumi wa Muungano. Uchumi huu unajumuisha na uchumi ule wa Zanzibar, ndiyo maana kila taarifa ya mwezi kutokea *BoTinatambua* uchumi wa Zanzibar, lakini utaratibu huu hautumiki pale ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapowasilisha taarifa zake za kifedha kule nje. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye mataasisi ya kifedha, kwa mfano *IMF* na *World Bank*, taarifa hizi haziendi moja kwa moja kwa sura ya kipekee ya kuitambua kama Zanzibar, isipokuwa inatambulika kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utaratibu huu unaleta madhara makubwa sana kwa uchumi wetu wa Zanzibar. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri, hivi karibuni tu tultoka kwenye janga kubwa la *Corona*, Tanzania nayo pia imeathirika kwenye janga hili la *Corona*, lakini Zanzibar nayo imeathirika zaidi kwenye janga hili. Ukiangalia Zanzibar, uchumi wake mkubwa sana asilimia 82 pato lake la Taifa inategemea kupitia utalii, lakini Bara ni asilimia kama 17 hivi na kidogo ndiyo inategemea utalii. Kwa hiyo, madhara haya yanakuja kutokezea endapo hizi taasisi za kidunia; *World Bank*, *IMF* yanapotoa fedha kwa ajili ya kuzisaidia nchi ambazo zimeathirika kifedha, inaleta madhara makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kuna nchi zetu za karibu hapa kwa mfano Kenya, Uganda na nchi nyingine za Afrika, zimepata misaada kifedha, lakini Zanzibar haijaonekana. Kwa sababu uwasilishaji wa taarifa za kifedha

kupitia *World Bank* pamoja *IMF*, Zanzibar haitambuliki. Hivyo Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri, nawaomba sana, tunapopeleka taarifa zetu za kifedha, basi lazima tutambue Zanzibar nayo ipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii makusanyo ya fedha ambayo yamepatikana Zanzibar kwa miaka miwili ambapo Zanzibar imeathirika zaidi na *Corona*, ndiyo maana kufikia kile kiwango cha fedha kwenye bajeti ni asilimia kama 70 tu, mpaka sasa hivi Zanzibar ndiyo ishaanza kupitia tozo tofauti tofauti. Kwa hiyo, hali hii ina athari kubwa sana.

Kwa hiyo, naiomba sana Wizara, tunapowasilisha taarifa zetu za kifedha nje, basi tupeleke taarifa zetu ambazo zitakuwa na sura ya Kizanzibar. Hii itasaidia sana. Naiomba sana Wizara tuzingatие hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye eneo lingine la wafanyabiashara. Kuna wafanyabiashara wapo Tanzania Bara na wengine Zanzibar. Changamoto ambayo tunayo, tuko kwenye nchi moja; wapo wafanyabiashara ambao wapo Bara ambao tayari wame *invest* kwa eneo kubwa, lakini wapo pia Wazanzibar ambao wame-*invest* kwa eneo kubwa. Changamoto inayopelekea Mzanzibar au Mtanzania wa kutoka *mainland* kwenda kuwekeza bara au wa labda wa Zanzibar akija bara wa bara akienda Zanzibar kunakuwa na changamoto namna ya kupata leseni. Akienda Mzanzibar, Mtanzania anaonekana kama *foreigner*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Wizara, hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wanapokuwepo wafanyabiashara ambao wamekuwa *interested* na kuja ku-*invest* aidha pande hizi mbili za Muungano, basi kuwe kuna *exemption* ya kuweza kumtambua kama Mtanzania; iwe baadhi ya kodi asikate, asirejee tena kwa ajili ya kukata leseni. Akija Zanzibar, basi apate *exemption* ndogo au hata atambulike. Isipokuwa anaweza akachangia kodi kutokana na mazingira gani ambayo anafanya biashara. Hii itasaidia sana; mojawapo linawenza likakuza uchumi wetu wa Tanzania pamoja na kuu-*boost*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, itatengeneza ajira kwa vijana wetu; na tatu, itatengeneza *variety commodities* pamoa na *production*. Hii itasaidia sana. Leo hii Mzanzibar akija Bara, anaanza *process* upya kwa ajili ya kupata leseni. Tuondoe hivi vikwazo ili tutanue wigo wetu sasa wa kukusanya kodi, lakini pia angalau tuonee huruma wafanyabiashara wetu waweze kuwekeza wanapokuja upande wa pili wa Muungano. Hii itasaidia sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, naipongeza sana Wizara kwa kulitambua hili kwamba sasa hivi makusanyo ya *visa* ya pande zote mbili za Muungano, basi upande ambao utapata fedha, itasaidia sana. Hii itainua uchumi wa Zanzibar, ambao kwa asilimia kubwa sana tunategemea uchumi wa vitu vidogo vidogo. Sasa tukiweka mwanya huu, itasaidia sana ku-*boost* ule ukusanyaji wa pato kupitia hii *visa*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia nchi zetu hizi mbili, huko nyuma tulikuwa tunakusanya zaidi ya shilingi bilioni 100 kwa ajili ya *visa*, lakini sasa hivi Mheshimiwa Rais ameliona hili jambo. Kwa hiyo, kutawanya hizi *visa* itasaidia kwa upande wetu Zanzibar na pia kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maana kwamba huku Bara nao pia wataweza kukusanya fedha vizuri kwa kupitia hii *visa*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, nampongeza sana Mheshimiwa Mama Samia kwa kuidhinisha pesa kila Jimbo kwa ajili ya Mfuko wa TARURA. Naiomba sana Wizara hii ilichukue jambo hili, ituangalie na upande wa pili wa Zanzibar, isiwe wenzetu tu, Watanzania Bara ndio wanaonufaika na huu mfuko wa fedha, bado na sisi kwa upande wetu wa Zanzibar tuna changamoto kubwa. Shilingi milioni 500 ukinipatia kwenye Jimbo langu, utaenda kunisaidia sana na kuwasaidia akinamama ambao sasa hivi wanatembea masafa marefu kwa ajili ya kupata huduma ya afya, akina mama ambao wanabebwa kwa vitanda kama Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba alivyozungumza hapa, watatusaidia sana sasa hivi kusafirishwa kutoka sehemu walipo kwenda hospitali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo, machache naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuzungumza machache kutokana na bajeti yetu hii. Nitazungumza masuala matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza, bajeti ya kilimo ya mwaka huu kwanza ni ndogo. Kilimo kinachangia asilimia 85 ya kazi ambazo Watanzania wamejajiri. Kilimo hiki kwenye pato la Taifa kinachangia asilimia 26.9 lakini kimetengewa kwenye bajeti asilimia 0.8. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba hizi shilingi milioni 500 kwa kila jimbo zitasaidia kutengeneza barabara za *TARURA* na hivyo kutoa mazao kwenye maeneo mbalimbali kupeleka kwenye soko. Kwa hiyo, hiyo nayo imechangia kwenye kilimo. Vilevile natambua kwamba tuna miradi mikubwa ya kimkakati ambayo inahitaji fedha nyingi, ndiyo maana pengine bajeti ya kilimo ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri kwamba baada ya bajeti hii, kwa sababu hii tunaipitisha na imeshapita, ni kwamba mwaka kesho Waziri wa Fedha na Waziri wa Kilimo waweze kukaa mapema na kuangalia umuhimu wa kuendeleza sekta ya kilimo ikiwa ni pamoja na kuimarisha skimu mbalimbali zile za umwagiliaji na kukarabati ambazo zipo. Tunahitaji takribani shilingi trilioni moja kwa miaka mitatu mfululizo kwa ajili ya kukarabati na kujenga skimu mbalimbali za umwagiliaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukumbuke na tukubali kwamba miundombinu ya umwagiliaji na miundombinu ya barabara zetu ni sawa kwa sababu *food security* inategemea kuwepo kwa chakula na chakula kile lazima kitokane na *irrigation*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Hayati Benjamin Mkapa alitoa waraka kwamba *District Cess* ambayo inakusanya kwenye Halmashauri, asilimia 20 irudi kwenye kilimo, lakini tumekaa muda mrefu, hajjawahi kutekelezwa. Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri kipindi hiki iweze kuwekwa kwenye *Finance Bill* ili angalau asilimia 20 ya makusanyo yanayokusanya kutokana na kodi ya mazao basi irudi kwenye kilimo kuliko kumkamua ng'ombe bila kumpa majani, anaweza akafa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile *nature* ya kilimo inahusisha pia masuala ya utafiti ambapo tunatakiwa tutoe fedha mapema. Fedha zote hizi zikitoka, shilingi bilioni 294, basi itasaidia sana katika kuhakikisha kwamba tunaandaa masuala ya kilimo ambayo yanahitaji maandalizi ya haraka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili katika bajeti hii ambalo nilitaka nizungumzie ni sera ya fedha. Serikali kama ilivyo kawaida, haifanyi biashara, lakini *BoT* inawabana Watanzania. Inawabana wafanyabiashara kutoweza kufanya biashara kwa kutosha kabisa kuititia mabenki ya biashara. Wanabana namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kama nilivyosema, sekta binafsi ndiyo *engine* ya kuendeleza uchumi, lakini Benki Kuu inabana mabenki ya biashara kwa kusababisha ukwasi, matatizo ya ukwasi. Mabenki ya biashara hayana fedha za kukopesha wafanyabiashara na Watanzania ili waweze kufanyabiashara pamoja na kulipa kodi za Serikali. Sasa yanababisha matatizo ya ukwasi namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni Serikali na taasisi zake zilikuwa zinaweka fedha zake kwenye mabenki ya biashara, lakini sasa hivi fedha zile zinalipwa moja kwa moja kwenye Benki Kuu ambapo mabenki ya biashara yanakosa fedha za kukopesha wafanyabiashara wadogo. La pili, hati fungani ambazo Serikali inakopa, inatoa riba kubwa sana kiasi ambacho mabenki ya biashara yanashindwa kufanya

biashara ya *fixed deposit*. Kwa hiyo, watu wanakimbilia kwenye hati fungani kufanyabiashara na Serikali badala ya kufanya biashara na mabenki ya biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuna riba kubwa sana ambapo wananchi na wafanyabiashara wanalipa mabenki ya biashara. Hii inatokana na kwamba Benki Kuu inapokopesha mabenki ya biashara inawatoza riba kubwa. Sasa hivi inawatoza asilimia 6.5 na mabenki ya biashara na yenyewe yanatoza asilimia 20; iwe ni *mortgage* au biashara nyingine yeoyote, lakini ni asilimia 20. Sasa cha kufanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri yafuatayo: La kwanza uwekwe utaratibu ili Serikali iweze kupitishia fedha zake kwenye mabenki ya biashara kusudi kuwe na fedha za kutosha za kukopesha watu ili wafanye biashara na waweze kulipa kodi ili tuweze kufikia shilingi trilioni 22 ambazo tunatakiwa tuzilipe kupitia kwenye kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Benki Kuu ishushe riba zake inapokopesha mabenki ya biashara kusudi na mabenki yale yaweze kushusha riba yanapohudumia wafanyabiashara. Lingine ni kwamba, kwenye hizi hati fungani tunaomba kabisa Serikali kupitia Benki Kuu pia washushe riba angalau ifikie asilimia 10 kusudi mabenki yaweze kukopesha, kuchukua fedha za wafanyabiashara kwa *fixed deposit* na wenye angalau waweke asilimia kidogo. La sivyo tutakuwa tumeshaua kabisa kabisa, tutapunguza uchumi wetu. Kwa sababu sasa hivi kusema ukweli tuko kwenye *middle income economy* lakini tusipolinda uchumi huu, itafika pahala ambapo tunarudi kule kule kwenye umasikini mkubwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha aweze kuongea na mabenki ya biashara ili waweze kufungua matawi mbalimbali ya mabenki huko mikoani kwa sababu mabenki mengi yamefungua matawi mengi Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Moshi pamoja na Mbeya wakati mikoa mingine yote haina mabenki kama

hayo. Hiyo ingesaidia kupunguza ghamara kwa sababu wakopeshaji wangekuwa ni wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, sera za *BoT* ziangaliwe. Sasa hivi sera zilizopo ni za kunyanyapaa vijana. Vijana kila wanapotaka kukopa wanaambiwa uwe na nyumba, uwe na *landed property*. Sasa vijana wataweza wapi kupata *landed property* ili waweze kukopa? Kwa hiyo, hilo nalo liangaliwe kusudi vijana waweze kukopa na waweze kuendelea na biashara vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu, ningependa kuzungumza suala la Sera ya bajeti lakini kwa ushauri, bajeti hii ni nzuri na tunaipitisha kwa asilimia 100 lakini ningependa kushauri mambo machache yafuatavyo; jambo la kwanza suala lilikuwa linaathiri sana bajeti zetu ni matumizi ya dharula ambayo hayakupitishwa na Bunge, tunalomba Serikali jjitahidi sana sana isiwe na matumizi ya dharura ambayo yanaathiri bajeti zetu ambazo zimetengwa na Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine ni kwamba labda tufanye utafiti kwa sababu nimeangalia hapa kuanzia mwaka 2005 mpaka leo kuna fedha zinazotengwa na Bunge na zile zinazotolewa kwenye mawizara inafikia tu asilimia 58 mpaka asilimia 67. Nadhani tuangalie inawezekana labda tuna *over estimate* bajeti zetu halafu tunashindwa kufikia malengo kutohaka na uwezo wetu wa kukusanya kodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kwamba tunaomba Serikali iangalie athari za *COVID* au UVIKO-19 ili tuweze kusaidia baadhi ya biashara ambazo zimekuwa *affected* kwa mfano mabiashara ya mahotel ambayo pengine yangeweza kusamehewa baadhi ya kodi ili waweze kusimama kwa sababu wamekua *affected*sana sana na huu ugonjwa wa corona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuona faida ya miradi mikubwa ya kimkakati lazima tuhakikishe kwamba

tunaimaliza mapema tuweze kuona faida yake na iweze kusaidia kujenga uchumi kupitia miradi mingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwamba Serikali iweze kulipa ihakiki madeni ya ndani na iweze kuyalipa ili tuweze kuongeza mzunguko wa fedha na wananchi waweze kuendelea na biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Namuita Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, wakati huo Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, anajianda.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante lakini nikupongeze kwa kweli unatuwakilisha vema sisi vijana hapo kwenye kiti chako hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa bajeti hii nasema kwa dhati kabisa kuna msemo mmoja wa kingereza unasema *all starts well ends well* na katka hili niseme bila kuwa na kigugumizi ama kwa hakika *legacy* ya hayati Dkt. John Pombe Magufuli kamwe haitafutika kwenye ramani ya Tanzania. Kwanini haitafutika tunaye Mama yetu ambaye anakwenda kukamilisha kazi waliyoanza pamoja na hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nimpongeze kwa ubunifufii mkubwa Mheshimiwa Rais na kauli yake mbiu ambayo anasema kazi iendelee. Jambo hili la msingi kabisa na kupitia bajeti hii tunaona kwamba bajeti hii imetoa taswira na dira kwa Taifa letu, inakwenda kugusa wananchi wa hali ya kipato cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lakini unapoongeza ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi maana yake nini? Unalinda viwanda vya ndani lakini pia unaongeza unachagiza ujenzi wa viwanda ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo,

nampongeza Mheshimiwa Waziri kaka yangu Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba kwa dhati kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa dhati hapa waingereza wanasema *normally people they do not care how much know until they know how much you care!* Maana yake nini siku zote watu huwa hawajali jinsi gani unajua mpaka waone jinsi gani unajali. Mheshimiwa Waziri kaka yangu Mwigulu Nchemba katika hili wewe ni Daktari kweli kweli, siyo wale madaktari wengine wewe ni *PHD holder* wa kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu umetafsiri uchumi wa nchi yetu kwenye bajeti hii, hivi vitu siyo vya kawaida sana ndiyo maana vitu hivi lazima akili kubwa ifanye hivi kwa kweli nakupongeza na pamoja na Naibu Waziri kaka yangu Mheshimiwa Eng. Masauni mchape kazi sisi tuko nyuma yenu tutawaunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa sababu kuu zifuatazo ya kwanza tunaona leo hii kulikuwa na ugumu wa makusanyo ya kodi ya *property tax* halmashauri tulipata shida kidogo huko nyuma, baadaye *TRA* nayo haikufanya vizuri. Lakini leo hii unapokwenda kukusanya kodi za majengo kwa kutumia *bill* za umeme kwa kweli tunakwenda kukusanya na naamini tunaenda kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niseme kuna changamoto hapa mbili ambazo watu walikuwa wakizungumza wanasema kuna watu hatutumii umeme tunatumia *solar power* sijui kuna watu tunaweka umeme kabisa. Nishauri hapa katika watu wa kundi hili tuwaache halmashauri waendelee. Kada hii ya watu ambao wanatumia *solar panel* na watu wasiotumia umeme au hawaajaunganishiwa umeme ile kodi iendelee kukusanywa na halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la mpangaji, sijui na mwenye nyumba hii hamna shida hapa ni jambo ambalo linawekwa kwenye mkataba tu na ni mahusiano kati ya

mpangaji na mwenye nyumba na mlipaji na mwenye nyumba. Kwa hiyo, ni jambo ambalo yaani hatuitaji akili kubwa sana kwenye tafsiri hili kwa hiyo, nakupongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu muendelee sisi tutaendelea kuwaunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo jingine niendelee nijikite kwenye sekta nyingine ni sekta ya ujenzi. Tunapozungumzia sekta ya ujenzi ni sekta muhimu sana kwa ukuwaji wa uchumi wa Taifa letu kwa sababu moja kuu kwanza inakwenda kurahisisha huduma za usafirishaji wa bidhaa, bidhaa kutoka viwandani kwenda kwa watumia lakini bidhaa hasa za kilimo kutoka mashambani kwenda kwenye masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu ninashukuru sana na ninampongeza Waziri wa Fedha lakini pia nampongeza Waziri wa Wizara ya Ujenzi, unavyozungumzia miundombinu unazungumzia pia barabara kuna suala hapa kimsingi limegusa wananchi wa Jimbo la Mlimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itoshe tu kusema, Waheshimiwa Madiwani wa halmashauri ya Wilaya ya Mlimba wako kwenye ukumbi wa Spika na wanasikiliza na wenyewe wamekuja kupongeza Wizara hii muhimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kuzungumzia nini? Barabara hizi kuu tunaziita barabara za Mikoa zinaunganisha makao makuu ya mikoa na mikoa faida yake ni kubwa mno. Kwa sababu kwa mfano hii barabara inayokwenda kujengwa kutoka Ifakara Mlimba, Madeke, Lupembe mpaka pale Kibena *Junction*, barabara hii inaunganisha Mikoa miwili, Njombe na Morogoro faida yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Mlimba ambao tunatoka Morogoro sisi tunalima Mpunga, lakini wananchi wa Njombe wenzetu wanashughulika na mazao ya mbao kwa hiyo, tutakwenda *comparative advantage* katika uchumi, maana yake wao wanatupa

mbao tunanunua sisi tunawapa mchele wanakula. Kwa hiyo, ni neema kwa wananchi Mkoa wa Morogoro na neema kwa wananchi wa Mlimba lakini haitoshi hata Jirani zetu wa Njombe. (*Makof*)

Mheshimiwa mwenyekiti, niende kwenye sekta ya ardhi, nikushukuru tena kwa mara nyininge Mheshimiwa Waziri, kitendo cha kupunguza kwenye marekebisho ya Sheria ya Sekta ya Ardhi tunaona Mheshimiwa Waziri unafanya marekeabisho ya Sheria ya Ardhi Sura Na.113 na unatueleza kwamba tozo ya mbele yaani *premium* inakwenda kupungua kutoka asilimia 2.5 mpaka asilimia 0.5 jambo hili ni la kheri kweli kweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka na naomba niseme kwa dhati, Serikali hii ni Serikali sikivu katika mchango wangu wa awali nilichangia kwa habari ya eneo hilli, mheshimiwa Waziri umesikia na umekwenda kupunguza leo naomba nishauri jambo lingine bajeti ijayo muliangalie hili pia. Kuna hii kodi ambayo tunaita *capital gain tax* yaani kodi ya ongezeko la mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi hii inadumaza sana biashara katika sekta ya ardhi, kodi hii ya asilimia 10, Mheshimiwa Waziri bajeti ijayo nakushauri kaka Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, bajeti ijayo tupunguze kutoka asilimia 10 ije asilimia 5 itasaidia *transaction* za kuuziana kwenye sekta ya ardhi na *ita-bust* uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo lingine naomba nishauri ni suala zima la upimaji hapa nimeona na nimeangalia takwimu hapa kwenye sekta ya ardhi mwaka wa fedha ukisoma kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa ukurasa wa 203 inaeleza; Mwaka wa Fedha 2020 viwanja viliviyopimwa nchini na mashamba ni 337,970 kwa mwaka 2020 lakini kati ya hiyo viwanja 90,000 vinatoka Dodoma sawa na asilimia 40 ya upimaji kwa nchi nzima ni takwimu hizi zipo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana nikasema sasa tunaona umuhimu wa sekta binafsi ku-*engage* kwenye

shughuli za upimaji na upangaji wa nchi yetu. Dodoma tumefikia viwanja 90,000 kwa sababu tumetumia sekta binafsi na niseme tu nitaendelea kusema sitasita kwenye eneo hili. Kwa sababu ni mafanikio kwa Dodoma nchi nzima 300,000, Dodoma 90,000 asilimia 40, kazi imefanyika, hili jambo halihitaji fikra ya juu sana ni jambo la kawaida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kidogo niguse kwenye eneo la kilimo lakini nizungumzie sana suala la masoko. Mlimba sisi tunalima mpunga sisi hatuhitaji masoko Mlimba, sisi tunachohitaji Mlimba, tunahitaji kuchakata mpunga kuwa mchele. Tufanye *packaging transport* tuuze Japan tuuze nchi nyingine ili tupate fedha za kigeni. Hili litatusaidia wananchi wa Mlimba sisi hatuhitaji masoko tunahitaji *processing*, unavyozungumzia kuchakata mpunga ukawa mchele ukafanya *packaging uka-brand* tutauza ndani na nje ya nchi na namna hili tu tuweze kusema tutapata fedha za kigeni na tutakuwa na *favorable balance of payment* ndani ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kusema, baada ya kuchangia haya kwa kweli, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni na niombe kwa Waheshimiwa Wabunge, mama yetu Samia Suluhu Hassan ameanza vizuri anahitaji tumsaidie na kimsingi tumpe ushirikiano wa kutukuka. Hoja yangu ya msingi ambayo leo ninaacha swali kwa kila mmoja wetu, Je. *Are we genuine?* Swali langu. Mheshimiwa Rais kwa dhati kabisa anahitaji ushirikiano wetu na kumsaidia swali langu niliache hapa leo katika Bunge letu, *are we genuine?* Ahsante naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Godwin Kunambi, kwa mchango mzuri, sasa namuita Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, wakati huo *okay* endelea Mheshimiwa Nape, nitawataja wanaofuatia.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa wasilisho nzuri la mapendeleko haya ya bajeti ya Serikali na kwa pongezi nilivyozisikia huu ni ushahidi

kwamba Chama cha Mapinduzi kinalea vizuri sana. Maana Mheshimiwa Naibu Waziri alikua mwenyekiti wa vijana wa CCM kwa hiyo alilelewa vizuri, Mheshimiwa Waziri amekua Mweka hazina wa Chama cha Mapinduzi Taifa na Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. kwa hiyo, ni ushahidi kwamba Chama chetu kinalea vizuri na matunda yake tunayaona, hongera sana Mheshimiwa Waziri na timu yako nzuri kwa kazi ambayo mmeifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Rais hii ni bajeti yake ya kwanza, Rais wa Awamu ya Sita na ni bajeti nzuri sana sana katika historia bajeti zetu hii ni bajeti nzuri na kama bajeti yake hii ya kwanza imefanyika hivi nadhani mama tukimpa bajeti kama 10 hivi nchi yetu itakwenda vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumuunge mkono kwa bajeti yake ya kwanza na bajeti zake tano za mwanzo halafu 2025 tumuungeze bajeti zingine tano ili mambo yetu yaende sawa sawa. Kwa tafsiri rahisi kabisa hii ni bajeti ya watu na Mheshimiwa Waziri umetutendea haki maana sisi hapa tumeletwa na watu umetuletea bajeti ya watu umehalalisha kurudi kwetu hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya watu kwanini? Kwanza umegusa maeneo ambayo ni ya muhimu sana suala la barabara vijijini, suala la maji, suala la afya, suala la miundombinu ya elimu, haya ni maeneo makubwa yanagusa watu na kumekuwa na kelele ya muda mrefu ya kushughulika na maendeleo ya watu. Sasa umeya-*identify* jambo la kwanza, lakini la pili umependekeza vyanzo vya fedha ya kwenda kutatua mambo haya hili jambo ni kubwa sana na mimi naunga mkono mapendeleko ya Wabunge wengi kwamba hizi fedha tuziwekee wigo, tuzikusanye ndiyo lakini tuziwekee wigo zikafanye hii kazi uliyokusudia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niwaombe Watanzania tuunge mkono na tulipe kodi ili tujivunie kujitawala ni kujitegemea na haya mapendeleko yanatupeleka kwenye kujitegemea badala ya matatizo haya kuendelea

kutegemea fedha kutoka nje. Mheshimiwa Waziri na Serikali hii tunawaungeni mkono kwa mawazo haya mazuri na ninaomba Wabunge wote bila kujali tofauti zetu, mwisho wa siku tupige kura ya ndiyo ili tukajenge barabara tukapeleke afya tukapeleke elimu tukapeleke maji vijjini. Mheshimiwa Waziri hii kazi nzuri hii ni bajeti ya watu, mmetafsiri vizuri ukuwaji wa uchumi wetu kwenye maisha ya watu tunawaungeni mkono kwenye jambo hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili, nataka kupongeza uamuzi wa Serikali wa kuamua kuangalia upya *finance* ya miradi yetu mikubwa. Hili jambo ni kumbwa sana litasaidia kupunguza mzigo mkubwa kwa wananchi wa kawaida *financing* ya miradi yetu, tumeshaanza wenyewe vizuri hapa tulipo sasa tuangalie *financing* yake na kwenye hili Mheshimiwa Waziri tuweke nguvu tuhakikishe tunafanya *credit rating* ya nchi yetu itatusaidla sana kupunguza hali ambayo tunapambana nayo kwenye mikopo mbalimbali ambayo tumekua tukiomba. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono *credit rating* ifanyike ni wakati sahihi tuko uchumi wa kati *credit rating* itatuweka mahali pazuri sana na tutapata fedha ya kuendeleza miradi hii. Kwa haraka sana nilitaka nizungumze eneo moja kubwa la hisa za Serikali kwenye makampuni, hisa za Serikali kwenye makampuni na hapa nazungumzia makampuni mawili *TIPER* na PUMA na bahati nzuri kuna fedha nydingi za kutosha huku, makampuni yote haya mawili Serikali ina hisa asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TIPER* tuna asilimia 50, na *ORXY energy* wana asilimia 50. Sasa nataka nizungumze namna ambavyo tunaweza tuka *maximize* hisa zetu zikatuletea vyanzo vingine vya mapato. Sasa hivi hapa *TIPER* tuna *infrastructure* ya matenki ya kuhifadhi mafuta. Sasa tusiruhusu wengine ndani ya Serikali humo humo wakatengeneza tena matenki mengine kuna hoja ya bandari kutaka kuingia huko hakuna sababu tutumie yale yale ya *TIPER*. Kuna hoja ya *TPDS* kwenda huku, kila mmoja atomize

wajibu wake kazi hii ya kupokea haya mafuta na kuyahifadhi waachiwe watu wa *TIPER*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa Mheshimiwa Waziri kuna jambo *very specific*, tokea *TIPER* imeanza *MD* wa *TIPER* amekuwa anatoka Ufaransa ambayo ni makubaliano na mimi nakubaliana. Lakini juzi imetokea fursa *MD* aliyopo anajiu zulu, wametangaza wameingia wazungu tatu, mhindi mmoja na Mtanzania mmoja, mtanzania kashinda kwenye mchakato baada ya kushinda kwa mujibu wa taratibu, wenzetu wanatakiwa kutuandikia Serikali tutoe *consent yetu*, *consent* tu tumekaa nalo, tunaangaika nalo na ni kwa roho mbaya tu, kashinda mtanzania, mtanzania akienda kwa faida ya nchi yetu anakwenda kuziangalia hisa zetu lakini tumeng'ang'ana nalo weee! Hivi angeshinda Mfaransa mngefanya vetting? Si mngetoa barua tu akaendelea ameshinda mtanzania roho mbaya mnambanlia ya nini na mkichelewa kujibu wataweka Mfaransa Watanzania hebu viongozi tuondoke kwenye roho mbaya, Mtanzania mwenzetu tumuunge mkono toweni *consent* ya Serikali aendelee, wamekaa wazungu wamemkubali sisi tunaweka roho mbaya hili jambo halikubaliki hii ni kwa *TIPER*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *PUMA* tuna hisa asilimia 50, Mheshimiwa Waziri tunaagiza mafuta hapa ya *bulk* kupitia *PPPA* lakini tunatangaza *tender*, wanaotuletea mafuta ni makampuni ya nje, hapa tuna kampuni yetu ya *PUMA* asilimia 50 ni Serikali yetu. Hivi ni kwanini tusiwatumie hawa hawa tukaagiza mafuta tukapata fedha lakini pia tukapata *income tax* kwa sababu hii kampuni iko hapa na sisi wenye Serikali tunapata. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya sasa hivi tumewaachia makampuni ya nje ndiyo yanayoleta yakituletea tukishawalipa wanaondoka zao lakini na hakuna mtu hatatushangaa kampuni ya *PUMA* ni ya kwetu tuna hisa asilimia 50 lakini ina uwezo wa kufanya manunuzi ya kimataifa tuondoke kwenye kuangaika na hao twendeni tukaitumie kampuni yetu ya ndani tutapata fedha za ziada, tutapata mapato na mambo yetu yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, moja ninaunga mkono bajeti hii asilimia 100, bajeti safi twendeni tukaitekeleze na tumpe nafasi mama na waziri umefanya vizuri na naamini umeanza vizuri na baada ya muda uta-*gain* uzoefu wa kutosha utatupeleka mbele zaidi. Lakini kwenye *financing* ya miradi mikubwa twende kwenye *credit rating* itatutoa hapa tulipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu twendeni tukaangalie matumizi ya hisa zetu kwenye makampuni yetu, na hizi hisa zetu zitatuongeza wigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza kuongeza wigo wa kodi siyo idadi tu ni pamoja na ubora ukiwaongeza uwezo wale ambao wanakulipa kodi alikuwa anakulipa Shilingi 10 ukimuongeza uwezo anakulipa mia 200, unakuwa umeongeza wigo na hapa ndipo ambapo tunalomba Serikali yetu ienda, lakini vinginevyo mimi naunga mkono ninampongeza Rais, kwa bajeti hii amelegeza vyuma sana tumuunge mkono aendelee kulegeza ili mambo yetu yaende, *style* aliyokuja nayo twende nayo tusonge mbele pamoja ninaunga mkono bajeti kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, namwita Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava wakati huo Mheshimiwa Jesca Kishoa na Mheshimiwa Judith Kapinda wanajiandaa.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nimshukuru Mwenyezi Mungu mwiningi wa rehema aliyetujalia uzima, lakini kipekee nitumie nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Fedha kwa hotuba yake nzuri lakini kwa ujumla nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hotuba hii inatoa mwelekeo mzuri sana wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi na inaonyesha namna gani kama alivyosema Kaka yangu Mheshimiwa Nape Serikali yetu inakwenda kuangaika na shida na matatizo ya watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii kuweka kipaumbele kwenye miundombinu ya barabara, kwenye masuala ya maji, kweye kukamilisha umeme vijiji lakini pia kwenye masuala ya afya na elimu hayo ndiyo mambo ambayo wanahangaika nayo Watanzania. Kama fedha zitakazokusanya wa zikitumika vizuri kwenye mambo haya hata huu wasiwasi uliopo kwenye baadhi ya kodi na tozo tulizoongeza utaondoka na niwaombe tu watanzania hatuna namna nyagine ya kuijenga nchi yetu zaidi ya kutafuta na kutengeneza kodi na kukusanya kodi, lazima tulipe kodi tuweze kutengeneza na kuijenga nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kipekee nipongeze kuongeza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 mpaka 35 kwenye magunia ya kitani yale ya *duty* lakini pia kuongeza ushuru wa forodha asilimia 10 kwa nyuzi za plastiki itatusaidia sana wakulima wa mkonge tunakwenda kuongeza soko na kulinda Mkonge wa Tanzania wa nchi hii. Ni jambo ambalo tunalipigia kelele muda mrefu tunashukuru Serikali, imelisikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende tu moja kwa moja kwenye jambo moja ambalo jana Kaka yangu Mheshimiwa Kitandula alisema wameniachia kulizungumza mimi mdogo wao watu wa Tanga na watu wa Morogoro tunataka tuishauri Serikali haswa kwenye kuongeza mapato na hapa nazungumzia sana mapato kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa. Niombe sana Waziri wa Fedha niombe sana watu wa TAMISEMI, watu wa Wizara ya Kilimo na watu wa Kamati ya Bajeti kama wako hapa watusikilize vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yako kwenye ukurasa wa 53 moja ya maeneo yanayokwenda kufanya marekebisho tunakwenda kuirekebisha sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa sura ya 290 na kwenye hotuba yako umesema, tunakwenda kufanya marekebisho, moja ili kubainisha mazingira ambayo kampuni iliyolipa tozo ya huduma haitawajibika kulipa tozo ya uzalishaji na ukasema marekebisho hayo yanalenga kutatua mgongano uliojitokeza kwenye kutafsiri kifungu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeingia humu 2018 miaka mitano iliyopita tumekuwa na changamoto sana kwenye jambo hili, lakini Waziri wa Fedha nikuhakikishie hatukuwa na mgongano wowote wa tafsiri kwenye sheria hii, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Kifungu cha Kumi na Sita inasema *corporate entity* inayolipa *service levy* haitalipa *produce cess* iukienda kwenye sheria yenyewe ya fedha inasema kwa mazao ya biashara mnunuzi anapaswa kulipa asilimia tatu ya *farm gate price* kama ushuru wa mazao kwa maana ya *produce cess* hakuwa na mgongano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tafsiri ya kisheria mgongano uliokuwepo ulikuwa ni mgongano wa kimaslahi nani afanye nini nani alipe nini tukasumbuana miaka mitano hapa na watu wa Wizara ya Kilimo ni mashahidi tumefanya vikao vingi leo limekuja kujitokeza, niliposoma kwenye hotuba yako na kukusikiliza nimerudi kwenda kuangalia *Finance Bill* ambayo inakuja, yanakuja marekebisho ya kurekebisha kifungu hichi kwenye Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda kuongeza specifically tunasema *corporate entity* ambayo inazalisha mazao ya kilimo haitalipa ushuru wa mazao kwa mazao yanayozalisha labda kwa mazao ambayo yanatoka kwa mtu mwagine. Tumesema tunataka kuongeza mapato na mwaka wa fedha tulionao Halmashauri zimekusanya kwa asilimia 88 na tumeongeza makadirio na moja ya vyanzo muhimu vinavyotegemewa ni huu ushuru wa mazao sasa haya mabadiliko yaliyofanyika tafsiri yake ni nini. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni kwamba yale makampuni wazalishaji wakubwa wa mazao tukichukuwa mfano wa zao la mkonge hawatalipa ushuru wa mazao kwa maana *produce cess* labda kama wamechukua mazao hayo kutoka kwa mkulima mwagine ambaye hapo sasa tunamzungumzia mkulima mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya jambo hili ni kubwa inakwenda kutupunguzia fedha na mapato kwenye

Halmashauri zetu na sisi ambao tunalima tunapata shida kidogo ukienda leo *Handeni DC*

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka wapi? Mheshimiwa Chumi.

## TAARIFA

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji, kwamba jambo hilo halitaenda kuathiri tu Korogwe hata Halmashauri ya Mji wa Mafinga, hata Halmashauri ya Wilaya Mufindi hata Halmashauri ya Njombe ambayo tunategemea misitu kwa sababu kwa mfano sisi asillimia 50 ya mapato yetu yanatokana na hiyo ambayo inataka ije ifutwe. (*Makofii*)

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa naomba tu muda wangu ulindwe vizuri. Nina takwimu hapa za Halmashauri nyangi lakini nichukue Halmashauri moja tu ya Korogwe, huko nyuma baada ya kutokea hii mivutano tukaenda mpaka kwenye Kamati ya Bajeti na Mheshimiwa Simbachawene akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, wakasema mgongano wa kisheria hapa nendeni mkatekeleze sheria, sisi wa Mkoa wa Tanga tukaenda kutengeneza *By Laws* kwamba huyu mkulima mkubwa kabla hajatoa mzigo wake usiondoke mpaka awe amepata ushuru wetu wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ni kwamba Sheria ya Fedha inataka mnunuzi ndiyo aliye, wakulima wakubwa wa mkonge wakimaliza kulima wanachukua wanapeleka nje, Halmashauri hatumjui mnunuzi ni nani hatujui ananunua shilingi ngapi tukawa na changamoto, tukaweka sheria kwa mabadiliko haya mnayoyaleta hata ile *By Laws* haitaweza kutekelezeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, chukua mfano wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe asilimia 70 ya eneo letu ni mashamba makubwa ya m Konge kwa hiyo m Konge ndio madini yetu, m Konge ndiyo kila kitu na ukitaka kuona hilo mwaka wa fedha tulionao kwenye bilioni moja na milioni tisa na kidogo mapato yanayotokana na ushuru wa mazao kwenye m Konge peke yake ni milioni 425 sawa na asilimia 39 ya mapato yetu. Leo ukiondo *produce cess* tunapata wapi mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu kupunguza mapato lakini pia mnatuletea mkanganyiko, huyu mkulima mkubwa ambaye anaambiwa asilipe *produce cess* kwa tabia ilivyo pia wanununa kwa wakulima wadogo, tunatofautishaje kati ya mkulima mkubwa na mkulima m dogo mazao yapi yametoka wapi hatuwezi kutofautisha, lakini shida ya pili kama mkulima mkubwa halipi *produce cess* maana yake mazao ambayo yana uhakika wa kulipa ushuru wa mazao ni mazao anayolima mkulima m dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake nini ukiwa na mnunuzi *independent* aliyekuja kutoka nje kwenda kununua mazao kwa wakulima wadogo ni lazima atafuata hiyo tozo tunayotaka tuichukue Halmashauri, kwa hiyo atapunguza bei kwa mkulima wetu ili aweze kupata nguvu ya kulipa ushuru na kununua yale mazao. Wakati huyu mwingine anachukuwa mazao yake anapeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilitokea mwaka 2019 mwishoni alikuja mnunuzi kampuni ya Kichina kununua m Konge akakuta kuna ushuru wa mazao kwa wakulima wadogo ukinunua, akatakiwa kulipa, akaona kuliko kulipa ule ushuru ni bora aache, ilitumika busara ya Mkuu wa Mkoa kuwaomba halmashauri wasamehe ili ule ushuru wa mazao hili mnunuzi huyo anunue wakulima wasiumie. Maana yake ni kwamba mazao ya wakulima wadogo yanakwenda kushindanishwa na wakulima wakubwa, akitosekana mnunuzi *independent* kwa sababu ya hii kodi, wakati hawa makampuni makubwa hawalipi, wakulima wetu watakuwa hawana *option zaidi* ya kuwauzia hawa wakulima wakubwa

ambao wana makampuni na mashamba kule kwenye maeneo yetu, wakienda kuwauzia bei ya mkonge itaporomoka, bei ya mkonge wataipanga wanavyojisikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha na ....

**MWENYEKITI:** Nimemwona Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge, Mtendaji wetu wa CCM Mstaafu anayejenga hoja kwa umakini mkubwa sana, amewakilisha Halmashauri nyingi tu, nilitaka nikiombe Kiti chako, Mheshimiwa Mbunge pamoja na mwingine aliyetoa hoja, tukahirisha Bunge hapa tukakae na timu yangu ya wataalam wanaoandaa *Finance Bill* tulipitie hilli jambo ili tulirekebishe ili tunavyo *print documentya mwisho* iwe imekaa sawa kwa maslahi mapana ya nchi yetu. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnzava unaipokea taarifa?

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa uungwana huu mkubwa uliouonyesha. Kwenye hili Mheshimiwa Waziri wa Fedha nataka niendelee kusema mengine Iakini kwa uungwana uliouonyesha kwenye hili naishia hapa tutaonana tuliweke vizuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie na moja tu maana Mheshimiwa Waziri wa Fedha nimefurahi sina haja ya kuendelea sana nimalizie na moja dogo. Tusaidieni tumeanzisha tozo kwenye zile skimu za umwagiliaji kwa maeneo ambayo yanakuwa yanasmamiwa na Vyama vya Ushirika na skimu za umwagiliaji kwa ujumla, hii iwe chachu ya kutufanya tuongeze fedha zaidi kuwa na miradi mingi, watu wa Korogwe kwa mfano, wanaangaika kwa zaidi ya 20 na Bwawa la Mkomazi bilioni sita inahitajika. Ukienda kilimo

wanasema tumepeleka Hazina, ukienda Hazina na tungeweza kupata mapato mengi kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwita Mheshimiwa Jesca Kishoa wakati Mheshimiwa Judith Salvio Kapanga anajiaandaa kwa ajili ya kuhitimisha.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba mimi ni Mbunge wa Kambi ya Wachache lakini pia pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mwigulu Nchemba amekuwa ni mpinzani wangu kwa *term* mbili mfululizo Jimboni kwangu Iramba Magharibi na nikiri kwamba tulitifuana kwelikweli, lakini ninaomba nikiri kwamba na bila kigugumizi kwamba bajeti hii ni miongoni mwa bajeti ambazo ni bora sana ambazo tumewahi kuwa nazo katika Taifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ni bora kwa sababu inakwenda kutua mzigo wananchi wetu, tumeona tozo nydingi zimefutwa, kodi, ushuru mbalimbali zimefutwa kama ambavyo zimeonekana kwenye ukurasa wa 28 na 31 wa kitabu cha bajeti. Kwa kusema hivyo ni wazi kwamba kama Serikali inaweza kuwapunguzia mzigo mkubwa wananchi wa tozo hizi, inatakiwa kugombezwu au kupongezwa, inatakiwa kupongezwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi yapo mambo ambayo lazima tushauri, nchi yoyote ambayo inaweza ikaonesha ina uwezo wa kujidhesha na kujisimamia kiashiria kikubwa kabisa ni kwenye mapato yake ya ndani, ukiangalia kwa mujibu wa sura ya bajeti yetu utaona kwamba tunatarajia kukusanya trilioni 26.03 mapato ya ndani, ukiangalia matumizi ya kawaida tunatarajia kuwa na trilioni 23 *point something*, sasa ukichukuwa mapato ya ndani

ukatoa matumizi ya kawaida unabaki na trillioni *three point something*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tusingekuwa na mikopo na misaada ya kibajeti ni wazi kwamba tulikuwa tunakwenda kutumia trillioni tatu kwa ajili ya miradi ya maendeleo jambo ambalo siyo zuri sana. Mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali inatarajia kukusanya trillioni 36.33 na ukiangalia katika bajeti yetu tunategemea, bajeti yetu inategema takribani asilimia 30 ya mikopo ya kibashara na misaada kutoka nje na ndani lakini kwa mazingira kama haya na ninaomba hapa Mheshimiwa Waziri anisikilize vizuri kwa mazingira kama haya nina ombi ni vema vyanzo vyote ambavyo zimebekwa kwenye *Finance Bill*, ambavyo vimetengwa kuwa mahsus kwa ajili ya kuchangia miradi ya maendeleo, vyanzo hivi viwekewe zuio kuwepo na akaunti ambayo itakuwa ni *special* kwa ajili ya kutunza vyanzo hivi, kwa mfano tozo ya *lane za simu*, miamala ya fedha, *petrol* na tozo nyingine, fedha hizi zipewe akaunti maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalisema kwa sababu tusipofanya hivyo tutajikuta tunaingia kwenye mtego mbaya sana wa kukusanya tozo hizi tukapeleka kwenye mfuko wa Serikali halafu zikapangija matumizi mengine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili Mheshimiwa Waziri *you must be very smart* kwa sababu mwisho wa siku utakuja kubeba mzigo ambao utashindwa kuutua, kama tunaona kuna kazi kuweka kwenye akaunti *special* basi tunaweza tukazipeleka Serikali Kuu lakini tukaweka kwenye *special reserve fund* kwa ajili ya matumizi ya kutelekeza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye akaunti hii ambayo itatengezwa kwa ajili ya kutunza fedha hizi, basi *CAG* apewe mamlaka kamili ya kuweza kukagua na kupitia kwa ajili ya kuhakikisha kwamba fedha ambazo zimekusudiwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zinakwenda kuliko kusudiwa, na hii itawapa *confidence* hata wananchi ambao wanakatwa tozo hizi, kwenye *lane za simu* na maeneo

mengine kwamba watakuwa wanaona moja kwa moja wanachangia fedha na inakwenda kutekeleza miradi ya maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nina hoja yangu nyingine ambayo ningemuomba Mheshimiwa Waziri wakati wa hitimisho, basi ajaribu kutoa ufanuzi zaidi kwenye tozo hizi, kumekuwa kuna ukakasi na kupindishapindisha na kutokuwa na uelewa wa tozo ambazo zimesoma kwenye bajeti hii. Ukweli ni kwamba bado tozo hizi hajizaeleweka vizuri na nina wasiwasi mkubwa kwamba kuna uwezekano mkubwa wananchi wakaingia kwenye mtafaruku wa namna mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano kwenye hii tozo ya hawa watu wa bodaboda, ukiangalia kwamba Serikali kwenye bajeti imemelea kwamba imeshusha kutoka elfu thelathini mpaka shilingi elfu kumi, lakini ukiangalia faini hii hiyo shilingi elfu kumi ambayo imeshushwa ni kosa moja, kuna hatari kubwa ya *traffic* kupambana na bodaboda kwa sababu bodaboda wanaamini kwamba ni kwa makosa yote kama ambavyo ilikuwa awali kwa shilingi elfu thelathini, kwa hiyo ni vizuri vitu hivi mkavitolea ufanuzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka nimalizie na hoja nyingine ambayo inahusiana na namna ya matumizi tumejikita sana kujadili namna ya kutumia fedha, ningependa sasa hivi nijaribu kuelezea kwamba ni namna gani bora tunaweza tukakusanya fedha na tukadhibiti mapato, wote tunajua kwamba Serikali yetu inamiliki *shares* kwenye makampuni mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo makampuni ambayo Serikali ina *total ownership* lakini yapo makampuni ambayo Serikali inamiliki kwa asilimia Fulani, lakini kumekuwa kuna tabia ya makampuni haya kuwa yanatoa taarifa ambazo siyo sahihi kwenye mitaji yake, kwenye gawio Serikalini, lakini hata kwenye faida inayoingiza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haikagui, Serikali haina mamlaka ya kukagua makampuni haya kwa sababu ya sheria ambayo inamzuia *CAG* kukagua makampuni ambayo Serikali inamiliki *less than 50 percent*. Nina mapendekezo ninaomba Mheshimiwa Waziri Mwigulu Nchemba mnaweza mkapeleka *shares* zile ambazo Serikali inamiliki *less than 50 percent*, mkazipeleka kwenye *stock market* mkazipeleka kwenye *stock market automatically share* hizi makampuni haya yatafanyiwa ukaguzi na zile fedha zitakuwa wazi kwa sababu kule kwenye *stock market* wanafanya *scrutiny* ya hali ya juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo tutakuwa tuna nafasi ya kujua kile ambacho tumeingiza kina uhalali kiasi gani. Pia nina pendeleko lingine tunaweza tukabadiisha sheria yetu tukampa mamlaka *CAG* akafanya ukaguzi hata kwenye makampuni yote ambayo Serikali inamiliki *less than 50 percent* bila kujali *shares* zetu ziko kiasi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendeleko la mwisho ambalo ni muhimu sana ni muhimu tunaweza tukaunda *PIC* (*Public Investimate Company*) ambayo kampuni hii itakuwa ni kampuni inayomiliki hisa ambazo Serikali inamiliki *minority shares*, tukiwa na hii kampuni, itatusaidia kuhakikisha kwamba hesabu zote zinakuwa wazi, zitalazimika kukaguliwa kwa sababu inakuwa ni kampuni tanzu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Judith Salvio Kapanga atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu vijana katika Taifa lolote duniani ndiyo wadhamini wa Maendeleo wa Taifa hilo yaani *they are the trustees of prosperity in the nation*. Lakini vilevile vijana katika Taifa lolote

ni zawadi kwa Taifa hilo na ndiyo maana kuna msemo unaosema wazee watatangaza vita, lakini ni vijana watakaoenda mbele kupigana au kufariki yaani *all the men declare war, but it is the youth must fight and die.* (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nusu ya watu wote duniani yaani asilimia 50.5 ni vijana chini ya miaka 30; nasema haya kwa sababu Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan siyo Rais wa wastani hata kidogo, *she is not an average president* anafahamu na anatambua vijana wa Taifa hili ndiyo walilobeba mustakabali wa Taifa hili kwa namna moja ama nyiningine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan anatambua makali yetu ya Taifa ya kesho yatazimwa na vijana wa Taifa hili na ndiyo maana juzi katika mkutano wake wa vijana aliahidi mkeka utakaokuja utasheheni na kupambwa na vijana wa Taifa hili. Ila sasa hapa tunamuomba Mheshimiwa Rais aharakishe kwa sababu wananchi mtaani wanalamika kwamba nazi zimepanda bei (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema maneno haya kwa sababu Rais anafahamu nguvu ya vijana na ndiyo maana tarehe 15 alituita pale Mwanza kuongea na sisi na kutupa moyo na kutupa muelekeo wa Taifa hili. Ndiyo maana nasema kwamba Rais wetu Samia Suluhu Hassan *she is not an average president at all*, anatambua kwamba vijana ndiyo walioikamata dunia hii, kwa hiyo, kwa mantiki hiyo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa mkutano ule, tunasema kwamba sisi kama vijana ametuthamini kweli kweli, sisi kama vijana ametupenda kweli kweli na sisi kama vijana ametujali kweli kweli. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama vijana tunamuahidi kufanya kazi kwa kuwa ametupa ari ya kufanya kazi, ametupa nguvu, lakini vilevile ametupa hamasa ya kuendelea kum-support kwa kila jambo atakalolifanya kwa sababu mambo anayotufanya sisi vijana wa Taifa hili ni ya mfano na tunatiwa moyo kweli kweli. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba kwa bajeti hii ya Serikali ambayo ipo mbele yetu Rais wetu Samia Suluhu Hassan anaupiga mwingi kweli kweli na ninataka niseme hapa kwamba Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan anaenda na *trend* za dunia inavyoenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani kwa lugha moja ama nyingine anaongea lugha moja na ulimwengu wote kwa ujumla na ningependa niwape mfano mmoja; wakati sasa hivi dunia inaenda kwenye *deployment* ya mtandao wa 5G ambao unaenda kuongeza *global economic value* ya *USD* triliioni 13.1 lakini inaenda kuongeza ajira takribani milioni 22.1. Juzi Mkurugenzi wa *TCRA* alifanya mukutano akatuambia Tanzania kwa mara ya kwanza tunaenda kwenye majaribio ya 5G; mtandao ambao kama leo ulikuwa una-*download movie* yako ya 20GB kwa zaidi ya lisaa limoja unaenda kui-*download* kwa sekunde moja mambo ambayo sisi kama Taifa tulikuwa hatufikirii kama tutafika huko, lakini Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan anatuonesha mfano wa namna ambavyo tunapaswa kuongea lugha moja na ulimwengu wote kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati naongea haya Mheshimiwa Rais pia alijiuliza itawezekana vipi tukafikia malengo haya makubwa ya kintandao kama Watanzania wengi kwa kiwango kikubwa hawana *smartphone*. Kodi ambayo imefutwa ya VATlabda kwa ambao hawafahamu ukileta simu hapa nchini kulikuwa kuna kodi tatu ambazo simu ilikuwa inatozwa; ya kwanza - *custom processing fee*; ya pili - *railway development fee* na ya tatu - *VAT* ambapo *custom processing fee* ilikuwa ni 0.6 percent, *railway development fee* ilikuwa ni 1.5 percent na *VAT* ilikuwa 18 percent. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani leo ukiingiza mzigo wako wa milioni 10 kodi ambayo ulikuwa unalipia ni asimilia 20.1, kodi ambayo imeondolewa ni asilimia 18 kwa hiyo, kodi ambayo imebaki kwenye simu ni asilimia 2.1 yaani labda niongee kwa lugha rahisi, ukiwa una mzigo wa milioni 10 kodi yako ilikuwa ni 2,010,000 yaani asilimia 20.1, lakini leo hii una mzigo wa milioni 10 kodi ambayo unachajiwa badala ya

milioni 2,100,000 ni shilingi 210,000 ni zaidi ya asilimia 97 ya kodi katika hizi simu ambazo zinaingizwa yaani simu janja, vishikwambi na *modem* imeondolewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema kufikia asilimia 80 ya watanzania wanaotumia mitandao ifikapo 2025 siyo ndoto ni suala ambalo linatekelezeka na litatekelezeka kabla ya 2025 na sisi kama vijana wa Taifa hili tunamshukuru Mheshimiwa Samia kwa sababu hapa ndipo ambapo tumejajiri kwa kiasi kikubwa sana. Kwa kweli ndiyo maana naendelea kusema bajeti hii Mheshimiwa Rais anaupiga mwingi kwelikweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tunashukuru kwa haya yote tungependa tuishauri Serikali masuala machache ambayo inabidi ifanyie kazi; moja, tunaomba Serikali ifuatilile masuala ya fedha za mtandao za simu kwa watu ambao wanafariki, yaani *Tigo Pesa*, *M-Pesa*, *Halotel Money*, *Zantel Pesa* zote hizo naona kwamba utaratibu haujaka vizuri na tunaona kwamba kuna fedha zinapotea za watu walifariki kwenye mitandao ya simu ambazo haziwi *claimed*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliopo sasa hivi tunatambua sheria inasema kwamba, ili uweze ku-*claim* fedha *either* katika mitandao ya simu au benki kuna utaratibu wa kufuata ule wa wasimamizi wa mirathi, lakini kwa dunia tunavyoenda sasa hivi tunaona huu utaratibu upo *very complex* kwa sababu ili uweze ku-*claim* hela za ndugu zako; kwanza huwezi kuambiwa salio mpaka uende na barua ya kuthibitishwa kama msimamizi wa mirathi na uende na viambatisho vingine ambavyo pamoja na hivyo. Lakini utaratibu huu wa kimahakama unachukua zaidi ya miezi mitatu au sita na sheria inasema kwenye mitandao ya simu *line* inafungwa baada ya miezi mitatu baada ya hapo hela inawekwa kwenye *holding fee*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi dunia inapoenda kwa nchi za wenzetu kama Uganda kuna mitandao ya simu ambayo mtu akienda *next of kin* wake yaani mnufaika wake

pamoja na uthibitisho wa marehemu kwamba amefariki na cheti cha kufariki anapatiwa hizi fedha. Tunaomba kwenye suala hili utaratibu uimarishe ili kuweza kuwalinda walaji, lakini vilevile kuhakikisha fedha hizi hazipotei na wanufaika wa makampuni ya simu hawanufaiki wao peke yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu pia hata *line ikifungwa* ndani ya miezi mitatu kuna fedha zinabaki kule, lakini hakuna utaratibu wa ku-*claim* fedha hizi kwa walaji ama kwa Serikali. Kwa hiyo, tunaomba suala hili fedha za watu wanaofariki kwa sababu siyo wote ambao wana-*claim* iangaliwe kwa namna moja ama nyingine ili hata Serikali iweze kuongeza fedha hapo ili makampuni ya simu wasinufaika wao peke yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua Mheshimiwa Waziri alisema itakuja sheria ya *Data Privacy and Protection Act*, lakini tunaona suala hili ni la muhimu sana kuna fedha nyingi sana zinapotea hapa za waliofariki, tunaomba Serikali ifuatilie. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine ambalo ningependa nishauri kuhusiana na *charge* za kwenye mitandao ya simu. Sasa hivi ukiwa unatoka kwenye simu unataka kuchukua hela benki yaani unatumia zile *USSD code*...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani naomba nimalizie kwa dakika moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano *NMB \*150\*66#* makampuni mengine yote ya simu una-*dial*/nyota hiyo, yaani *charge* yako inaenda benki yaani uhitaji kuwa na salio ili uweze ku-*access* benki yako, lakini kwa *Vodacom* huwezi ku-*access* mpaka uweke salio la kawaida hata kama ukiwa na *bundle* hata kama ukiwa na *bundle* haikubali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali itusaidie *Vodacom* wabasilishe utaratibu huu ili sisi tuweze ku-access benki zetu na kama kuna ma-charge waende kwenye benki. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia 100 bajeti hii na ninakushukuru sana. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa *session* yetu ya asubuhi saa tatu mpaka saa saba na kabla sijahitimisha naomba nitambulisse wageni wachache waliopo Bungeni.

Wageni wanne wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri wa Maji ambaao ni familia yake kutoka jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Elizabeth Lukaza, ahsante. (*Makof!*)

Wageni 41 wa Mheshimiwa Godwin Kunambi, Mbunge ambaao ni Waheshiwa Madiwani wa Halmashauri ya Mlimba na Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Kilombero wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Ndugu Innocent Mwangasa, ahsante. (*Makof!*)

Wageni 28 wa Mheshimiwa Abdallah Chikota, Mbunge ambaao ni wachezaji wa *Ocean Fitness Centre* kutoka Mkoani Mtwara wakiongozwa na Ndugu Bakari Self. (*Makof!*)

Lakini pia yupo baba yake mzazi wa Mheshimiwa Shamsia; Mzee Azizi Mtamba, ahsante. (*Makof!*)

Tunao wageni 41 wa Mheshimiwa Joseph Kamoga, Mbunge ambaao ni wanafunzi wa Vyuo Vikuu vilivvopo Dodoma ambaao ni wenyeji wa Ludewa wakiongozwa na Ndugu Steven Mwasanga, karibuni sana. (*Makof!*)

Pia tuna wageni 63 wa Mheshimiwa Rashid Abdallah, Mbunge na Mheshimiwa Maryam Azan ambaao ni wana kikundi cha mazoezi cha *Gombani Fitness Club* kutoka

Chakechake Mkoani Pemba wakiongozwa na Ndugu Issa Juma. (*Makofi*)

Tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde ambaao ni wajumbe wa *Mothers Club* kutoka jjini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Gillian Samanyi, pia karibuni, ahsante. (*Makofi*)

Tunao wageni wa Mheshimiwa Suma Fyandomo kutoka Kanisa la Moravian Ushirika wa Katumba Rungwe Mkoa wa Mbeya ambaao ni waombaji, waimbaji na wachungaji, karibu sana sana Bungeni. (*Makofi*)

Tunao wageni wa Mheshimiwa wa Nicodemus Maganga, Mbunge ambaao wanatoka Jimbo la Mbogwe ambaao ni walimu, ahsante sana na karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninasitisha kikao hiki cha Bunge mpaka saa 11:00 jioni ya leo.

(*Saa 07:10 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11:00 Jioni*)

(*Saa 11.00 Jioni Bunge Lilitrudia*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Sasa namwita Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Isack Mttinga, wakati huo Mheshimiwa, Sanitiel Eric Kirumba, anajandaa.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyezekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa afya na nguvu. Jambo la pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa bajeti hii ambayo ni nzuri kwa kweli, inatia moyo. Kipekee nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu, kwa kasi aliyoanza nayo kwanza ya kuibua miradi mipyä, lakini pia kuendeleza miradi ile ambayo iliachwa na mtangulizi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa ambalo linaelekea kujitegemea, lazima tuhakikishe tunawekeza kwenye mapato ya ndani, hasa hasa upande wa kukusanya kodi. Ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, mapato ambayo yanakusanya kutokana na kodi ni asilimia 4.5 ambayo inatoka kwa watu milioni 2.7. Kwa kweli bado tunayo kazi kubwa ya kuhamasisha Watanzania kulipa kodi. Hili jambo Waheshimiwa Wabunge, tusiachie Serikali, tunahitaji kuwa mstari wa mbele. Tunakuja hapa tunahitaji maendeleo, tunahitaji barabara, tunahitaji maji na huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya yote hayo, lakini tusipohamasisha Watanzania kukusanya kodi, siku moja mara mbili hivi, nimeenda kule Kariakoo. Ukinunua vitu vya milioni mbili, unashangaa wanakwambia tuandike shilingi 300,000, sasa ni wangapi ambao wanafanya hivi? Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, lazima tuwe mstari wa mbele kuhakikisha tunawahamasisha Watanzania kukusanya kodi, ndio tutaweza kufika kujitegemea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Serikali imekuwa ikiweka nguvu sana kwenye viwanda. Hapa niishauri Serikali, viwanda hivi viendane na kilimo, ili viwanda vyetu viweze kupata malighafi ambazo zinatoka ndani. Kwa sababu, tutakapopata malighafi zinazotoka ndani nina uhakika uzalishaji utapungua. Kwa hiyo, hili lazima Serikali iliangalie, tuwekeze sana kwenye kilimo. Tumekuwa tukiimba, Mungu ametujalia Taifa lina ardhi nzuri, tuna vipindi virefu vya mvua, hebu tutumie fursa hii au nafasi hii, ambayo Mungu ametujaalia kuweza kuwekeza kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo hiki ili kiwe na faida, lazima tuhakikishe tuna soko la uhakika, wataalam watoke waende kutafuta masoko. Tusiishie kukaa ndani, tukaishia kukaa maofisini bila kutafuta masoko na ili tutakapotafuta masoko, nina uhakika uzalishaji utaongezeka, kwa sababu, mkulima atakuwa na uhakika ni wapi anaenda kuuza mazao yake. Kwa hiyo, hili nalo tulipe kipaumbele tuliangalie sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilisemee, niipongeze Serikali kwa upande wa vijana wetu hawa wa bodaboda. Hii ni ajira, niiombe sana Serikali pamoja na kupunguza hii kodi, bado niiombe Serikali upande wa Polisi tusijikite kutoza faini. Tutoe elimu kwa vijana hawa na hili naamini litawasaidia kwa sababu, hii ni ofisi kama zilivyo ofisi nyingine. Vijana hawa wanafanya kazi kwenye mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilisemee, niipongeze Serikali kwa upande Madiwani. Tumefanya kazi nzuri, lakini Madiwani hawa wamechaguliwa kama sisi. Pamoja na malipo yao kulipwa na Serikali kuu, lakini niiombe sana Serikali, iangalie namna gani ya kuboresha posho ya hawa Madiwani ili iweze kuendana na kazi wanazozifanya. Waheshimiwa Wabunge leo hii sisi tupo hapa, lakini wanaofanya kazi kubwa ni Waheshimiwa Madiwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba, tunao hawa watu wetu Wenyeviti wa Vijiji. Kwa kweli niseme Serikali hili jambo lazima iliangularie, inaitwa Serikali ya Vijiji, ni Serikali gani ambayo Mwenyekiti wa Kijiji halipwi, hakuna chochote anachokipata. Kwa hiyo, niombe, tumeboresha kwa Watendaji, tumeboresha kwa Madiwani, hebu twende kuangularia, Wenyeviti wetu wanafanya kazi kwenye mazingira magumu. Mwenyekiti yuko ofisini lakini hakuna anachopata. Mwisho wa siku ndio maana hawa Wenyeviti wa Vijiji wanaanza kuwaibia wananchi. Kwa sababu, hana kipato mwananchi akija kupata huduma, anachomwambia lazima uache Sh.20,000/=. Kwa hiyo, niombe sana Serikali hili iliangularie na lenyewe ilipe kipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niipongeze Serikali, leo hii tumepata chanzo cha mapato kwenye barabara zetu. Niombe na niishauri Serikali, tunataka tuone hizi fedha zinaenda kufanya kazi kwa wananchi. Nina uhakika wananchi wetu hawana shida kwa sababu, hizi fedha zitakapokatwa kwenye simu, zinaenda kutoa huduma

kwa wananchi wetu. Zinaenda kujenga barabara, zinaenda kuboresha miradi ya maji na afya na tunaenda kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamefanya kazi kubwa, kama wameweza kujenga maboma ya mamillioni, leo hii ukiwaambia Watanzania wachangie miradi ya maji, wachangie umeme, wachangie barabara, sidhani kama lina shida. Kinachotakiwa, hizi fedha lazima ziwekwe kwenye Mfuko Maalum, ziende kufanya kazi iliyokusudia, watu waone huduma za maji, watu waone umeme, watu waone barabara. Kwa hiyo, niombe sana Serikali hili nalo iliangularie sio mnaweka tu, maana kuna fedha nyingine inaweza ikakusanywa, lakini mwisho wa siku ikatumika tofauti na iliyokusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie jambo lingine la *Corona*, niipongeze Serikali kwa juhudhi ambazo zimekuwa zikifanyika. Hata hivyo, niwaambie ndugu zangu, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, Taifa hili ni Taifa la Mungu na ninyi mtakuwa mashahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majirani zetu wanaotuzunguka sio kusema hawachukui hatua kama sisi, lakini Mungu analo kusudi na Taifa la Tanzania. Kama italazimika kutumia barakoa, tutazitumia, kama italazimika kupata chanjo tutazipata, lakini nataka niwaambie Watanzania, kama tusipoendelea kumpa nafasi Mungu, ambaye amelilinda Taifa hili, wenzetu wanakufa, lakini Taifa hili lipo salama. Hatua zote tuchukue, lakini lazima tutambue, Mungu ndiye namba moja. Tusipompa Mungu nafasi namba moja, tutachoma hizo chanjo, tutavaa barakoa hizo na tutakufa. Taifa hili liko salama kwa sababu, Mungu analo kusudi na Taifa la Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Francis Isack Mttinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii, ambayo ni nzuri na inatia moyo sana Watanzania. Nichukue nafasi hii kumupongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote, kwa kuchukua mawazo ya Wabunge kwa kiasi kikubwa sana na kuyaweka kwenye bajeti hii. Hili linafanya hata sisi tunapochangia, tunakuwa na moyo kwa kuamini kwamba Serikali inatusikia. Kwa hiyo, nimshukuru sana kaka yangu Mwigulu na ukizingatia ni Jirani yangu pale Jimboni, basi najisikia furaha sana kwa jinsi kazi nzuri anayoifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamesemwa, tunarudia kukazia pale ambapo tunaona ni muhimu zaidi pia na kwa sababu jambo likisemwa na wengi linakuwa pia ni sauti ya Mungu, naomba tu nijikite kwenye suala la elimu haswa ya Sekondari. Nishukuru kwamba Serikali sasa inaenda kutujengea shule moja kwenye kila Kata, shule kamili hasa katika kata mpya na zile kata kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sana kuikumbusha Serikali kuziimarisha shule zetu za Kata ambazo tumezijenga pamoja na wananchi nchi nzima. Shule hizi zilanza kwenye wakati mgumu, lakini zimeendelea kuimarika mpaka zimetoa wataalam wakubwa katika nchi hii. Hata hivyo, bado shule hizi zina changamoto kubwa. Kama tunavyofahamu kata zetu hazina tofauti na baadhi ya wilaya, kata zetu ni kubwa sana na shule hizi zimejengwa katika maeneo ambayo iweze kuhudumia angalau vijiji vyta kwenye kata hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nchi yetu hii kijiji hadi kijiji kuanzia kilometra 10, 15 mpaka 20 ni jambo la kawaida kabisa. Kwa hivyo, watoto wetu wa kike na wa kiume wanatembea mwendo mrefu sana mpaka kufika shulen. Huko wanakutana na majanga mbalimbali, watoto wa kike wanabakwa, watoto wa kiume wanajingiza kwenye vitendo viovu mpaka kuvuta bangi. Hii inapelekea mpaka wazazi wanaamua sasa kuwapangishia vyumba watoto wao, karibu na maeneo ya shule katika mazingira magumu sana, vyumba vinaitwa mageto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa Mkuu wa Wilaya ya Chemba, nimefika nakutana na watoto wanakaa geto. Sasa mtoto wa *Form One*, anaenda kusoma anakaa geto, ajitegemee, mazingira magumu, hakuna umeme, halafu tunategemea kwamba mtoto huyu apate elimu bora, ni jambo gumu sana. Hata Walimu wenywewe, inabidi wakatafute mahali pa kuishi mbali sana na shule. Wanatumia usafiri, wengine wanatembea kwa miguu, wengine wana pikipiki, anafika shulenii amechoka, atoe elimu bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naomba nitoe ushauri kwamba, pamoja na hii nia nzuri ya kuanza kujenga shule mpya. Niombe Serikali iangalie jinsi ya kuimarisha hizi shule zetu, sasa tuzijengee mabweni ya wasichana na wavulana ili watoto wetu wakae shulenii. Kwa sababu, Serikali inalipa ada, mzazi tukimwambia alipie chakula kwenye hosteli atalipa. Atampa mtoto wake chakula kile ambacho angekula nyumbani, sasa atakipeleka hosteli ili mtoto akee shulenii aweze kula chakula kile kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali ijenge nyumba za Walimu ili Walimu wakae shulenii. Ni kweli tunalalamika kwamba, elimu yetu ina tatizo, watoto wetu wana akili sana, lakini mazingira tuliyowapa ni magumu. Shule hizi tulizianzisha, zimetusaidia, lakini tuendelee kuziimarisha. Naamini kabisa fedha ambayo inayotumika kujenga shule kila kata, ingetumika kuimarisha hizi shule kwa kujenga hosteli na mabweni, *impact* yake ingekuwa kubwa zaidi pengine kuliko hata hii shule moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikatai shule ni kitu kizuri, lakini kama ningeambiwa kipaumbele, ningeona ni bora tujenge hosteli kwanza kwenye hizi shule za wasichana na wavulana, ili shule hizi za kata zilizopo ziimarike. Kwa sababu, hata aliyepo mbali, hata aliyopo kwenye kata mpya kama shulenii kuna hosteli atakwenda kukaa kule na atapata elimu bora. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu hizi shule tusizisahau, tukaanza kujenga shule mpya kubwa kubwa, wakati kuna shule ambazo tukiziimarisha tutakuwa na *impact* kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihamé niende kwenye suala la mikopo ya hawa vijana. Kwa kweli, Serikali yetu ina nia njema, imetenga fedha kwa ajili ya vijana, halmashauri hata kwenye Wizara, imetenga fedha kwa ajili ya akinamama, lakini, urejeshaji wa hii mikopo umekuwa mgumu sana. Vijana wamechukua fedha, miradi imekufa, halmashauri inashindwa kuwapeleka mahakamani na hata ukiwapeleka dhamana zenyewe hakuna. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ile fedha inapotea na vijana wengine ambao hawakupata mkopo wanakosa. Kwa hiyo, ningeshauri, tufike mahali tubadilishe mbinu ya jinsi ya kutoa hii mikopo. Serikali itengeneze mradi, mradi ukamilike. Kama ni mradi wa nyuki inunue mizinga, itundike, ikusanye vijana, iwave elimu jinsi ya kufuga nyuki, inawakabidhi, ni rahisi kuwa-*monitor* ili waweze kurudisha ile fedha. Kama ni ufgajli wa kuku inunue *incubator*, ijenge mabanda, itoe elimu kwa vijana, wanakabidhiwa pale, ni rahisi kuwa-*monitor* na kurudisha ile fedha na wengine wapate. Hii kuendelea kutoa *cash* tunapoteza fedha na hakuna *impact* tunayoiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri kwamba, tubadilishe huu mtindo, kuliko hii fedha ziendelee kupotea, tutengeneze miradi. Kwanza hii njia italeta ajira ya uhakika, kwa sababu ukitengeneza mradi unachukua vijana wote kuanzia wa darasa la saba mpaka wa chuo kikuu. Mle kutakuwa kuna watenda kazi, kuna mameneja, kuna kila kitu kwa sababu ule mchanganyiko unakuwa ni wa kutosha. Kwa hiyo niombe, Serikali ibadilishe mtindo, ili tupate *impact* ya hizi fedha za kukopesha vijana wetu. La sivyo, tutakuwa tunapoteza ajira bado hakuna na fedha zinaendelea kupotea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia niende nikawasemee Madiwani. Kwanza niishukuru Serikali kwa kuwashamisha tu mahali pa kulipiwa fedha, kutoka kwenye halmashauri kwenda kwenye Mfuko Mkuu. Kilichopatikana hapo ni uhakika na kutokucheleweshwa na heshima, lakini kiukweli tatizo hasa kubwa bado, hawa Madiwani

wanafanya kazi kubwa sana. Ule usumbufu wa matatizo ya wananchi tunaopata sisi Wabunge kwenye Jimbo zima wao wanaupata pia, kwenye kata zao. Kwa hivyo, ni watu ambao wanahitaji wawe na angalau na *peace of mind*, hii posho ya Sh.300,000 ni ndogo mno. Ningombwa kwa sababu, Serikali Kuu imebeba mzigo wa hii shilingi 300,000, tuwaagize halmashauri, sasa Wakurugenzi wawaongeze hata shilingi 100,000 kama posho ya madaraka ili ukichanganya angalau ziwe shilingi 400,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walikuwa wanaweza kuwalipa shilingi 300,000, sasa kama Serikali kuu imechukua, tukisema wawaongezee hata shilingi 100,000 utakuwa ni mzigo mwepesi. Angalau bado hazitoshi, lakini angalau itapunguza hata kidogo. Kwa hiyo, tutakuwa tumewapa heshima ya kuwalipa kwenye Mfuko Mkuu lakini pia, tuwaongezee chochote, kiweze kupatikana. Hawa ni wenzetu na *wana-deal* na wananchi na wote tunaelewa, jinsi wananchi wanavyotegemea Wabunge, wanavyotegemea Madiwani na sisi ndio watu wa kutatua shida zao. Wenzetu hawa na wenyewe wakiwa katika hali nzuri na hata huko majimboni patatulia. Tukiwa huku na sisi tunapumua. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla naomba hili liangaliwe, ni jambo linawezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kwa Madiwani sasa hivi, hii posho ya vikao, vikao vyenyewe vya Baraza la Madiwani ni kama vinne tu kwa mwaka, lakini sasa kuna hii posho hii ya kikao inaitwa nyingine sijui ya kujikimu, Diwani inabidi akae kwenye kikao sijui mpaka kwenye saa 9.00 au saa 10.00 ndio alipwe ile fedha. La sivyo, siku nyingine anaambiwa wewe wa karibu, itabidi ulipwe nusu usipate *night*. Fedha yenyewe ndogo, bado ametoka huko Mheshimiwa Diwani amesafiri mwingine na pikipiki, anafika inabidi akae kwenye kikao walazimishe mpaka ifike saa 9.00 ndio ile fedha iingie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali, hii shilingi 100,000 ukiachana na ile Sh.40,000/= ya *sitting*, hii shilingi

100,000 iitwe tu fedha ya kikao, ili hawa walipaji waweze kulipa hii fedha bila matatizo, lakini unapoita *nights* jui mpaka ifike saa 9.00, sijui mpaka saa ngapi kunakuwa kuna *double standard*, kuna vurugu kila wakati. Madiwani wangu wa Mkalama juzi wamekaa hapa wengine wamelipwa *night*, wengine hawajalipwa, mchanganyiko na naamini hii iko katika maeneo yote ya Wabunge wote. Hebu tuiite tu shilingi 100,000 ya kikao, shilingi 40,000 *sitting*, vikao vyenyewe mara nne kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na dada yetu Waziri wa TAMISEMI, wapeleke waraka. Waraka wamepeleka ule, wenzangu wa TAKUKURU kwa sababu, wenyewe wanafanya kazi yao, wakaingia nao pale kama hamjafika saa 9.00, fedha haitoki. Sasa inasababisha hata mambo mengine hayapiti, wanakwamisha tu Madiwani ili angalau ifike saa 9.00. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu niombe hii fedha ya shilingi 100,000 na shilingi 40,000 ya *sitting* utoke waraka, ni fedha ya kikao, ielewewe katika maeneo yote...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, wakati huo Mheshimiwa Saashisha Mafuwe na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, wanajiandaa.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote napenda kuipongeza Wizara ya Fedha kwa bajeti hii ambayo imekuwa ni rafiki kwa maendeleo ya nchi hii, bajeti ambayo ieonesha dhima nzima ya Mheshimiwa Rais ambayo siku ile alikuwa ana hotubia

hana. Pia, bajeti hii imelenga hasa katika suala kamilifu la kutekeleza kuboresha mazingira ya kibiashara. Tumeona kwamba katika bajeti hii kodi nyingi zimefutwa. Mama amejitahidi kwa kiasi kikubwa kuonesha nchi hii ni sehemu salama kwa kwa ajili ya watu kuja kuwekeza. Viel vile bajeti hii imeweza kurahisishwa ulipaji wa kodi. Kwa hiyo, napenda kuipongeza sana Awamu ya Sita kwa kazi kubwa inayofanya na Wizara ya Fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchangia kwenye kitu kingine na kutilia mkazo katika Halmashauri zetu. Halmashauri zetu zinafanya kazi vizuri, lakini kuna nyingine ambazo makusanyo yake ni madogo. Sijui Wizara ya Fedha imejipangaje katika kwa Halmashauri ambazo vipato vyake ni vidogo, makusanyo hayo ambayo yanakwenda kuathiri zile asilimia 10 ambazo tumewaaahidi wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikichukulia mfano kama Halmashauri ya Shinyanga Vijijiini, Ushetu, kwa kweli kwa mwaka hawa watu mapato yao ni madogo. Unakuta makusanyo kwa mwaka ni shilingi milioni 137, watu walilokopeshwa unakuta ni vikundi 10. Sasa fikiria kwa haraka haraka, ni vikundi vingapi vitakuwa vimefikiwa ili kuwezesha hawa vijana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnaona huku kwenye Serikali ajira bado ni ngumu kupatikana na pia huku tumeweka katika llani yetu kwamba tutawezesha vijana, wanawake na walemvu kupata mikopo. Ukija huku nako bado mapato yanayopatikana ni machache kiasi kwamba hawawezi kukopesheka na hawawezi kupata fedha za kutosha kwa ajili ya kutenga ile asilimia 10, vijana wote na wanawake wote wakaweza kufikiwa. Licha ya hivyo, bado fedha nyingi zipo mikononi. Sijaelewa kwa jinsi gani Wizara ya Fedha itaweka msisitizo katika hizi Halmashauri zile fedha ziweze kurudishwa ili zikawasaidie wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nakuja kwenye suala lingine la *TRA*. Mmeona kabisa tulivyokuwa kwenye semina imeonesha kwamba walipa kodi ni 5% katika nchi hii ambayo

ina watu milioni 60 ambapo walipa kodi *almost* milioni tatu. Utafikiria kwamba kwa kiasi kikubwa wananchi hawalipi kodi. Vilevile Serikali haijaweka mazingira rafiki kwa ajili ya watu kulipa kodi. Unaweza kufikiria kwamba kwa kipindi kilichopita kuna watu walikuwa wanabambikiziwa kodi kitu ambacho kinaweza kikawafanya wale wafanyabiashara wakaingia hofu na kutufanya tupoteze mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali itaweza kujipanga na ituoneshe kwamba katika bajeti hii imejipangaje kwa wale watu ambaao walibambikiziwa kodi? Maana kuna watu walibambikiziwa kodi mpaka wamefunga maofisi. Je, haioni kwamba ni wakati sahihi sasa hivi ya kukaa tena na wale wafanyabiashara na kuzitoa zile kodi ambazo zilikuwa siyo sahihi? Wali-*double charge* kwenye VAT katika mapato yao ya kipindi cha nyuma. Naona Wizara ya Fedha ingekuja na mkakati mpya wa kupitia wale wafanyabiashara ambaao walikuwa wamefanyiwa huo mchezo. Nami nakuomba Mheshimiwa Waziri, nakuona hapo, mimi nitakuufuata kwa sababu nami ni muhanga wa suala hili, kwa sababu hiyo inamfanya mtu akwepe kabisa kulipa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, kuna hizi *Agency Notice* zinawekwa. Unakuta kuna wafanyabiashara wanafanya kazi *on credit bases; thirty days, sixty days of invoice*. Sasa unakujakuta hata yale malipo hajayapata, ameshatumiwa *Agency Notice* kwa mteja wake. Ile inamfanya huyu mlipaji kodi ashindwe kulipa hii kodi. Kwa hiyo, naomba kabisa Wizara ya Fedha ifanye mkakati wa kufanya hii Taasisi ya *TRA*, walipa kodi walipe kwa hiari, siyo kwa kutumiwa *task force*, siyo walipe kodi kwa kulazimishwa. Mtu afike mahali aone ni hiari kuichangia Serikali yake, siyo Serikali itumie nguvu kum-*force* mtu alipe kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kuchangia sehemu nyingine ambayo ni ya mwisho, nayo ni sekta ya afya. Nimeona kwenye sekta ya afya mmetenga bajeti kwa ajili ya kumaliza maboma 8,000. Hiki ni kitu muhimu sana. Haipendezi tena tunaporudi kule kwa wananchi wetu

tuwakute tena wanalamika na wameweza kupandisha mabomba maboma hayo 8,000 mpaka kufika hapo. Serikali inabidi sasa mkafanye mpango kama mlivyofanya kwenye barabara na pia kujenga shule. Mheshimiwa Ummy umefanya jambo moja zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nakuomba sana, wanawake wakasaidiwe kupata sehemu salama za kujifungua kwa sababu haya maboma 8,000 yanaweza kufanya ushawishi mkubwa sana kwenye Sekta ya afya, itafanya mapinduzi makubwa sana kwa sababu kuna yale maeneo ambayo kweli yana mwendo mrefu mtu kukuta Kituo cha Afya. Nina imani kwamba hili nalo likitekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sisi Wilaya ya Kishapu ina maboma 20 ambayo hayajakamilika. Ukienda Wilaya ya Shinyanga Vijijiini, ina maboma 39 ambayo hajakamilika. Sasa utaona kwa jinsi gani kukiwa na mama mjamzito atapata shida, amba ni wanawake wenzangu; kuna Watoto na wazee ambao wanaenda mwendo mrefu kupata huduma ya afya. Nina imani hilo nalo linaenda kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, hayo ndiyo yangu, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwita Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hotuba hii nzuri na kihistoria. Nianze kwa kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo ameanza vizuri; kwanza kuendeleza miradi mikubwa ile ambayo awamu iliyotangulia ilikuwa imeanza nayo. Nampongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote wa kwa bajeti nzuri

waliyotuletea, iliyochukua mawazo ya Waheshimiwa Wabunge. Niliwahi kusimama hapa nikauliza, ni kwa asilimia ngapi michango ya Wabunge inachukuliwa kufanya matengenezo kwenye mipango ya Serikali? Sasa naomba nipongeze sana kwamba wamechukua kwa asilimia kubwa mawazo yetu. Kwa msingi huo, nianze kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Siyo tu kwamba naunga mkono hoja, ni wa sababu nimeona kwenye bajeti hii Jimbo letu la Hai tumetengewa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya viwanda tumetengewa shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya kufufua kiwanda cha *Machine Tools*. Siyo hivyo tu, tumepelekewa fedha kwenye elimu na barabara. Wananchi wa Jimbo la Hai wameniambia niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuunga mkono, narudia tena kumpongeza Mheshimiwa Rais. Niseme, akina mama popote mlipo Tanzania, huu ni wakati wenu wa kuiga mfano mzuri na kila mmoja ambaye anafanya shughuli yake afanye kwa ujasiri kwamba akina mama wanaweza. Siyo kwa sababu mimi ni kinara wa kutetea haki za akina mama na watoto, siyo hivyo tu ni kwa sababu ya kazi nzuri wanayoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme jambo, kwa msingi huo huo tu, tunaye baba yetu ambaye ndiye anamshauri Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan kufanya haya. Naye nampongeza sana. Kwa heshima hiyo, namwomba Waziri; sasa hivi tunajua kwenye mikopo ile ya Halmashauri asilimia zile 10, akina mama wanapata, walemavu wanapata na vijana. Kwa msingi huo huo kwa sababu kuna baba anayemshauri vizuri mama, hebu akina baba na wenyewe waingizwe kwenye kundi hilo wapate mikopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nishauri kuhusu bajeti hii. tumeambiwa hapa tunapanga kuongeza pato la Taifa mpaka kufikia kwenye asilimia sita na ushee.

Mimi naona hii ni ndogo kwa sababu kama tutafuata maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuwekeza kwenye kilimo, tunaweza kuvuka lengo hili. Hakuna namna yoyote tunaweza kuepuka kuinua uchumi wetu tukaacha kilimo nyuma, haiwezekani. Tunaambiwa asilimia 25 ya pato la Taifa linatokana na kilimo, lakini ukienda kuangalia ni wangapi wanashughulika na biashara hii? Utakuta ni eneo dogo sana. Naomba tuamue kwa dhati bajeti hii, fedha ambazo zimetengwa kwenye eneo la kilimo zije kwa asilimia 100 zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo zuri tumeliona hapa. Wananchi wa Hai wamekuwa wakinipigia simu, vipi kuhusu tozo iliyowekwa kwenye umwagiliaji? Ile asilimia tano? Niseme, naiunga mkono Serikali tozo hii iwepo kwa sababu imehamishwa kule kwenye ushirika, imeletwa kwenye umwagiliaji. Kazi yake ni nini? Ni kuhakikisha wanajenga miundombinu, lakini fedha hii asilimia tano itafanya matengenezo. Jambo ambalo sasa hivi Serikali inajenga ile mifereji na zile skimu, lakini fedha za matengenezo haipo. Kwa hiyo, hii tozo iliyowekwa hapa itaenda kufanya kazi hiyo. Naomba ibaki hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nimezungumza vizuri na Naibu Waziri, Mheshimiwa Bashe akanihakikishia ile Mamlaka ya Umwagiliaji inaenda kuanzishwa, itafanya kazi hii. Kwa hiyo, naomba sana kwenye eneo la kilimo tuwekeze nguvu ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wetu wengi wapo huko kwenye majimbo yetu. Hawa tukiwawezesha kwa hatua ya kwanza; kwanza kufanya utafiti. Tuweke fedha nydingi kwenye utafiti, naona zimebekwa, zije kama zilivyo. Wakiwepwa fursa ya kufanya utafiti, tukahakikisha tunayo mbegu yetu, tuna watalaam wa kutosha kwenye kilimo, tuna maji ya kutosha, eneo linalobaki ni kuhakikisha tuna viwanda vya kuongeza thamani ya mazao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna namna tunaweza kuinua uchumi huu kama hatuongezi uzalishaji. Hili

linawezekana. Mheshimiwa Mama Samia Suluhu leo akisimama akitamka kwamba jamani Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa mlioko huo, kila Mkuu wa Wilaya kwenye wilaya yake tunampa malengo ya kukusanya, kwamba kila msimu tunataka tani 300,000 za mahindi, hizi lazima zipatikane; za maharagwe kadhaa, baada ya kufanya utafiti, kila mmoja tunampa lengo lake. Watatuletea hizi tani. Wale ambao tunaona wanasuasua, basi zile kadi ambazo Mheshimiwa Waziri ulishauri, itumike moja. Waki pigwa wawili, watatu *speed* itaongezeka kuhakikisha wananchi wanafanya kazi ya kulima kuongeza uzalishaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo hiki kitatusaidia mno. Pale Jimbo la Hai Mheshimiwa Waziri, mimi nakuhakikishia, nyie tuleteeni fedha. Fedha yenu itarudi. Tuleteeni fedha za kujenga skimu za kutosha zile tano za kimkakati, tuleteeni viwanda vya kuongeza thamani ya mazao sisi tulime, tuuze. Siyo tu kwa kuza, kwa sababu pale Jimbo la Hai tumewe ka mkakati, tuna soko hili naomba sana, sijalionia kwenye bajeti lakini uone namna ya kutafuta fedha popote lile soko la kwa Sadala lijengwe. Lile soko letu lina tofauti kidogo na masoko mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile soko tume-*design* litauza yale mazao ya wananchi lakini kutakuwa na viwanda vidogo vidogo vya kuongeza thamani ya mazao haya. Kama ni nyanya, inaondoka pale ikiwa imepakiwa vizuri kwenda nje ya Nchi. Kwa hiyo, hapa tutatengeneza fedha. Lile soko ni la kwako kabisa, ni la kimkakati, ukilitungia vizuri litatusaidia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze kuhusu kazi nzuri ambayo Serikali imefanya kwenye maslahi ya watumishi. Bajeti hii tunayojadili hapa wanaokwenda kutekeleza ni watumishi. Nawashukuruni sana kwa kupokea mawazo yetu. Waheshimiwa Madiwani mmewajali, Maafisa Tarafa; na nakumbuka mimi ni Afisa Tarafa Mstaafu, kwa hiyo, nililisema kwenye Kamati na mmeliweka hapa. Endeleeni

kuboresha maslahi ya watumishi kwa sababu hawa ndio ambao wanatufanya kazi nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine hapo kwa watumishi, kuna jambo ambalo halijakaa vizuri kuhusu *promotion*. Fedha zimeshatengwa hapa, mara nyingi sana humu ndani tunasimama tunasema shida ipo kwa Maafisa Utumishi. Naomba leo tuweke kumbukumbu sawa. Maafisa Utumishi wakimaliza kazi yao, kuna watu wanaitwa *Approver* wako pale Utumishi. Hawa lazima tutenge fedha za kutosha ili wawepo wa kutosha na *speed* ya kupandisha watu madaraja iongezeke na watumishi wetu waweze kufanya kazi kwa bidii na kwa *speed* ambayo inategemewa. Tukifanya hivyo, itatusaidia sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona mikakati ambayo mmeweka ya kuongeza mapato ni nzuri sana. Awamu iliyopita kwenye tathmini tumeweza kukusanya kwa asilimia 86 mpaka kufikia Aprili, lakini mikakati tuliyoweka hasa pale bandarini, mmeefanya jambo zuri sana la kutumia mifumo kukusanya. Ninaomba kuweka tahadhari kubwa ya kuangalia, hii mifumo tuhakikishe inafanya kazi masaa 24. Kwa sababu kosa linalotupata hapa ni kwamba wakati ambapo mifumo hii inasimama, ndiyo wakati tunapopigwa. Kwa hiyo, kama tumeamua kutumia hii mifumo, basi tuhakikishe mifumo hii inakuwa kamili kweli kweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sito tu pale bandarini, huku kwenye mahospitali yetu kuna makusanyo kwa kutumia mifumo wa *GoT-HOMIS*, ndiyo hali ipo hivyo hivyo, pale mifumo unapo-shake, tunaposema tunataka kwenda *paperless*, hawajajiandaa. Umeme unazimika, ndiyo fursa inatumika kutupiga. Kwa hiyo, naomba sana watu mitandao na mifumo wahakikishe tunakuwa na mifumo ambayo imesimama vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongezee hapa jambo. Niliwahi kusema humu ndani, hivi kuna shida gani kama tukiamua kuwa na mipango yetu ambayo itapangwa kwa kipindi cha miaka 50 na miaka 100? Nimejaribu kufanya

tafiti, nimezungumza na maprofesa wa uchumi wananiambia jambo hili linawezekana. Ifike mahali Mheshimiwa Waziri, alika Maprofesa, alika wataalam wa uchumi, alika nchi nyingine duniani ambazo zimeweza kuwa na mipango hii. Hii itatusaidia sana kuwa na mipango ambayo itatekelezwa kwa kipindi cha muda mrefu lakini kuondoa utashi wa Kiongozi kufanya yale anayoyapenda yeye. Hii mipango itatusaidia kusukuma. Tunakuwa na mambo haya, tunasema hizi ni *interest* za Tanzania, ziwekwe hapa, tutatekeleza kwa kipindi cha miaka 50. Aje mweusi, aje mweupe atatekeleza, atalazimika kwa misingi ya sheria kuweza kutekeleza hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Hongereni sana kwa bajeti nzuri inayogusa maisha ya wananchi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Saasisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai. Tunashukuru kwa mchango wako mzuri. (*Makofi*)

Sasa namwita Mheshimiwa Pricus Jacob Tarimo, wakati huo huo Mheshimiwa Venant Daud Protas na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma wanajandaa.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia hutuba hii ya Wizara yetu ya Fedha. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, wote ni ndugu zangu. Nawashukuru Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji wote kwa shughuli hii nzito. Naipongeza Serikali kwa kweli, tayari tumeshaona mwanga mbele, tunawashukuru sana, tunawapongeza. Kazi ya muhimili huu huwa ni kuwakumbiza nyie, lakini ninyi wenywewe mmetuonesha njia na tutawaunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na miradi ya kimkakati. Nimeshawahi kuteta na Mheshimiwa Waziri. Kule Moshi katika miradi ile ya kimkakati, Halmashauri yetu tulipewa Stendi ya Kimataifa pale. Stendi ile imeshameza

shilingi bilioni saba za Serikali Kuu. Serikali ya Halmashauri imetengeneza barabara za kuzunguka na kutokea eneo lile na kuzamisha pale zaidi ya shilingi milioni 500, lakini miradi ile imesimama, mwenzangu juzi alitoa mpaka takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali tumeishaianza kazi, ile fedha tusiifukie. Nasi tuna maombi mawili; tunaomba aidha Serikali itusaidie tumalizie, mradi ule una kama shilingi bilioni 17 au 19, lakini kama Serikali itaona imebanwa, itusaidie kusaini kibali cha kuturuhusu sisi Halmashauri iweze kukopa. *Original plan* ndiyo hiyo. Kwa hiyo, tunaomba hayo yaweze kufanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na madhara ya UVIKO-19. Dunia nzima hayo madhara yameonekana na kumekuwa na utaratibu wa kutoa kitu kinaitwa *stimulus* na kiukweli katika nchi yetu, kila mahali wamedhurika, lakini zaidi kwenye utalii na usafirishaji na hoteli. Sasa naiomba Serikali, kama itashindwa kutoa *stimulus* kwa maana ya kupeleka fedha, maana naona baada ya ile Kamati alioiunda mama yetu, naona Benki ya Dunia kama siyo *IMF* wamesema watatoa dola milioni 400 na kitu. Sijajua mpango wa Serikali na hizo fedha ni vipi kama tutapewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *stimulus* we katika maeneo haya. Kama Serikali itashindwa kabisa kutusaidia fedha, basi itusaidie hata kwenye kuhuisha zile leseni bila ghamama, lakini ikishindikana hiyo, basi kuna zile *charges* ambazo zimepanda ndugu yangu wa Arusha jana alilalamika sana, basi zibaki zile za mwaka jana na zile nyingine mpya hasa zile za ardhi zisimamishwe kabisa mpaka hao watu watakapo-recover kwa sababu kuna muda mrefu sana mpaka wa-recover. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande huo huo, wafanyabiashara wengi hasa wakubwa na wa kati wanafanya biashara kwa mikopo na wengi wamekopa kwenye mabenki ya ndani. Sasa hatua za mwanzo, zile benki zimepunguza au zimeondoa *principal*, zimebakiza *interest*. Sasa kwa kawaida unajua, ile *interest* ikiendelea kuchajiwaa

ni umesogeza tu na mzigo mbele unazidi kuwa mkubwa. Naomba Benki Kuu kama inaweza, kama njia ya *stimulus*, iondoe *interest* pamoja na *principal* mpaka angalau mwakani mwezi wa Sita au mwezi wa Kumi na Mbili, hali hii ikishatulia, basi wale wafanyabishara waweze kurudi kwenye biashara zao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina lingine la kuishauri Serikali, hasa kwenye sera za uwekezaji. Hatujawa na sera za wazi kabisa ambazo zinaweza kum-*support* mtu anayetaka kuja kuwekeza hapa. Kwa majorida ya Kimataifa yanasema, katika nchi ambazo hazitabiriki ni pamoja na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitatoa mifano michache tu, moja ya sera ambazo zinaweza kuvutia watu ni pamoja na *interest* za benki na watu wengi wamezelongelea. Hiyo ni *positive*, lakini *negative* ya sera ambazo zinatukosti ni kipindi ambacho Serikali ilizivamia biashara zenye leseni, tena leseni kutoka za mamlaka tofauti tofauti, viwanda na biashara na BoT zile *bureau de change* na kuzifunga bila ya maelezo mengi na kunyang'anya zile hela. Sasa hizo sera za namna hiyo ndio zinasababisha tunakuwa nchi ambayo haivutii sana wawekezaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kuishauri Serikali. Na sehemu nyengine ambazo tunaweza kusaidia kwenye sera za uwekezaji ni kwenye kodi, sheria zetu za kodi zinamatatizo kidogo. Nilishawahi kutoa mfano hapa kuhusiana na kodi kwenye ile *Tanzania Revenue Appeals Act*. Ile sura ya saba inatoa haki ya *ku-appeal*, sura ya 16 wanaku-*limit* kwamba mambo haya na haya na haya, yaani kwamba ni kama tu ukiwa umeonewa na Kamishna na una-*appeal* kwenye *board*. Lakini hiyo pia inaenda kinyume pia na *Tanzania Appeal Act* sura ya 53 ambayo inatoa haki ya *appeal* kwa lolote. Sasa hizi ni moja ya vitu vichache ambavyo vinasababisha tuwe hatuna mazingira mazuri ya kuwekeza, kwa hiyo, ningeshauri hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali, imetenga fedha nyingi kwa ajili ya kuangalia na kupandisha

madaraja kwa watumishi wa Serikali, lakini kwenye hili peke yake halitoshi, lazima tukumbeke wale watumishi ule mshahara wao ni *factor* ya kodi ya Serikali kwa sababu inakatwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeshauri, pamoja na hizo juhudzi zilizofanyika zote kipo kitu amabacho inabidi tukiangalie, watanzania wote walioajiriwa na waliojiajiri tunajenga nyumba zetu kwa *cash* hii ni gharama kubwa ukija kuangalia, yaani unapokuta barabarani mtu anaendesha mkokotenzi amepakia geti ni mjasiriamali anapambana, ninajua Serikali imeweka mazingira mazuri kupita Watumishi *Housing* lakini bado. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie uwezekano wa kuitumia benki kama *TIB*, maana sitaki kurudi nyuma tuiufufue Tanzania *Housing Bank*, lakini *TIB* iwe na mfumo wa kuhakikisha tunawezesha wafanyakazi kujenga nyumba zao, iwe ni *security* kwao na ni *security* pia kwenye maeneo yetu ya kazi. Haya mambo ya uwajibikaji na rushwa hayataweza kuisha kwa sababu kila mtu atataka kujenga na nyumba leo imeonekana ni moja ya vitu vitakavyo msaidia kama *retirement*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo mazuri ningeshauri hilo, pia kwa Polisi wamekuwa wakihoji, Polisi peke yao ndio ambao hasa kuanzia Inspector, wanatakiwa kustaafu wakiwa na miaka 55, Magereza na *Immigration* wao wanaenda mpaka miaka 60, sasa wanasema kunini, na wao ni watu wanaofanya mazoezi wako fiti, wanaomba liangaliwe hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la viwanja vya michezo, mimi nina mambo mawili pale, kwanza niipongeze Serikali pamoja na masuala ya nyasi bandia, kwa mfano wa viwanja vya Halmashauri, tunavitumia kama chanzo cha mapato na mambo mengine mengi yanafanyika pale, vikiwekwa viwanja vya nyasi kidogo vinakuwa haviwezi kutumika kwa michezo mengine na vitu vyengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ile mliyosema kwa majiji sita haya majiji ndio yenyе viwanja. Hebu tuangalieni halmashauri zenye maeneo kama Moshi, tunauwanja wa majengo, Waziri Mkuu alifika pale akasema atatusaidia, sisi tuko tayari tumeshachimba maji na tumshafanya *grading* na tumeshaanza juhudzi za kuweka majani na tumetenda milioni 300, hebu njooni muanze na sisi, na sisi wenyewe tutakuwa jiji karibuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana eneo la madini wamefanya vizuri sana, na nimeona kuondoa VAT kwenye kwenye yale madini ambayo yatakuja kubusti viwanda vyetu vile yya uchenjuaji ni hatua nzuri sana. Niongezee tu Serikali iunde kamati ya kwenda kushawishi sasa zile nchi ambazo hayo madini yapo ili yeje yachenjuliwe hapa, ili kubust *export* yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazo ambalo nimeona litatusaidia kuhakikisha vile viwanda vya uchenjuaji vinafanya kazi vizuri. Mwisho kabisa nilishaongelea tena suala la kuangalia kuunganisha bandari, reli na yale maeneo ya muhimu ya kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona mda umeisha nashkuru sana naunga mkoni hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ninamwita Mheshimiwa Venant Daud Protas.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi hii kuwa mionganoni mwa watu ambao watachangia bajeti kuu ya Serikali, iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha. Kwanza nianze kuipongeza Serikali, nimpongeze Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo wameifanya, kwa muda mchache ameleta bajeti yenyе matumaini makubwa kwa wananchi, kwa sababu wananchi wetu walikuwa na kero kubwa sana juu ya maendeleo yao sasa hata kodi zetu ambazo tunakwenda kuzilipa zitaleta tija kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachi walitaka hatima ya maboma ambayo wanayaanzisha yaweze kukamilika, pia kwenye bajeti hii imejipambanua wazi kabisa kuwa maboma yetu yanakwenda kukamilika na watu wataanza kupata hudama, hongereni sana Serikali. (*makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watanzania wanahitaji kulipa kodi, lakini waione kodi yao inafanya kazi. Leo tumeleta mpango wa kufuta baadhi ya kodi na kuongeza baadhi ya kodi, lakini inahitajika elimu iongezeke zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tunaishukuru Serikali kwa kupunguza tozo au faini ambayo ilikuwa ilikuwa inatozwa kwa watu wa boda boda wanashukuru sana, na tumekuwa tunapokea simu hasa mimi kutoka jimboni wanasema mmetupunguzia faini lakini mmeongeza fedha kwenye mafuta, uklangalia uhalsia fedha kwenye mafuta hajaongezwa ni utaratibu wa kawaida ambao ulikuwa tangu zamani, na wananchi wanaona mafuta yamepanda zaidi kwa kipindi hiki kifupi, basi wanajua fedha sasa Serikali imepunguza faini imekuongeza kodi kwenye mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali, tunapokuwa tunafanya hivi vitu basi tuongeze na wingo wakutoa elimu. Kwa mfano watu wa mamlaka inayohusika na upandishaji wa bei za mafuta, basi wanapokuja kupandisha au kushusha wanatakiwa watoe taarifa kwa wananchi ili waweze kujua tumeongeza kwa sababu gani au tumpunguza kwa sababu gani, ili tuweze kupunguza haya mengine ambayo wananchi wanashindwa kuelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze kwa kupunguza faini kutoka shilingi 30,000 mapaka shilingi 10,000, mmewasaidia sana boda boda na Mheshimwia Waziri ulisema hapa unahitaji boda boda wasiwe ndio chanzo cha mapato ya Serikali, unahitaji Polisi wafanye kuwaelimisha boda boda ili wesiwe mionganoni mwa wavunja Sherika. Nikupongeze sana, maana Polisi walibadilika kuwa mungu watu. Sisi kwetu kule boda boda ndio *ambulance* ya

kupeleka wangojwa, ili mgonjwa aweze kukaa vizuri kwenye pikipiki lazima ubebe na mtu mwengine wa kumshikilia, ukikutana na Polisi anawaza tu yeye kutoza faini, sasa ilibadilika kuwa ni kero kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa kuipunguza hii imetusaidia sana. Na mimi niiombe na nimuombe Waziri wa Mambo ya Ndani, Polisi wetu watusaidie sana kuwapa watu elimu. Unajua kuna mazingira mengine hayahitaji hata faini, unaweza kukutana na mtu amevunja taa kwa bahati mbaya wakati huo huo umekutana naye anakwambia gari lako bovu, ukumwambia nimevunja sasa hivi anakwambia hamna lete nikupige faini, wakati ilikuwa ni kitendo cha kuweza tu kumwambia, changamoto hii nenda kairekebishe, hilo litatusaidia sana na litatupunguzia malalamiko kwa watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwa Madiwani, niipongeze Serikali kwa kulibeba jukumu hili ambalo ilikuwa ni kero kwa madiwani wetu. Madiwani kero kubwa ilikuwa ni kupata ile stahiki yao kwa wakati, ilo sasa Serikali mtakwenda kulifanya kwa utumilifu, kwa uhakika mkubwa kwa sababu Serikali ikipanga jambo lake na likiingizwa kwenye bajeti basi haliwezi kukwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madiwani walikuwa hawahitaji kulipwa ile pesa kwa wakati tu, bali walikuwa wanaomba waongezewe posho, kiukweli sisi wenyewe tunajua tukirudi kule majimboni tunakuwa sisi wenyewe ni madiwani, wananchi wote wakiwa na matatizo basi kabla hawaajaenda sehemu yoyote basi wanamkimbilia Diwani, wanamkimbilia Mbunge, wanamkimbilia sehemu zengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali. Kwa kuwa tulimebeba hili jukumu basi tuone namna gani ya kuwasaidi hawa Madiwani. Na pia tumepata changamoto nyengine, kuna muongozo ulikuja kule kuna Madiwani wamekuwa wakikatwa posho zao, leo tunakwenda kulalamika kumkata Diwani shilingi laki moja na ishirini eti kwa sababu anakaa Makao Makuu ya Halmashauri, hiyo imeleta changamoto

sana, majukumu ya Diwani ni yale yale, ni sawa sawa na mbunge anaetoka Kongwa, anaetoka Bahi ukamkata usimlipe *per diem*, hiyo sasa siyo sawa kwa sababu wale wadiwani wanaposafiri kwenda pale wamebeba dhamana ya wananchi wao kutoka kwenye kata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Serikali, tuwaangalie madiwani wanamajukumu makubwa sana kama tulivyo sisi, tunapokwenda kuwapunguzia posho zao. Kwanza posho ni ndogo, unaenda kupigana nae kwa shilingi laki moja, anafanya kazi kubwa, anapitisha mapato yote ambayo yanatekelezwa katika halmashauri. Kwa hiyo, niombe Serikali itusaidie hili nalo litoe muongozo, kwa sababu wamekuwa wakigombana na wakurugenzi, wakurugenzi wanaosimamia sheria, inakuwa imeleta tabu. Kwa hiyo, niiombe Serikali iweze kutusaidia katika hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lengine kuhusu tozo za simu. Serikali imekuja na nia njema sana katika kukusanya kodi kwa kuititia simu zetu, niiombe Serikali. tumekuwa tukifanya miamala tunalipa mara mbili mbili, leo ukitaka kutuma milioni moja kwanza wewe unaetuma unakatwa shilingi elfu nne, yaani unatuma kwa mtu akapate hela wanakatwa elfu nne, akifika tena yule mtu kabla hajaitoa anakatwa elfu nane. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali kama mnataka kuitoza vizuri hii kodi, wale makampuni tunahitaji waendelee *ku-survival* katika ufanyaji wa biashara, basi kama inakatwa ile ya kutumia iwe ya Serikali, ile nytingine iwe ndio iwe makato ya kampuni na wale wengine watoa huduma, kwa sababu unakuta milioni kuituma na kitoa zaidi ya shilingi 12,000. Serikali inaenda kupata haifiki hata elfu tatu, sasa zingine zote zinapotelea hewani hewani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Serikali. Tumekuja na mpango mzuri lakini kuna sehemu kuna *linkage* hasa hii mitandao ya simu, imekuwa kero kwa sababu wanaongeza tu yaani makato yamekuwa yanaongewa kiaina aina tu hata haieleweki. Leo wanakwambia kufikia

5599 ikifika tu na kamili ile wanaongeza tena 300 zaidi ya ile kilichokuwa. Kwa hiyo, niiombe Serikali iangalie hili suala, na ndio maana tulikuja hapa kwenye uchangiaji wa sekta ya mawasiliano, tulisema tuimarishe shuirika letu la *TTCL*, haya yote hayatokuwepo, lile shirika ni la Serikali asilimia mia moja, haya makampuni mengine yapo kibiashara na hii tukiimarisha shirika letu linaweza kutusaidia hata tozo zenyewe za makato yakapungua, watu wakapiga simu vizuri, Serikali ikapata fedha zake vizuri bila ya hata kulalamika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Serikali, kwa kuwa imekuja na mpango huu mzuri tuangalie na sehemu zinapo-*link* haya matatizo yanayotokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, nakushkuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Venant Daud Protas kwa mchango mzuri. Ninamwita Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma. Wakati huo Mheshimiwa Salum Mohammed Shaafi pamoja na Mheshimiwa Anatropia Theonest wanajiandaa.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushkuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhi Hassan, Kwa kazi nzuri sana anayoifanya. Pili nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na wataalamu wote wa fedha kwa kazi nzuri wanayoifanya, hongereni sana. Kwa kweli nimeipita hii bajeti yote nzima nimeiona kweli bajeti nzuri sana, ambayo kila mmoja anaisifia na kila mmoja hata kule nje wanaisifia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hapa niweze kuongelea kuhusu mambo ya kilimo. Kila mmoja anaelewa kuwa kilimo inaajiri asilimia 65 ya wananchi, pia kilimo 100%

ya chakula kinachotolewa na kinachozalishwa kinaliwa na sisi wananchi kwa 100% wanazalisha hichi chakula. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo licha ya hayo yote imetengewa bajeti kidogo, kwa mwaka huu wa bajeti ya 2021/2022 imetengewa kiasi cha fedha ya bilioni 294.2 ambayo hii ni kidogo sana. Kilimo inamambo mengi, kilimo ina umwagiliaji, kilimo ina mambo ya mbegu, kilimo ina utafiti, kilimo ina kupima udongo, kilimo ina mambo kweli mengi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mambo yote ambayo yametengwa kwenye bajeti hii iweze kutolewa, kusema kuwa ni ndogo kwa upande wa nchi zinazoendelea, kufuatana na Azimio la Malabo ilitupendekeza kuwa, bajeti ya kilimo iwe angalau asilima kumi ya bajeti nzima ya Taifa. Sisi bajeti yetu iko chini ya asilima moja, unaweza ukalona kuwa kweli tunakazana na kilimo hatuwezi kuwalauku Mawaziri ni sisi wenywewe, nilikuwa nashauri kuwa Mheshimiwa Waziri unanisikia kuwa safari ijayo mwaka wa bajeti unakuja 2022/2023, hii bajeti ya kilimo kama kweli tunataka kupunguza umasikini iweze kuongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuongelea ni kuhusu mikopo ya elimu ya juu, mikopo ya elimu ya juu wote tunafahamu, wote wabunge tunajua, kuwa Watoto wa vyuo vikuu huwa wanatusumbua huko vijijini na mjini, wengi wamedahiliwa na wamepata vyuo na hawakuweza kupata mikopo, kwa hiyo bado wapo vijijini wako huko. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naipongeza Serikali kwa kuweza kutenga bilioni 500, ambayo itaweza kwenda kwenye mikopo ya elimu ya juu. Saa nashauri hawa wanafunzi ambao walidahiliwa na wakapata vyuo na wakakosa mikopo, wawe wa kwanza kuwapa kipaombole kuona je, kama watawe kuomba wanaweza wakamit requirement ya kupata hii mikopo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lengine ambalo naongelea ni ukusanyaji wa mapato, nashukuru kwa kupunguza ushuru wa mashine za kukusanya mapato. Jambo muhimu ambayo inabidi tuangalie na wote tunajua watu hawadai risiti na watu hawatoi risiti, na ukienda anaweza akakwambia nikupe risiti feki, na wewe kama unataka vitu vya rahsi unakubali pia nilikuwa naomba tutoe elimu kuhusu ukusanyaji wa mapato ndio tunaweza kuendeleza nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongelea kuhusu lishe, miaka mingi lishe huko nyuma ilikuwa ni kwa Wizara ya Kilimo, na kwenye Wizara ya Kilimo ilikuwa inaenda vizuri sana, kiasi kinamama walikuwa wanafundishwa vizuri hata kupika uji, wanafundishwa lishe vizuri sana, hakuna mtu aliyeongelea kuhusu lishe humu ndani. Jambo ninalo omba bajeti ya lishe iweze kuangaliwa, na ikiwezekana lishe itolewe huko kwenye Wizara ya Afya iweze kwenda kwenye Wizara ya Kilimo kama zamani, au iweze kwenda TAMISEMI ambavyo inaweza ikaratibu vizuri mambo ya lishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu imetolewa asilimia tatu ya bajeti tu ambayo haitoshi, kwa hiyo, nilikuwa nashauri kuwa iweze kutengewa zaidi ya asilimia tatu...

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Lugangira taafira.

## TAARIFA

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru, ningependa kummpa taarifa mzuingumzaji kwamba, Chama cha Mapinduzi tayari kimeona umuhimu wa suala la lishe kuwa kwenye sekta ya kilimo, na kwenye ilani yake ile lengo la kushusha hali ya udumavu kutoka asilimia 32 mpaka asilimia 24 imewekwa chini ya sekta ya kilimo. Kwa hiyo, kilichobaki ni Serikali na yenyeewe kufanya kama hivyo, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ishengoma unaipokea hiyo taarifa.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naipokea kwa mikono miwili, halafu kuongezea hapo hata wale maafisa lishe wanafundiswa na vyuo vya kilimo, kuanzia kwenye cheti mpaka kwenye Chuo Kikuu cha Sokoine wanafundisha hadi lishe. Inakuwaje inaratibiwa na afya?

Naomba sana afya iungane kama idara nyengine lakini mratibu mkubwa aweze kuwa ni kilimo. Pia tuweze kutunga sera na sheria ambayo inaweza kuwabana watu wa halmashauri, kutenga hiyo elfu moja kwa kila mtoto chini ya miaka mitano kusudi iweze kuratibu mambo ya lishe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu *TARURA*, watu wengi wameongelea lakini na mimi nashukuru kwa shilingi milioni mia tano ambazo zinatolewa kila Jimbo kusudi kutengeneza barabara zetu za *TARURA*. Ukweli barabara ni mbaya zinaweza zikaenda vizuri, halafu napongeza kuwa kwa ushuru ambao utakuwa ni shilingi 100 kwa kila lita ya *diesel* na kila lita ya petroli ambazo hizi fedha zitakwenda kutengeneza barabara za *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye mafuta. Naishukuru na kuipongeza Serikali kwa kupunguza ushuru na kwa kuongeza ushuru wa mafuta yanayotoka nje ili kusudi kulinda viwanda na kulima mbegu zinazozalisha mafuta ndani ya nchi yetu. Hii hapa nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye juzi kule Singida alizindua kampeni ya kilimo cha alizeti na kilimo cha alizeti ndugu zangu Wabunge mnapotoka hapa nendeni kwenye Majimbo yenu, hamasisheni kilimo cha alizeti ili kusudi tuweze kuondokana na kuagiza mafuta kutoka nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pia kwa kuhamasisha kilimo cha michikichi ambayo na yenye inazalisha mafuta ya mawese.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba kuongelea ni kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Vifaa vya umwagiliaji ukweli ni ghali hasa ukileta kwenye mipira ile ya matone ya maji. Mheshimiwa Waziri, angalia kama kuna VAT kwenye vifaa hivi vya umwagiliaji VAT iweze kutolewa kusudi tuweze kumwagilia kwa urahisi mambo yetu ya mboga mboga. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hapa napongeza kwa kutoa ushuru hasa *cold chain* au chumba cha baridi. Hii itasaidia kwa ukulima wa bustani, wakulima wa bustani kwa sababu wataweza kulima mbogamboga na matunda na wanawea wakaweka kwenye chumba cha ubaridi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni nzuri sana kwa sababu inaendeleza kilimo cha bustani ambacho ni rahisi sana kwa kumtoa mkulima kwenye umaskini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninaunga hoja na hayo yote niliyoyaongea naomba yachukuliwe. Ahsante sana. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Dkt. Ishengoma kwa mchango mzuri.

Tunao wageni ambao wengine ni wanamichezo kwa hiyo ni vizuri tuwatambulisho halafu waweze kuendelea. Tuna wageni 26 ambao ni Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (*TASWA*) wanaokuja kucheza na *Bunge Sports Club* siku ya Jumamosi. Pia, wamekuja kujifunza jinsi *Bunge* linavyoendesha shughuli zake wakiongozwa na Ndugu Majuto Omary. Karibuni sana. (*Makof!*)

Tunao wageni 313 kutoka vilabu vya *jogging* vya Mikoa mbalimbali nchini ambao wamekuja kujifunza namna *Bunge* linavyoendesha shughuli zake wakiongozwa na viongozi wa *Dodoma Fitness Club*. Ahsanteni sana kwa kuhamasisha *jogging* nchi nzima na hivyo kusaidia kupunguza magonjwa yasiyoambukiza. (*Makof!*)

Pia tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Atupele Mwakibete (Mbunge) ambaao ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo Ndugu Anyeswisye Njobeloo pamoja na ndugu Chamboga Mwakatika. Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao wageni 16 wa Mheshimiwa Aida Khenani (Mbunge) kutoka kanisa la mtakatifu Bakhita la Nkasi Kaskazini Mkoani Rukwa wakiongozwa na Ndugu Imelda Mzaliwa. Ahsante. (*Makofii*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambaao ni ndugu zake kutoka Jijini Dodoma Ndugu Yahaya Hussein na Ndugu Fatma Ahmed. Ahsante. (*Makofii*)

Tunao wageni 14 wa Mheshimiwa Simon Songe ambaao ni wanafunzi wa Chuo cha Uuguzi na Ukunga Shirati Mkoani Mara wakiongozwa na Ndugu Michael Adui. Ahsanteni sana, karibuni wageni wetu. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Nilimtaja Mheshimiwa Anatropia Theonest, atafuatiwa na Mheshimiwa Salum Mohammed Shaafi. (*Makofii*)

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru lakini pia nishukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya bajeti. Ninachangia hotuba hii ikiwa inaingia kwenye rekodi. Hotuba ambayo kwa mara ya kwanza tunapata Rais Mwanamke. Nadhani imekuwa ni ndoto ya zaidi ya miaka 50 kwa Taifa letu, kwa wanawake lakini kwa watu wote wanaoamini katika mabadiliko na kwa watu wanaoamini katika 50/50. Kwa hiyo, ninamshukuru Mungu leo ninakuwa sehemu ya historia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mama yetu, ameanza vizuri. Ameanza vizuri nadhani ni kazi yetu Wabunge kumshauri, ni kazi yetu Wabunge kumtia moyo, na ni kazi yetu kumuelekeza pale tukiona mambo hayaendi vizuri. Hiyo, niseme ni moja kati ya *commitment* yangu mimi pia kama Mwanamke kuelekeza, kutumia mamlaka niliyopewa ya Katiba kama Mbunge kuishauri na kuielekeza Serikali na mimi

niseme nitamshauri Mama yangu kama alivyosema kwa staha kuhakikisha anafanya vizuri. Akifanya vizuri, wanawake tutafanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kwa kusema malengo tuliyokuwa nayo ya kuwa na Tanzania ya Uchumi wa Kati, malengo tuliyokuwa nayo ya mipango ya miaka mitano, miaka 25 yanaweza yasifikasiwe kwa sababu uchumi wetu hauendi kwa namna ambavyo tulikuwa tunatarajia. Uchumi ambaao ulitarajija katika mwaka 2021 uwe unaenda kwa asilimia Nane mpaka asilimia kumi leo unaenda kwa asilimia Nne (4). Kwa hiyo, matumaini yetu hayawezi kufika kama watu wanavyotaraji. Kama matumaini hayawezi kufika yale ni lazima tuyabadilishe au tuone namna gani tunaweza kubadilika ili tuendane na mabadiliko yaliyoko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na mpango wa kuhakikisha kipato cha Mtanzania kinafikia *at least by* 2021 dola 1,500 ambayo ni shilingi 3,469 lakini *in reality* ni kwamba haiwezekani. Leo kipato cha kawaida ni sawa na shilingi 2,557 ambayo ni dola 1,080. Kwa hiyo malengo hayawezi kufikiwa na sababu zimeelezwa ni kutokana na ugonjwa wa corona. Lakini, nitarudi kusema hatuwezi kuwa na mabadiliko ya msingi kama idadi kubwa ambayo tunapaswa kuwaleta *on board* ambaao ni wakulima hawajafikiwa kwa kiwango kikubwa. Wote tutakubaliana idadi kubwa ya Watanzania ni wakulima ambaao ni zaidi ya asilimia 64 lakini ni kiwango gani tumewekeza kwenye kilimo? Ukiwasikiliza Wabunge wanaongea mara nyangi na tuseme maeneo mengi wengi tunatokea kwenye mashamba, kwenye vijiji, watalalamikia namna ambavyo kilimo kinaendeshwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya maeneo ambayo tunafanya vizuri kutegemea na asili zetu kwamba tuna mvua za kutosha na kadhalika lakini bado hatufanyi vizuri. Kuna watu wanalalamikia mahindi kukosa soko. Kuna watu wanalalamikia kahawa kukosa soko. Kuna watu wanalalamikia alizeti na mambo mengine. Ni kwa kiwango gani sasa wakati ambapo tunaona uchumi kwa *trend* ya Dunia hauendi vizuri tumejiandaa katika *ku-exhaust* kwenye

masoko ili *at least* mazao ya kiuchumi ambayo tuliyonayo, mazao ya kilimo yaweze kufanya vizuri kwenye soko. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa msemaji mzuri sana katika zao la kahawa na ninaamini kama nchi tukiwekeza vizuri kwenye zao la kahawa tutaweza kufanya vizuri kama kilimo kwenye Pato la Taifa. Leo mchango wa kilimo kwenye Pato la Taifa ni asilimia 27, *it's just a peanuts*. Ukiwa na watu wa zaidi ya asilimia 64 wanachangia asilimia 27 kwenye Pato la Taifa *then you have failed*. Nadhani bado tuna kazi yak uji-stretch ili tuweze kuongeza mapato. Kama tunataka kufanya *transformation* ya uchumi wa Kati na Watanzania wa-*feel/kwamba* wako kwenye uchumi wa kati tunapaswa kuwekeza kwa watu ambao ni wengi zaidi. Takwimu zinaonesha *export* ya kilimo ni asilimia 24. Narudia, *t's just a peanut*, tunahitaji kufanya vizuri na tuna nafasi ya kufanya vizuri tukiamua kufanya hivyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshaongelea suala la kahawa na niseme leo ninavyoongea leo nimeongea na wakulima wa Kagera wa Kahawa, Uganda kilo ya kahawa ni zaidi ya shilingi 2,500 lakini waliouza kahawa Tanzania kule Kagera wanauza shilingi 1,200, siyo sawa! Ni lazima tuangalie ni namna gani tunaweza ku-*trade* katika hii biashara ya kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uganda wanauza wapi ambapo sisi hatupaoni? Nchi nyingine zinauzwa wapi? Lakini siyo hiyo tu, nimeeleza humu ndani nikasema Uhganda na udogo wa Uganda wanalahisha tani zaidi ya 200,000 kwa mwaka lakini sisi tunazalisha tani 65,000 siyo sahihi! Wakulima wa kahawa wamekuwa *frustrated* wameacha kulima kahawa kwa sababu ya soko ambalo haliko *promising*. Lengo hapa ninalolisemea ni namna gani wale waliokuwa wengi wanaweza kuchangia kwenye Pato la Taifa na tutaona mabadiliko *drastically* kimsingi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa mahindi wanalamika, wakulima wa maharage wanalamika, tunakosea wapi kama Taifa? Kwa hiyo, mimi niiombe Serikali

i-exhaust namna ambavyo tunaweza kutumia masoko ya nje, i-exhaust namna ambavyo tunaweza ku-penetrat kwenye soko na nimeeleza mara moja hapa Bungeni, nikasema Duniani au Afrika Kahawa ya Tanzania inashika namba mbili kwa ubora. Kwa hiyo, bado tuna nafasi ya ku-compete kwa sababu tunazalisha kahawa iliyokuwa bora. Wakulima ambaao nimeongelea ni zaidi ya asilimia 64 wanapata changamoto gani? Wakulima hawakopesheki kwa sababu ya aina ya kilimo wanachokifanya na hawakopesheki kwa sababu kilimo chenyewe kiko unpredictable, mtu amekopa fedha zake amewekeza kwenye kilimo lakini huwezi kupata soko huwezi kuuza, kwa hiyo automatic uta-default. Kwa hiyo ninafikiria ni lazima tuangalie namna gani tutaweza kuwasaidia wakulima waweze kukopesheka. Mmeanzisha Benki ya Kilimo lakini ni kwa kiwango gani Benki ya Kilimo imewezeshwa? Ni kwa kiwango gani Benki ya Kilimo inaweza kumkopesha hata mkulima wa kawaida? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija wale mnaowasema asilimia 64 ya wakulima lakini unakuta wanaokopesheka ni less than three percent kwa hiyo hatuwezi hata ku-achieve tunachokitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu ya mikopo na nieleze, mfano kama Kagera, bado tuna fursa ya kufanya biashara. Nimekuwa nikiongelea masoko ya kibashara ya Mrongo na Nkwenda. Hilo ni eneo jingine ambalo budget na niseme bajeti mwanzoni nilifikiria kwamba inategemea walipa kodi asilimia 20 lakini *real/tyni* walipa kodi asilimia tano. *Imagine* walipa kodi asilimia tano kutegemeza nchi, ina maana the 95 percent wanaangalia asilimia tano, it's not fair and the vice versa. Kama tuki-convert the 95 percent ambaao ni wakulima na wengine tukawawezesha kufanya biashara kuwapa mikopo wakaweza kuzalisha wakalipa kodi hata mzigo wa wale five percent hautakuwa mkubwa. Kwa hiyo, masoko ya kitega uchumi ambayo yapo Murongo na Nkwenda yakiboreshwa tutaweza kufanya biashara vizuri na watu wa Uganda. Hiyo ni concern nyingine naileta ambayo sasa tunapaswa kuangalia katika sekta ya kilimo ili tuweze kuongeza tija. Hilo ni suala la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wale wakulima wa kawaida tunawasaidiaje waondoke kwenye umaskini? Nimeona takwimu, kuanzia 2016 takwimu za Serikali zinaonesha umaskini ulikuwa asilimia 28 *point something* na mliahidi kwamba *by 2021* tutakuwa tumefika asilimia 16 lakini *reality* mabadiliko yamekuwa ni asilimia mbili tu, yaani umaskini umepungua kwa asilimia mbili tu. Hatuwezi kupata mabadiliko tunayoyategemea. Tunawezaje kusaidia kupunguza umaskini, mmeefanya kazi ya kupeleka umeme vijiji kuititia *REA*, ni kitu kizuri na ni namna moja ya *ku-stimulate* uchumi wa vijiji kwa sababu umeme kama umeme bado unakuwa na *impact* kwa sababu hata wafanyabiashara watafanya mambo mengine ya kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka njiulize, ni kwa kiwango gani tumejiaanda miradi ya leo iwe *sustainable*. Leo tumepeleka umeme kwa kasi vijiji lakini huo umeme utakuwa na *cost implication* baadaye. Kuna nguzo zitadondoka, kuna mafuriko na vitu vingine. Kwa hiyo, tunavyopeleka umeme ni lazima tuangalie *to what extent* huo umeme utaendelea kuwepo pale vijiji. Lakini tukijiaanda na *emergency* zinazotokana na umeme, kunaweza kuwepo na radi zikaharibu miundombinu, lakini kunaweza kuwepo na shoti kutegemea na mazingira ya vijiji. Ni kwa kiwango gani tumejiaanda miradi hii ya umeme hairudi nyuma? Hilo ni swali la pili ambalo kama tutaweza ku-*sustain* tutakuwa tumeweza kupunguza umaskini katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho Mheshimiwa Waziri umeongea kwenye bajeti yako unaufutaje msamaha kwenye vifaa vyta umeme vinavyotumia umeme wa jua? Leo ukienda kwenye vijiji miradi ya *REA* ambayo inaelezwa imeenda vijiji zaidi ya 8,000 wakienda kwenye kijiji kimoja wanafunga umeme katika nyumba 20 tu na nyumba zilizosalia zinatumia umeme wa nishati ya jua - sola. Unavyoenda kuongeza kodi maana yake unawarudisha wale watu kutumia vibatari. Unawarudisha wale watu kununua mafuta ya taa. Unawarudisha kwenye maisha yale ambayo wakati tunazaliwa tuliyaona yako hivyo. Mimi ninashauri

Serikali, hebu tafuteni vyanzo vingine vya mapato hiki cha misamaha ya kodi msikiondoe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namuita Mheshimiwa Salum Mohammed Shaafi wakati huo Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib, Mheshimiwa Amour Khamis Amour na Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris wanajiandaa.

**MHE. SALUM MOHAMMED SHAIFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia bajeti hii muhimu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue fursa hii nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuweza kukutana hapa na kujadili jambo muhimu ambalo ndiyo msingi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niishukuri Wizara kwa namna walivyoweza kutuwasilishia bajeti hii nasi kuweza kuichambua na kujadili na kuitolea maoni yetu na kama hatuna la kushauri basi tumepata nafasi hiyo. Mimi leo sina mengi ya kusema lakini naomba niseme machache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza binafsi nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa kipekee kabisa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Sulu Hassan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenye macho haambiwi tazama. Sote tunaona namna Mama yetu anavyoongoza Taifa hili na niseme Mheshimiwa Rais wetu Mwenyezi Mungu kamjaalia kipaji cha hekima na busara. Namuomba Mwenyezi Mungu ampe afya njema, ampe umri mrefu wa kuzidi kutuongoza Watanzania kusimamia haki na kujali utu wa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii kuna mambo mengi yamezungumzwa. Mimi leo naomba nitoe rai na

kuishauri Serikali. Mara baada ya kupitisha bajeti hii siku ikifika tunaenda kuwapa fedha Wizara au mamlaka husika. Naomba niishauri Serikali iende ikazisimamie fedha hizi katika yale maeneo yote ambayo yamepangangiwa kupewa hizi fedha. Wawasimamie ili tuondokane na ile kadhia ya watu kuhujumu uchumi, watu kuiba fedha za Serikali, watu kuiba fedha za walipakodi wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya tukifanya haya tutakuwa tumedumisha nidhamu Serikalini lakini tutakapoziacha tu hizi fedha ziende ile nidhamu ya fedha Serikalini itakuwa haipo, lakini mara baada ya kuwapa fedha hizi naishauri Serikali sasa iwakumbushe watumishi hawa wajibu na majukumu yao katika kazi zao. Jeshi la Polisi likumbushwe wajibu wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mengi yanatokezea wananchi wanalamika juu ya kadhia ya baadhi ya Wanajeshi la Polisi, yapo mitaani! Leo tukiangalia tu Taifa letu linapita katika hali ya usalama na amani ya kutosha kabisa ni kwa sababu wanasiasa ndiyo walioleta amani hii. Ni wanasiasa ndiyo walioleta amani hii katika nchi hii. Nani anasema haya? Mengi yalipita, kule kwangu Zanzibar mengi yalifanyika kupitia Jeshi hili la Polisi pamoja na vikosi vya SMZ, watu walipigwa, watu walinyanyaswa, walipigwa risasi, yale makovu Wazanzibari wameyafunika, wanaamini sasa tumekuwa kitu kimoja tunasonga mbele, tunesahau yaliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yaliyopita yasije yakarejea tena. Ili yasijirudie lazima Serikali muende mkawakumbushe sasa hawa watumishi wajibu wao katika utekelezaji wa kazi zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niwasemee wenzetu wastaifu. Hawa wastaifu wamelitumikia Taifa kwa muda mrefu sana, wamejitoa kwa hali na mali, wamejitoa kwa kila hali kuhakikisha kwamba wanatumikia nchi yao. Naomba bajeti hii iwe ni sababu ya kwenda kumaliza kero za wastaifu hawa, isiwe kila mwaka wa bajeti katika Bunge

hili tunawajadili hawa wastaafu kwamba bado posho zao hawajzipata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wastaafu wengi na wana miaka mingi bado hawajapata posho zao. Naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kijana mwenzangu, muonekano wa sura yako inaonekana ni msikivu na mtiifu, nenda kalisimamie hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tu niendelee kusema Serikali hebu nendeni *TFF*. Wizara husika nendeni *TFF* mkaangalie kuna nini *TFF*? Kuna shida gani *TFF*? Manung'uniko haya yaweze kuisha, niishauri Serikali nendeni huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kikubwa tu na cha mwisho ambacho naomba nikiseme ni kudumisha Muungano wetu na ninachukia sana wanapojojiteke baadhi ya watu kuunyoshea vidole upande wa pili kwamba hawaupendi Muungano, sio kweli, wao wanaonyosha ndio ambao hawaupendi Muungano. Hakuna aliyesema hataki Muungano. Sote tunataka Muungano, lakini tunataka Muungano wa haki na usawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya nikiamini hapa Wabunge wengi wamesimama, wamesema na ninaishukuru Serikali kwamba wameingiza hizo shilingi milioni 500 ili kuweza kusaidia maendeleo katika majimbo yao, lakini leo, jana na juzi, baadhi ya Wabunge wanahoji fedha hizi je, na kule Zanzibar zitapatikana? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa muono wangu mimi naamini sisi sote ni Watanzania. Kama tutabaguliwa Wazanzibari katika fedha hizi sasa hapa ndio tutaanza kuhoji kuhusu suala la Muungano, kwa sababu Serikali yangu ni sikivu, Serikali yangu nawaelewa ni wasikivu, sidhani kwamba ikifika Jumatatu jambo hili litajadiliwa tena humu kwa sababu mimi nafahamu Serikali yangu ni sikivu na jambo hili italisikia na Wazanzibari nao ni sehemu ya Muungano. Hapa Bara Wazanzibari wapo wanafanya biashara, wanalipa kodi, sasa leo iweje eti Wazanzibari wasipewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siamini; mimi siamini, mimi naamini tutapewa, zitatumika Zanzibar na ile fedha ambayo injenga shule ya sekondari kila kata na Zanzibar kila jimbo tutajengewa shule ya sekondari. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nimalizie kwa kusema naishukuru Serikali. Waziri Mheshimiwa Mwigulu unanisikia sana rafiki yangu, shilingi milioni 500 hii ni haki ya Watanzania, hatuna Mbunge wa Bara wala hatuna Mbunge wa Zanzibar; ni Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sote tuliomo humu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nashukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kwa kuweza kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niweze kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kaka yangu Mwigulu Nchemba, lakini nimpongeze sana Naibu Waziri wa Fedha, kaka yangu Mheshimiwa *Engineer* Hamad Masauni, lakini niweze kumpongeza sana Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na timu yake yote kwa pamoja kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kutuletea bajeti ambayo inaenda kumgusa mwananchi mwenye kipato cha chini moja kwa moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Tanzania, Mheshimiwa Mama yangu Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa aliyofanya ndani ya miezi mitatu, hakika natuheshimisha wanawake wote wa kitanzania, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kuangalia suala la Liganga na Mchuchuma kwa sababu ndani ya Bunge hili limeongelewa kwa muda mrefu toka sijawa Mbunge mpaka nimekuwa

Mbunge, hiki ni kipindi changu cha pili, awamu zote mbili kwa sasa ye ye ndio *at least* ameamua kuliingilia suala hili. Na suala hili litakapofanikiwa kufufua Liganga na Mchuchuma vijana wataweza kupata ajira kwa wingi, lakini tutaweza kununua pembejeo kwa wakulima wetu, lakini pia tutaweza kutengeneza barabara zetu kwa pesa zetu za ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kumpongeza pia Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kufuta tozo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu asilimia sita, lakini kama mimi ni Mbunge wa vijana kama sijawasemea vijana wenzangu nitakuwa sijawatendea haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kiukweli juzi alituonesha upendo wa dhati Jijini Mwanza siku ya tarehe 16 na alituahidi mambo mazuri ambayo kwa sisi kama vijana atatupatia. Niseme ahsante sana, lakini naomba niyanukuu mambo machache kwa ufupi ambayo ametuahidi kama vijana; kuwajengea mazingira mazuri ya kufanya biashara, kuwapa ujuzi, mazingira bora ya kufanya kazi ya uzalishaji, lakini kubwa zaidi kusubiria mkeka wa ma-DC, ma-DAS na Wakurugenzi ambao wengi wao watakuwa wanatokana na vijana. Nimuhidi Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kuwa sisi vijana tuko nyuma yake na hatutamuangusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa kumaliza tatizo la kuunganishwa kiuchumi kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa kutunga sheria ya kuondoa kodi kulipia mara mbili. Nishukuru sana Serikali yangu, lakini bado kumekuwa na changamoto kuhusu wafanyabiashara wa Kizanzibari wamekuwa wakilalamika kwa muda mrefu sasa kuhusu mfumo wa kodi uliokuwepo sasa hivi. Niiombe Wizara ya Fedha iweze kuangalia upya kuhusu mfumo wetu wa kodi kwa wafanyabiashara wetu wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala Wabunge wengi hasa kutoka Zanzibar, wameliongelea na mimi nikiwa mmojawapo, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha hebu

tukae tuangalie Zanzibar na Tanzania Bara ni nchi moja, lakini sijui kwa nini kumekuwa na ukiritimba katikati ambao haueleweki kati ya wafanyabiashara wetu kutoka Zanzibar kuwa-*charged* tena mara mbili kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania Zanzibar tayari wameanza kufanya marekebisho ya Sheria ya VAT kwa kuondoa tozo mpaka kufikia asilimia sifuri, lakini kwa bidhaa za viwandani peke yake. Hii haijaidia kwa mfanyabiashara ambaye hana bidhaa za viwandani na niishauri Serikali hata ikiwezekana kuiruhusu sukari yetu ya Zanzibar kuuzwa Tanzania Bara kama itawapendeza Serikali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Mheshimiwa Waziri wa Fedha amependekeza kodi mpya inayotokana na simu pamoja na mafuta ili kuweza kupata fedha kwa miradi ya kimaendeleo. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri wa Fedha wa Tanzania Bara, je, amewasiliana na Waziri wa Fedha Tanzania Zanzibar kuhusu mgawanyo wa miamala na matumizi? Kwa sababu kwa upande wa Zanzibar bado sijaona kitu chochote kuhusu kodi hii inayotokana na mafuta na simu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa mwaka tutakusanya zaidi ya shilingi triliuni mbili kwa tozo zinazotokana na sim una mafuta. Hizi fedha ni nyngi sana, ili Watanzania wawe na imani ya kuchangia fedha hii ni lazima Wizara iweke wazi jinsi ya kutumia fedha hii, lakini nataka niishauri Serikali kwanza kuwa na uwazi jinsi miradi itakayotumika kwa fedha za tozo hii ya mafuta na simu, lakini pia kuwe na ukaguzi wa CAG tena wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Mheshimiwa Waziri, hivi karibuni tumemuona Mheshimiwa Waziri Mkuu akitumbua wafanyakazi wa Wizara ya Fedha, aliwasimamisha kazi kutokana na matumizi mabaya ya fedha ambayo yalikuwa yanatumika bila ya mpangilio maalum. Ndio maana nimesema hizi fedha ambazo zitakusanywa zikaguliwe na CAG tena ikiwezekana mara kwa mara. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu upungufu wa wafanyakazi wa *TRA*. Nimemsikia Mheshimkiwa Waziri kuwa tutaweza kuajiri wafanyakazi 40, lakini niseme jamani wafanyakazi 40 ni wachache sana. Mimi binafsi nilikuwa katika Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira nimeona jinsi watu wa *TRA* wanavyolalamika kuhusu wafanyakazi wao, tunapoteza sana mapato ya Serikali kwa sababu watumishi ni kidogo. Niiombe Serikali iweze kutoa kibali cha kuajiri wafanyakazi wengine wapya tena wenye weledi na uelewa wa jinsi ya kuweza kukusanya mapato. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2020/2021 tumekusanya shilingi triliion 14.52 sawa na asilimia 82 tu; bado malengo ya Serikali hatujafikia. Kwa hiyo, niiombe Serikali iweze kuajiri watumishi wa *TRA* ili kuweza kupata fedha zaidi kwa sababu sasa hivi wamekuwa hata wananchi zamani ilikuwa kuna elimu mwananchi aweze kudai risiti ya kielektroniki, lakini sasa hivi mwananchi mfanyabiashara hawatoi risiti za kielektroniki na tunaweza kupoteza kodi kubwa ya Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie, nimeona matairi ya pikipiki tayari yameongezewa *charge ya VAT*, lakini sasa hapa Tanzania tunakiwanda chetu cha *General Tyre* ambacho tulikuwa tunazalisha matairi. Niiombe Serikali kama kweli tuko tayari kuwasaidia vijana na ajira tungeangalia suala la kufufua kiwanda hiki cha *General Tyre* kilichopo Arusha. Toka mimi sio Mbunge kiwanda hiki cha *General Tyre* kinapigwa makelele. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekunde 30; naomba nipongeze sana Wizara hii na niseme inaenda kufufua uchumi wa mwananchi, vyuma vinakazuka chini ya Rais mwanamke Mama Samia Suluhu Hassan. Naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib kwa mchango mzuri. Sasa ninamuita Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataallah* kwa kuwa ye ye ndiye aliyetuumba kuwa wanadamu na hakutuumba Wanyama, kwa hiyo, ametuumba wanadamu tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu *Alhamdullilah.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana na kumshukuru sana Rais wa nchi hii ya Tanzania, mama yetu Samia Suluhu Hassan, mwanamke wa kwanza Afrika Mashariki kuwa Rais na ninampongeza pamoja na wote wafuasi wake wanaomsaidia Dkt. Mpango, Makamu wa Rais na Mawaziri wote na Naibu Mawaziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza kwa pongezi za kipekee kwa kutuletea hotuba hii au bajeti hii ambayo ni nzuri sana. Bajeti hii imewachukua mpaka wale ambaa ni wachache kwenye Bunge hili wakadiriki kusema kwamba ile yaani inawasababisha kupata raha mpaka wanasema kwamba inawatekenyatekenya, inawafinyafinya, kwa kweli mimi nilijisikia faraja sana. Namuomba Mwenyezi Mungu ampe nguvu sana Mama yetu Mama Samia, nguvu za kipekee za katuongoza kule tunakokuhitaji na amuepushe kabisa na maadui na mahasidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ndio itaenda kutekeleza llani yetu ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025 na ninaimani kwamba mwaka 2025 Bunge hili linaweza likawa la Chama cha Mapinduzi peke yake kwa sababu *reference* mama yetu Mama Samia alivyokuwa Makamu wa Rais wakashauriana vizuri na Mheshimiwa Magufuli ambaye ni Hayati sasa hivi, walitekeleza ilani ipasavyo wakatufanya hata sisi Wabunge kutoka Pemba wa CCM tukawepo hapa. Leo tunajivunia sana kuwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kuwemo ndani ya Bunge hili kutoka Pemba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni tabia tu kama alivyokuwa akilalamikia hapa Mbunge kutoka upinzani hapo, alikuwa

akilalamikia kwamba, hakuna haki, lakini inavyoonekana kwamba haki lazima wapate wao ndio tatizo lao pia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza pia mama kwa kutupatia zile shilingi milioni 500 kwa kila Jimbo, namshukuru sana na watu wasiwe na wasiwasi jamani, hizi ziliviyotajwa zilitajwa kwamba kila jimbo. Unapofanya wasiwasi kwamba sisi wapemba, sijui sisi Wazanzibari hatutapewa, maana yake una wasiwasi kwamba kule hakuna majimbo. Hizi fedha zitatoka jamani, msiwe na wasiwasi, haya maneno kasema mama, mna wasiwasi na mama? (*Makofii*)

**MBUNGE FULANI:** Hatuna.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sasa kuhusiana na hii nyongeza ya shilingi 100 katika mafuta, lakini pia katika mitandao ya simu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbarouk unaweza ukatafuta pengine *microphone* ya jirani.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Na kutaendelea kuwa na utulivu katika Ukumbi wa Bunge, ukitaka kuzungumza utaomba idhini. Ahsante, endelea mchangiaji.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Shilingi 100 hizi mimi najiuliza hivi zitakuwa na *alarm?* Yaani zitakuwa na sauti zitakapoingizwa? Kiasi kwamba ikifika kwa mfano saa 6:00 ya usiku itamueleza Waziri wetu Mheshimiwa Miwgulu Nchemba kwamba leo kumeingia kiasi fulani cha fedha? Kwa sababu mwenzangu aliyeppita kuchangia sasa hivi alikuwa anasema kwamba Waziri Mkuu alitumbua watu kwenye Wizara ya Fedha kwa sababu ya matumizi mabaya, sijui wanajilipa shilingi milioni 400 kwa siku na hizi zitakuwa na usalama gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamuomba Waziri ajue kwamba yeze ndio kaka yetu katika familia hii ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini katika Chama cha Mapinduzi na ajue kwamba yeze ndio kaka mwenye fedha anatakiwa awe makini sana na mfuatiliaji sana na msimamizi sana wa hizi fedha. Kwa sababu wananchi wetu wako tayari kuchangia tena kwa heshima ya Serikali hii tukufu, lakini kwa heshima ya Mama Samia Suluhu Hassan. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo na sisi Wabunge tunalipa baraka jambo hili ila tunaomba kile kilichokusudiwa kitendeke. Na si eneo hili tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuna eneo lingine ungeweza kulitumia vizuri lingeweza kutusaidia sana hata katika tiketi za mabasi makubwa yale yanayokwenda mikoani ingetusaidia kama utafanya kifungu kidogo, kwenye tiketi za usafiri wa ndege, kwenye tiketi za boti; unaweza kuongeza hapo, lakini je, kweli itakwenda kuwanufaisha Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hicho ndio kitu cha kuzingatia. Kadri tutakavyokuwa tukilichangia jambo hili tuhakikishe kwamba, kile kichokusudiwa ndio kinaenda kutendeka kwa sababu nina imani kwamba Tanzania hii tukishatandika barabara zote hizi kodi zitapunguzwa pia, wananchi wetu watapungua kwenye kulipia kodi. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali ifikirie namna gani ya kuzisimamia kodi hizi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi hizi zikikusanywa vizuri tutaondokana kabisa na madeni nje kwa sababu tunavyokopa au kadri tunavyopewa misaada hata wanafunzi wa darasa la sita najua *plus minus is equal to minus*, kwa maana sisi kadri tunavyokuwa tunapokea misaada ndio tunatoa yaani tunapoteza. Ni *logic* ndogo ambayo inatumiwa na wanafunzi wa darasa la saba, darasa la tisa, darasa la kumi, kwa hiyo ninaamini Mheshimiwa Waziri anajua hii hajaisahau kwamba *plus minus is equal to minus* kwa kadri tunavyokuwa tunapokea misaada ndio tunavyokuwa tunatoa. Kwa hiyo namwombwa sana Waziri wetu, kiongozi wetu, kaka yetu katika familia hii, atuongoze

katika jambo la kujitegemea na si kuendelea sana kukopa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niishauri Serikali kwamba katika mikakati iliyowekwa kuhakikisha bajeti hii inapatikana inayosimamiwa sikuona, inawezekana imo lakini sikuona kwamba kunahitajika kuwe na usalama wa nchi. Nilimsikia Mheshimiwa Noah hapa akieleza orodha ya matukio ya ujambazi ambayo yapo, ambayo yangeweza kufanya wafanyabiashara kama walikuwa wanafanya biashara mpaka saa sita ya usiku, sasa wataogopa kwa sababu kuna ujambazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili naomba sana Serikali ilifanyie utafiti ni muhimu sana kufanya utafiti. (*Makof*)

*(Hapa kengele lilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nashukuru kwa kunipa nafasi. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, wakati huo Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi anajandaa.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu, lakini kubwa zaidi nikupongeze wewe binafsi kwa kazi kubwa ambayo unaifanya hapo katika kiti katika kutuongoza. Hakika wewe ni mtoto wa nyoka na kama sio wa nyoka basi ni mjukuu wa nyoka, maana yake damu ya ukoo wa Adam Sapi Mkwawa inaonekana inafanya kazi yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wetu wa Fedha

ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Naibu wake na timu nzima ya wataalam kwa kutuletea bajeti ambayo kiuuhakika imebeba dhana ya maelekezo ya mama yetu Samia Suluhu Hassan, lakini kubwa zaidi llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi katika kumsaidia Mtanzania kusonga mbele kutoka hapa tulipo na kwenda mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni uthibitisho tosha umeona kila Mbunge aliyesimama anapongeza, lakini sio Mbunge kwa sababu sisi Wabunge tulichangia katika bajeti katika Wizara mbalimbali, tukieleza zile kero za wananchi wetu na wananchi wetu huko nje vile vile wamepata faraja kubwa na wanaendelea kuipongeza Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hongera sana kwa mdogo wangu Mheshimiwa Mwigulu na timu yake kwa kufuata maelekezo ya mama, lakini kwa kufuata maelekezo ya llani ya Uchaguzi ya Chama Chetu Cha Mapinduzi. Ni imani yangu kabisa tukienda hivi ndani ya miaka mitano hii tutafanya mambo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mama yetu Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jemedari mkuu katika nchi yetu, kwa kazi kubwa ambayo amelfanya ndani ya kipindi cha siku 100 anakoelekea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika mama huyu ni Mama shujaa, mama shupavu ambaye kwa uhakika niwaambie Watanzania na naendelea kusema mama huyu anatosha, anatosha na atatuvusha salama Watanzania kule tunapotarajia kwenda. Hata hivyo, nitumie nafasi hii...

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa tu ndugu mzungumzaji kwamba mama huyu sio tu anatosha bali anatosha na chenji inabaki. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kalogeris endelea na kuchangia.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nimeipokea taarifa. Ni kweli chenji bado inabaki na itatosha kufanya mambo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii vile vile kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndugu yetu kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ndani na nje ya Bunge katika kutekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, lakini kuwa kama kiungo kati ya Mama Baraza la Mawaziri lakini na sisi Wabunge katika kuona kipi kifanyike. Ni imani yangu kwamba hata haya yaliyokuja kuna majumuisho makubwa ambayo yamefanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii vile vile kutoa pongeza za dhati kwa Serikali yangu. Hakika kauli yake Mama, anatusalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sisi tunatakiwa kujibu kazi iendelee, kazi inaendelea tena kwa kasi kubwa zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona tumepata milioni 500 kila Jimbo kwa ajili ya *TARURA*. Wabunge tumepiga kelele kwamba barabara mbaya, barabara mbovu, lakini mama ametusikia ametupa. Pia nimpongeze ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu na naamini hayo ni maelekezo ya Mama kwa kubuni vyanzo mbalimbali ambavyo tunaamini kwa mwaka huu wa fedha tutakwenda kutengeneza bilioni 300 ambayo inaonekana inakwenda *TARURA*. Ombi langu kwa Serikali, Halmashauri, Majiji na Manispaa tumetengwa katika fedha za Mfuko wa Barabara, wamependelewa wenzetu wa Majiji na Manispaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu fedha hizi katika mgao wake uende kwa majimbo bila kujali la Manispaa au la Jiji na kadhalika ili na sisi Halmashauri twende tukajenge barabara ambayo ukitilia maanani mtandao wa barabara kwenye halmashauri ni mkubwa kuliko kwenye majiji au manispaa. Kwa hivyo niwaombe Wabunge wenzangu katika hili tuwe pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Fedha TAMISEMI mgao wa fedha hizi bilioni 300, zigawiwe katika majimbo, nikiamini kila Jimbo litapata karibu millioni 800 na tutaenda kufanya kazi kubwa ya barabara. Ndani ya miaka mitano nataka nitibitishé katika Bunge hili kwamba suala la barabara litakuwa ni historia katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii vile vile kutoa pongezi za dhati kwa Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi tuliahidi na bahati nzuri nilikuwa ni Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa mpaka naingia hapa Bungeni. Nilipita Mkoa mzima wa Morogoro tukiahidi kila kitu tutafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *REA*, walipotuambia umeme tulisema mpaka kufikia 2023 tutakuwa tumekamilisha kabisa. Nataka nitoe taarifa na shukrani za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini na Mkoa wa Morogoro. Jana Mkoa wa Morogoro tumezindua rasmi *REA* III mzunguko wa II, vijiji vyote vinapata umeme. Hongera sana kwa Serikali yangu ya Chama Cha Mpinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru leo asubuhi katika kuuliza swali imeonekana vijiji vile ambavyo vimepungua, Wizara imesema kwamba navyo vitaingia hata kama havipo. Kwango vimebaki vijiji vitano tu, ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niishukuru Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi kwa kazi kubwa ambayo imeifanya, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli alipokuwa katika ziara yake katika siku zake za mwisho katika dunia hii, alisimama Morogoro na akasema atatoa kilometra 40 kujengwa kwa lami kutoka Mjini Morogoro mpaka tutakapoishia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru katika bajeti hii tumetengewa kilometra 15 na tayari imeshatangazwa maana yake kazi inaenda kufanywa, nina kila sababu ya kuipongeza Serikali, lakini niiombe Serikali barabara hii inakwenda mpaka kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere inakwenda mpaka kwenye Hifadhi ya Mwalimu Nyerere tuendelee kutenga fedha ili tufike huko, utalii ukaendelee kuwepo kwenye Hifadhi, lakini vile vile katika hilo bwawa la Mwalimu Nyerere. Naamini bwawa hili likikamilika utakuwa ni utalii mkubwa ambaao utaingiza fedha nyingi kwenye Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, naomba nichangie kwenye maeneo mawili. Eneo la kwanza ni kwenye kodi; ni imani yangu hakuna Mtanzania ambaye hataki kulipa kodi, ila lipo jambo ambalo Serikali inatakiwa kufanya kupitia *TRA* kwamba kodi inayokadiriwa iwe na uhalisia na inayolipika. Katika maeneo mengi wafanyabiashara wanalia na ukweli usiofichika wanalia, kuna kama dhuluma ambayo inatendeka. Sasa katika hili, Mama yetu amesema hataki dhuluma, anataka watu walipe kodi kwa hiyari, naomba Mheshimiwa Waziri akasimamie hili *TRA*, kodi ikawe ya uwazi na iwe inayolipika kulingana na mwananchi alivyopata kipato chake, *failure to that*, ni kwamba watu watakwepa au tunatengeneza mianya ya rushwa kati ya watu wa *TRA* na walipakodi, mwisho wake kodi itakuwa haiwezi kulipika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho ambalo ningependa...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa  
Mzungumzaji)*

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Muda umekwisha?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja ili kazi iendelee, haya yote niliyosema yakamilike. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa namwita Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi wakati huo huo Mheshimiwa Jonas Van Zeeland na Mheshimiwa Deus Clement Sangu wanajandaa.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyezekiti nashukuru kwa kunipa fursa hii. Kwa kuanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kunifanya nisimame mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia nitume nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya na anayoendelea kuifanya.

Vile vile nimpongeze Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Serikali nzima kwa ujumla, wanafanya kazi kubwa sana. Mwisho, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu na Watendaji wote chini ya Katibu Mkuu ndugu yangu Tutuba. Nafahamu umahilri wake, naamini tutaenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, bajeti tunayojadili ni bajeti nzuri sana na nitumie nafasi hii kuwaomba sana Watanzania na hasa wa eneo la Ukerewe waipokee bajeti hii kwa sababu ni bajeti nzuri, inagusa mambo mengi ya msingi yanayogusa maisha ya waanchi wa ujumla wake. Pia bajeti hii inaonesha uelekeo mzuri na zaidi na inatia matumaini, kwa hiyo niwaombe Watanzania waipokee kwa moyo ya dhati kabisa kwa mikono miwili kwa sababu ni bajeti inayotunesha tunapoelekea ni pazuri.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, ningependa kushauri kwenye maeneo machache sana. La kwanza, bajeti hii kama nilivyosema ni bajeti nzuri, imegusa mambo mengi sana ya msingi na imizingatia ushauri ambaao Wabunge tumeutoa katika mijadala mbalimbali. Bajeti hii ili tuweze kuitekeleza vizuri na yale manufaa tunayotarajia tuweze kuyaona, ni lazima tu-*maintain* walipakodi tulionao, lakini tutengeneze walipakodi wengine ili tuweze kupata nguvu ya kutekeleza haya tuliyoyapanga kwenye bajeti, kwenye mpango, mwisho wa siku yale tunayotarajia yaweze kupatikana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo katika mambo yaliyosaidia sana kuchochaea kukua kwa uchumi mpaka tukafikia uchumi wa kati ni pamoja na kusambaa kwa umeme, jitihadi zilizofanywa na Serikali kusambaza nishati ya umeme, kuboresha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya, maji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia eneo hilo hilo, ningependa kuongelea kwenye eneo la nishati ya umeme. Umeme ni injini kubwa sana ya kuchochaea maendeleo ya wananchi kwa ujumla wake na nimefarijika kwenye bajeti hii, bajeti kuu lakini hata bajeti ya Wizara ya Nishati, Serikali imeonesha dhamira yake ya kuendelea na *program* ya usambazaji wa umeme kwenye vijji ambavyo havikufikiwa na umeme lakini mpaka kwenye vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo jema sana na likifanyika hili itasaidia sana kuchochaea uchumi wa watu wetu na litasaidia kuongeza wigo wa walipa kodi kwasababu tuna vijana wengi ambaao wana mawazo, wangependa kujajiri, lakini wanaweza kujajiri kama watakuwa na nishati ya umeme ili kuweza kuanzisha shughuli zao ndogo ndogo. Kama hili litafanyika litakuwa ni jambo jema sana. Kwa hiyo niiombe Serikali iweke mkazo na iweze ku-*finance fully* kwenye eneo hili la usambazaji wa umeme. Tusingahau kwenye bajeti ya Wizara ya Nishati illionekana katika mipango waliyonayo ni pamoja na kusambaza umeme kwenye maeneo ya visiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo la Ukerewe kwa mfano, ambalo linaundwa na visiwa 38, katika wakazi zaidi ya 400,000 tulionao karibu asilimia 40 ya wakazi wanaishi katika visiwa vidogo vidogo ambavyo bado havina umeme. Kwa hiyo kutofikiwa na umeme kunadumaza maendeleo ya watu hawa na kwa maana hiyo kunadumaza vile vile jitihada za kuongeza walipakodi wengine kuititia shughuli mbalimbali ambazo wangezifanya kuititia ujasirimali. Kwa hiyo niiombe Serikali tuhakikishe kwamba kuititia bajeti hii tunaweza ku-*finance* kwa kiwango kikubwa ili kuhakikisha kwamba *program*

tuliyonayo ya upelekaji umeme vijijini na hasa visiwani tunaikamilisha kwa asilimia 100. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Mpango wa Pili wa Maendeleo vile vile unaonesha kwamba Sekta ya Kilimo hasa kwenye eneo la uvuvi iliongezeka na ndio maana utaangalia hata kwenye uchakataji wa minofu ya samaki kwa kipindi kilichopita tani zaidi ya 26,000 zilisafirishwa ukilinganisha na tani 23,000 zilizosafirishwa miaka minne, mitano kabla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni jema sana na shabaha ya Mpango wa Tatu ni kuchochea maendeleo ya watu. Katika kuchochea maendeleo ya watu ni pamoja na kukuza uchumi wa watu wetu hasa kwenye maeneo ambako shughuli mbalimbali za uzalishaji zinafanyika. Sasa niombe, Kanda za Ziwa ambao wanazunguza ziwa Victori kuna uzalishaji mkubwa wa Samaki. Kama nilivyoonesha hapa kumekuwa na ongezeko kubwa sana na ufanisi kwenye sekta ya uvuvi. Katika samaki wanaozalishwa katika ukanda ule karibu asilimia 30 ya samaki wale wanapatikana kwenye Visiwa vya Ukerewe, lakini bahati mbaya sana Ukerewe hakuna Kiwanda cha Kuchakata Samaki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali ilione hili, ili kuweza kuchochea maendeleo ya watu wa eneo lile na kwa sababu ndio shabaha ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo, basi Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Mwigulu aangalie uwezekano wa kuwa na Kiwanda cha Kuchakata Samaki kwenye eneo la Ukerewe pale. Kwa sababu samaki wanazalishwa pale na wakichakatwa pale, shughuli za ujasiriamali zitakuwepo na kwa maana hiyo kuongeza wigo wa walipakodi na wananchi wengi watashiriki kwenye kuchangia pato la Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe Wizara iweze kuliangalia jambo hili. Eneo lingine ambalo napenda kushauri ni kwenye eneo la Madiwani. Niipongeze sana Serikali kwa kufanya uamuzi wa kuchukua jukumu la kuwalipa Madiwani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Sasa pamoja na

kuchukua jukumu hili kumekuwa na kilio kikubwa sana cha Madiwani wetu kuomba posho hizi wanazozipata ziweze kuongezwa. wamesema Wabunge wenzangu ni jambo jema. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile pamoja na kuchukua jukumu la kulipa posho za Madiwani kuna kundi kubwa sana la viongozi wetu wa vijiji na vitongoji na mitaa; Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Vitongoji na Wenyeviti wa Mitaa. Niiombe Seirkali itoe mwongozo kupitia TAMISEMI, basi lile eneo ambalo Halmashauri zilitumia kulipa Madiwani zihakikisha mafao ya Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa yaweze kulipwa *effectively* ili kuweza kuhamasisha shughuli za maendeleo kwenye maeneo yetu. Nakushukuru sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jonas Van Zealand.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya hatimaye nimeweza kusimama katika Bunge Iako Tukufu kutoa mchango wangu. Nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kaka yangu Mwigulu Nchemba na Naibu wake kwa kazi nzuri ambazo wamezifanya katika Wizara hii ya fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kwa kazi nzuri ambazo amezifanya toka amechukua madaraka ya kuongoza nchi yetu kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nimpongeze kwa namna ambavyo tumeona ana nia ya dhati kabisa ya kuhakikisha miradi ya kimkakati ambayo walianshisha pamoja na Mheshimiwa Hayati, ana nia ya kuimaliza lakini pia na kuanzisha miradi mipya ya kimkakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na suala la Madiwani. Naomba pia ku-*declare interest*, mimi nilikuwa

Diwani kwa miaka 10 na nilikuwa Mwenyekiti wa Halmashauri kwa miaka 10. Moja ya changamoto ambayo Madiwani walikuwa wanapata ni suala la posho hizi za mwezi. Serikali kwa kuamua sasa kuwalipa moja kwa moja Waheshimiwa Madiwani, kwa kweli watakuwa wamewasaidia sana. Wakurugenzi walikuwa wana-take advantage ya kuwalipa Waheshimiwa Madiwani kwa namna wanavyotaka wao na kama kuna mambo ambayo yanataka kujadiliwa kwenye vikao, Madiwani hawana sababu ya kupinga maamuzi ya Mkurugenzi kwa sababu wanajua mwisho wa siku Mkurugenzi hatatulipa posho zetu. Sasa kwa kuwalipa moja kwa moja, wataenda kutenda haki kwenye vikao bila kumwogopa mtu yejote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia jambo kubwa hapa ni kuongezewa posho. Madiwani wanalipwa shilingi 350,000. Kazi kubwa ambazo wanazifanya Waheshimiwa Madiwani kwenye Kata kule ni kuhakikisha wanasimamia miradi ya fedha nydingi ambazo ndizo tunazipitisha hapa Bungeni, wao ndio wanakwenda kuzisimamia, lakini kwa mwezi Diwani analipwa shilingi 350,000. Hata mtendaji wake wa Kijiji anapata fedha nydingi kuliko Mheshimiwa Diwani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri hebu endeleeni kuwaangalia Waheshimiwa Madiwani, angalau na wenyewe hata wakiongezwa shilingi 100,000 au shilingi 200,000 posho za kujikimu, ikafika kwenye shilingi 400,000 na kitu au shilingi 500,000, tutakuwa tumewasaidia sana. Mwisho wa siku na wenyewe wapande hadhi sasa walipwe mishahara. Wanafanya kazi kubwa, nasi Wabunge tunawategemea sana Waheshimiwa Madiwani watusaidie tukiwa huku Dodoma. Wao ndio wanafanya kazi kule usiku na mchana kwa wananchi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine sasa, Wakurugenzi waache visingizio vya kukosa pesa za vikao. Wameshapunguziwa mzigo mkubwa sana kwenye hii shilingi 350,000/=, wafanye vikao kwa wakati. Kamati ya Fedha inatakiwa kukaa kabla ya tarehe 15 kila mwezi, lakini baadhi

ya Halmashauri wanakaa miezi mitatu halafu wanapitisha miezi miwili yote kwa pamoja kwa siku moja. Au miezi mitatu wanapitisha kikao cha siku moja, lakini kisingizio ni nini? Mkurugenzi anasema hana pesa. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri hili nalo mliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nawashukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wako kwa kututengea shilingi milioni 600 kwa kila Jimbo kwa ajili ya sekondari ya kata. Nina ushauri kidogo hapa Mheshimiwa Waziri. Mfano kwangu tuna upungufu katika Kata ya Kweuma, Mkindo, Lubungo, Kikeo, Msongozi na Homboza. Nina upungufu wa kata sita hazina sekondari ya kata. Kwa hii shilingi milioni 600 kila mwaka itabidi nikae miaka sita ndiyo jimbo langu zima liwe limepata sekondari za kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, hii shilingi milioni 600 kama inawezekana, kama mtaona mnaweza mkaigawanya na Halmashauri wenyewe kwa kushirikiana na Mbunge na Waheshimiwa Madiwani wakaweza kuhamasisha wananchi wakachangia fursa, hii shilingi milioni 300 ikanunua vitu vya madukani; mabati, nondo, *cement* na kulipa fundi, tunaweza tukajenga sekondari mbili kwa shilingi milioni 600. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna sekondari ambazo tumezijenga wenyewe, Serikali imekuja kumalizia kwa fedha ndogo sana. Sasa shilingi milioni 600 ni fedha ambazo tunaishukuru sana Serikali kutupatia, lakini kwa sekondari ambazo ni nyingi kama kwangu mimi; sekondari sita, hatutaweza kumaliza kwa muda mfupi, itahitaji miaka sita ili tuweza kuzimaliza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishukuru Serikali, kwa kipindi chote, bajeti ya TARURA katika Wilaya ya Mvomero haizidi shilingi milioni 600. Sasa hivi kwa mwaka huu wa fedha mmetenga shilingi milioni 815. Nina imani tutakwenda kutengeneza barabara hizi za TARURA vizuri zaidi na hasa barabara za pembezoni mfano Kata ya Maskat, Kata ya

Kinda, Kibati Pemba, Kikeo, Nyandila na maeneo mengine, hizi barabara za TARURA ziweze kuitika vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, tulilalamika hapa wakati tunachangia bajeti ya TAMISEMI kuhusu suala zima la TARURA na mmesikia kilio chetu, mmeweza kutuongezea shilingi milioni 500 nje ya bajeti. Hizi zitakwenda kufanya kazi kubwa na nzuri katika Jimbo letu. Nami nikuhakikishie Mheshimiwa Waziri kama kila mwaka tutaendelea kupata hizi shilingi milioni 500 basi miji ile yote ambayo iko ndani ya Wilaya yetu ya Mvomero tunakwenda kuipa vipande vidogo vidogo vya lami. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni hii faini ya boda boda. Faini ya Boda boda ilikuwa ni shilingi 30,000/=. Mama yetu amesikia kilio, mmepunguza mpaka shilingi 10,000/=. Tatizo kwenye hizi faini sasa, Askari wanapokamata pikipiki, badala ya kulipa lile kosa moja shilingi 10,000/= sasa watalipa makosa nane, tisa mpaka 10. Ile shilingi 30,000/= itarudi na zaidi ya ile 30,000/=. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi na bahati nzuri Waziri wa Mambo ya Ndani uko hapa, hawa Askari wakikamata hizi pikipiki, anaweza akawa amekamata kwa kosa moja pengine la kutokuvaa *helmet*, yule dereva wa bodaboda hana ile hela, anachukua pikipiki wanaipeleka kwenye Kituo cha Polisi. Wakati pikipiki iko pale, anapoenda kuitafuta shilingi 10,000 au ile shilingi 30,000 ya zamani ili aende akagomboe ila pikipiki, akirudi pale anaambiwa hii pikipiki ilifanya mauaji, ilibeba mtu ambaye amekwenda kushiriki mauaji. Yule dereva wa bodaboda anakimbia anaitelekeza pikipiki na yule mwenye pikipiki hakanyagi kwa sababu anajua dereva wake alishakwenda kufanya mauaji na ile pikipiki. Mwisho wake ile pikipiki inakwenda kuuzwa kwa Askari wenyewe, wanauziana ile pikipiki. Baadhi ya vituo wamefanya hivyo, hata Mheshimiwa Waziri ukitaka ushahidi nitakupa. Wamekusanya pikipiki, wameshindwa kuzigomboa, wamewapa kesi za kutisha za mauaji, wamezitelekeza, wameuziana wenyewe maaskari hizi pikipiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii shilingi 10,000/= hii ambayo mama ametaka kuwalenga hawa vijana, kama hamtakuwa makini, watakwenda kutengenezewa kesi na pikipiki watazisahau kule kwenye vituo vya polisi. Kama ni faini, hatalipa shilingi 10,000/=, atalipa kuanzia makosa Matano, sita na kuendelea kama ambavyo walikuwa wanafanya. Kwa hiyo, Mheshimwa Waziri naomba hili nalo mliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni mpango wa bima nchi nzima. Hili ni jambo jema sana, lakini hizi zahanati zetu hazina madawa na wala hazina vifaatiba.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Namwita Mheshimiwa Deus Clement Sangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Abeid Ramadhani Igondo, halafu Mheshimiwa Omar Issa Kombo na kisha atamalizia Mheshimiwa Jumanne Kishimba.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kutoa mawazo yangu katika Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kufikisha salamu za wananchi wangu wa Jimbo la Kwela. Wamenituma nisimame ndani ya Bunge hili Tukufu nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa mambo makubwa aliyotufanya. Mwanzoni mwa Bunge hili nilikuja kulalamika, tulikuwa na maafa makubwa; madaraja karibia 18 yaliondoka katika Jimbo langu. Nashukuru Mheshimiwa Rais katika Awamu hii ya Sita ametutizama kwa jicho la huruma, ametuletea fedha takribani shilingi bilioni 3.6 za kwenda kurekebisha madaraja haya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi katika barabara ya Kata 13 za Bonde la Ziwa Rukwa, Mheshimiwa Rais ametukumbuka katuletea shilingi bilioni 4.8. Kwa kweli wananchi wamesema tufikishie pongezi kuitia Bunge hili Tukufu ili Mheshimiwa Rais ajue Wana-Kwela wanathamini jinsi anavyowajali na anavyowakumbuka wakati wa matatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe ametuletea shilingi bilioni moja kujenga ofisi ya Makao Makuu katika Mji Mdogo wa Laela na shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya miradi ya afya na elimu. Wananchi wa Jimbo la Kwela ndani ya kata zote 27 wanampongeza Mheshimiwa Rais, wanamwombea afya njema na siha, aendelee katika *speed* hii hii alioionesha ndani ya miezi hii mitatu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe, shilingi milioni 500 ambazo tumetangaziwa neema na Waziri, dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu, pia shilingi milioni 600 za barabara; na wananchi wa Jimbo la Kwela pia wanamshukuru Mheshimiwa Rais na timu yake ndani ya Serikali kwa namna ambavyo amekuja kwa kasi ya ajabu kuwaleta wananchi maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna shukurani ambazo nimetumwa na Waheshimiwa Madiwani wa Jimbo langu kwamba katufikishie salamu kwa kutukumbuka. Nasi tunaanza kulipwa kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. Shukrani ya pekee wanaomba, angalau hii isiishie hapa, iwekewe sheria maalum ili kesho asije mtu mwingine akabadilisha kwamba hii ilikuwa batili. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, nakuletea hii habari ya Madiwani wangu, naomba uisikilize na mkaifanyie kazi, muifanyie *reinforcement*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nitoe pongezi kwa Wizara hii ya Fedha. Nakupongeza ndugu yangu, *First Class Economist*, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, kwa kweli unaitendea haki hiyo *First Class* yako ya uchumi. Ndugu yangu kwenye Kamati yangu tulikuwa

naye *PAC*, tulikuwa tunamwita *Engineer* wa Kamati ya *PAC*. Kweli kazi mnayoifanya kwenye Wizara hii ya Fedha mna-deserve sifa kubwa sana, mmetuletea bajeti ambayo ni *realistic*, ambayo inakuwa *communicated*. Tunai-*communicate* vizuri kwa wananchi na wameielewa. Naomba kwa *spirit* mliyokuja nayo mwendelee hivi hivi. Kweli Watanzania wanaanza kupata matumaini makubwa kutokana na bajeti hii ya kwanza katika Awamu hii ya Sita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa pongezi zangu, nina mambo ya kuishauri Serikali. Naomba hapa tusikilizane vizuri kwa umakini mkubwa sana. *Ni-declare interest* kwamba, nisipoona mkulima wangu au wakulima ndani ya nchi hii wanatetewa, nakuwa mnyonge kwa sababu kwanza mimi binafsi ni mtoto wa mkulima. Nimekuja niongelee jambo moja kwa umakini mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NFRA* - Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, ndiyo *instrument* pekee ya Serikali ambayo inaweza ikawa na *touch* au *DNA* na wakulima wetu kwa sababu hili ndilo soko la uhakika la wakulima kwa mazao yetu ya nafaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa napitia bajeti hapa. Tumewatengea bajeti ya shilingi bilioni 14. Mwaka wa fedha uliopita ilikuwa shilingi bilioni 15; kwa hiyo, kila mwaka tunapunguza kidogo. Miaka minne *back* hapo, tulikuwa tunawatengea shilingi bilioni 100. Sasa tunapoi-*cripple* hii *NFRA* maana yake tumeamua tuwazike wakulima wetu na hawa ndio wata-*participate* vizuri katika ku-*implement* bajeti hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tukafikirie, *NFRA* ina vyanzo vingi, achana na *grant* ya Serikali, wao pia walikuwa na *room* ya kwenda kukopa kwenye *Commercial Bank*. Mwaka 2019/2020, nina *story* naisikia kwamba mmewazuia Wizarani kwako Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, *fieldmarshal*, naisikia hamtoi vibali, wakakope. Wamekopa shilingi bilioni 35, lakini wamerudisha kwa uaminifu mkubwa,

mpaka *Commercial Bank* nyingine wamethamini kwamba *NFRA* ni wateja wazuri. Hizi hela hawaendi kulipana posho, zinaenda kununua mazao hata kwa dada yangu, Mheshimiwa Jenista Mhagama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana, nendeni mkatoe hicho kibali *NFRA* wakachukue hizo bilioni nyingi, warudishe kwa wakulima, wanunue mazao; na kwa sababu jukumu lao ni kutafuta masoko nje, wataenda kuuza huko, tutafanya *recycling* ya ile, itarudi tena kwenye mzunguko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa *construction industry* imefanya vizuri tume-*invest* mabilioni ya pesa; na ndiyo inafanya vizuri, ime-*contribute* asilimia 13 katika uchumi; kilimo 4.8; lakini *investment* kwenye kilimo ni *short term investment* ambayo *impact* yake tunaiona kwa haraka. Msilwanyime, waende kwenye *Commercial Bank* na ziko *willing* kutoa hiyo mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba kabisa, ndugu zangu naamini ninyi ni wasikivu, naombeni msikilize ili mkawakomboe wakulima. Kwa sababu mtapopeleka fedha ile tunaongeza *purchasing power* yao na ndio hao wataweza kuonja kwamba tuko kwenye uchumi wa kat, kwa sababu ya fedha zile tulizowapelekea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja ambalo limekuwa likisikitisha na hili naomba niongee nikutwishe mzigo dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama. Kutokana na ripoti ya CAG, inaonesha *NFRA* ilikopwa na Kitengo cha Maafa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, shilingi bilioni 167. Hizi zinanunua karibia tani 365,000. Sasa miaka 12 hamjarudisha hata senti moja, nendeni mkaweke utaratibu mzuri tukawalipe walau kwa *installment 12 years*, hawarudishiwi kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutai-*paralyse* hii *institution* ya *NFRA* ambayo ni muhimu sana kwa wakulima wetu masikini wakiwemo wakulima wa Mkoa wa Rukwa, Ruvuma, Njombe

na Iringa wanaitegemea sana *NFRA*. Nawaomba mwende kama Wizara, m-discuss jambo hili muone ni namna gani ambayo mtarudisha hizi fedha kwa wakulima. (*Makof*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULAMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULAMAVU:** Namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kukumbusha hilo deni ambalo anasema limejitokeza kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu. Naomba tu kumpa taarifa kwamba deni hilo ni yale mahindi ambayo yanakwenda huko huko kwenye Halmashauri za Waheshimiwa Wabunge ili kushughulikia matatizo mbalimbali wakati wa maafa na vitu vya namna hiyo, lakini hasa wakati wa maafa, ndio yale mahindi tunayowaletea huko. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote, ulizaneni kwenye Halmashauri zenu; Halmashauri ambazo hazijalipa zirudishe hiyo fedha haraka sana ili iweze kufanya hiyo kazi ambayo Mheshimiwa Mbunge anaishauri.

Kwa hiyo, naomba nitoe hiyo taarifa, nadhani Mbunge atakubaliana nami Halmashauri waharakishe kurudisha hizo fedha. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbunge unapokea taarifa hiyo nzuri?

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Taarifa hiyo naipokea, lakini mzigo mzigo tunawakabidhi Wanyamwezi kwa maana Ofisi ya Waziri Mkuu watusaidie kulibeba hili. Huko Halmashauri ni wadogo, likiwa

kwa mkubwa, Waziri Mkuu naamini litafanyiwa kazi kwa umakini mkubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme jambo moja. Nchi yetu kama Tanzania tuna *advantage* kubwa. Kwenye uzalishaji; *productionwise* na *locationwise* katika nchi zilizopo kwenye ukanda wa Maziwa Makuu, tuna faida kubwa. Sasa *NFRA* walishapewa *mandate*; katika dhima yao mojawapo ni kuhakikisha usalama wa chakula nchini kwa kununua, kuhifadhi na kuzungusha chakula. Kwa hiyo, wanaruhusiwa kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Waziri Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu hapo, tusaidieni, kaiwezesheni hiyo ofisi ika-*capitalize* hayo masoko yaliyopo katika nchi za Maziwa Makuu ili tukawanusuru wakulima wetu. Kama tukiwa *serious* kweli kuiwezesha hii *NFRA*, nawahakikishieni nchi yetu tutaenda vizuri katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. Ahsanteni sana. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango mzuri Mheshimiwa Deus Clement Sangu. Sasa namwita Mheshimiwa Omar Issa Kombo, wakati huo Mheshimiwa Jumanne Kishimba anajiaandaa kuja. Mheshimiwa Omar hayupo, Mheshimiwa Jumanne Kishimba. (*Makofî*)

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naungana na Wabunge wenzangu kuchangia kwenye bajeti hii ya 2021/2022. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Baraza zima la Mawaziri pamoja na Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru sana Serikali kwenye suala hili la barabara baada ya kukubaliana na kilio cha Wabunge na kuweza kutenga pesa hasa upande wa *TARURA*. Nashukuru sana kwa sababu kama kilio cha Wabunge wote kilivyokuwa, ilikuwa ni tatizo kubwa sana

kwenye maeneo yetu, nami mwenyewe kwenye Jimbo langu la Kahama nilikuwa mwathirika mkubwa sana wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye barabara naomba kushauri kidogo kwamba zamani mpaka miaka ya 1990 barabara zilikuwa na mtu anaitwa *Road Surveyor* ambaye alikuwa anaamka asubuhi akiwa na baiskeli; mmoja anakwenda upande mmoja kilometa tano, mwingine anakwenda na baiskeli kilometa tano akiwa amebeba koleo au jembe akiangalia zile sehemu ambazo barabara imeumia. Hii ilisaidia sana barabara zile kuendelea kutibiwa yale maeneo ambayo madogo madogo yanaoonesha ubovu, lakini baadaye watu hawa waliondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba wenzetu wa *TARURA*, kama wanaweza kuwarudisha tena. Maana yake kwa sasa hivi kwenye maeneo yetu *TARURA* inakuwa na wafanyakazi wawili au watatu. Kwa wingi wa barabara, haiwezi kuzi-*repair* zile barabara mpaka mwakani. Kama unaweza kuwarudisha watu hao na leo tuna pikipiki, inaweza ikatusaidia sana kuliko kusubiri mpaka barabara zote zimeharibika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wetu ni kama tembo aliyebebwa na sisimizi, lakini tembo huyu huwa hafahamu kama amebebwa na sisimizi. Mara nydingi akipata shida kidogo huwa anapenda sisimizi watoke. Nasema hili nikiangalia hili suala la machinga. Sisi ambao tunatoka maeneo ambayo miji yetu haina ajira rasmi; kwenye Jimbo langu watu walioajiriwa na mishahara kabisa katika watu 500,000 hawafiki watu 5,000; na wenye mshahara ambao unaweza kutosha kutoka tarehe 1 mpaka 30, hawafiki 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali inavyoendelea, Mheshimiwa Waziri inaonekana kama kuna mchaka mchaka dhidi ya machinga au wafanyabiashara wadogo wadogo kuja kuondolewa kwenye maeneo yao. Watu hawa tumekuwa nao zaidi ya miaka mitano, wametusaidia sana kwenye shughuli za kibiaшara na wame-stable na wamepata ajira. Leo kama tutaona kwamba tuwatoe, linanipa shaka

sana kwa sababu watu hawa wamesaidia sana maeneo mengi hasa kwenye shughuli za wakulima. Bidhaa wanazouza ukiacha zile za nje ni bidhaa za wakulima wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo viazi ulaya kwa wenzetu wa Kusini wameongeza ukulima mara tano zaidi lakini aliyesababisha viazi ulaya viende ni Mama Ntilie. Kwa sababu, leo huwezi kuipika chipsi nyumbani kwa sababu ukipika chipsi unahitaji zaidi ya lita mbili za mafuta, lakini mama ntilie na machinga wameendelea kupika chipsi hizo na kusababisha ulaji mkubwa sana wa viasi. Sasa sijui wenzetu wateule nini hasa kinachowabuguzi, maana yake leo mahindi wanayochoma ni mahindi ya wakulima, ina maana wamemsaidia mkulima na wao pia wamepata ajira. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wanauza miwa wanaikatakata wanalkamu miwa wanawasaidia wakulima wetu lakini na wao wanapata ajira. Nafikiri wachumi wetu wajaribu kwenda kwa data ndani zaidi, leo hii ukiangalia uuzaaji wa kuku wa kizungu, waliosababisha ulaji wa kuku leo, siyo matajiri wala siyo watu wa hali ya juu, walio sababisha ni watu wa hali ya chini ambao mpaka wamewezesha watu kula utumbo wa kuku. Kwa sababu, leo wanaweza kumkatakata kuku mpaka shilingi 400, 500 kwa hiyo wamepeleka biashara hiyo na wamefanya nyie mnachosema kitaalamu wame *add value* nafikiri hawa ndiyo walio *add value* kuliko mtu yoyote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea Serikali ikawape motisha lakini kama Serikali inang'ang'ana kwenda kuwatoa au kuwakataa na vijana wetu waliomaliza shule wote tunategemea waende kwenye kazi ya machinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye majimbo kama ya kwetu ambayo yameathirika sana na shughuli za migodini, ukiondoa wale wajane ambao wako kwenye Biblia na Quran, sasa hivi tuna wajane ambao wametelekezwa na wanaume na wana watoto kuanzia wanne mpaka watano mpaka saba, shughuli zao hawa wakinamama ni shughuli hizo hizo ndogo ndogo. Serikali yetu haina utaratibu wowote wa

kumsaidia mjane, haina utaratibu wowote wa kumsaidia mama aliyetelekezwa na ana watoto atafanya nini unapomtangazia klama. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rahisi sana mtu ambaye anamaisha mazuri kutamka, kwamba machinga wanaleta uchafu, nirahisi sana lakini machinga wamekwenda *Oyster Bay* wanatamuuzia nani? Hakuna machingia ambaye yuko *Oyster Bay*, hakuna mashinga ambaye anakwenda Masaki, kama wako Kariakoo sisi wenye halinzuri ndiyo tumewafuata, tumeenda kutafuta nini kule kariakoo? Maana sisi tuna maduka yetu kule *Oyster Bay* yapo, sisi tunaenda kutafuta nini Je, tunaripoti yoyote yenye lawama zidi ya wenye duka na machinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kama sisi Kanda ya Ziwa hatuna ugomvi wa Wafugaji na Wakulima kwa sababu sisi tunazo ng'ombe zaidi ya miaka 200, lakini ugomvi uko kule Morogoro ambako wafugaji wameenda mara ya kwanza lakini machinga, hawajawa na ugomvi wowote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kinanipa kigugumizi ni nani hasa ambaye anawaza kwamba hawa watu hawafai. Baada ya uhuru tulikuwa na wahindi na wa-Asia na waswahili kwenye miji yetu, lakini mwaka 1980 baada ya kuvunjika ujamaa na viwanda *collapse* watu walibaki kule mjini, hawa wamezaliwa kule mjini baada sehemu hiyo imevutia, tena watu wameenda kukaa kule, hii ni kabila mpya imeonekana mjini, hawa watu hawawezi kulima, hawawezi kufuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, tunataka waende wapi hasa, labda Serikali wakati wa kuhitimisha watupe jibu kwamba watu hawa wanatakiwa kwenda wapi? Hawawezi kulima, hawajawai kulima, wamezaliwa mjini hata kabile zao ukiwaliza wanasema kwetu Mwanza, kwetu Moshi lakini hajawai kufika Mwanza utawafanya nini? Nafikiri wateule wetu wajaribu sana kuwa wabunifu, watu hawa ni *resources* nzuri sana ya uchumi, nzuri sana wamefanya mabadiliko makubwa mno ya uchumi ila uwezi kuyaona. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye watu wa Mpesa sehemu zinazoongoza kwa kutuma Mpesa ni maeneo ya machinga peke yake ndiyo wanaongoza kwa kufanya biashara, hizi biashara bidhaa zote wanazouza, si Serikali amepata kodi. Lakini wao wanamlazimisha mtu kila mtu anatembea wanamlazimisha ina maana kazi wanayofanya ni kazi ngumu sana, sasa ni ajabu kama sisi tunaenda kungangana kuwatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, machinga ndiyo chuo kabisa *original*/cha kutoa wafanyabiashara leo Watanzania, je, hii ya kwenu CBE imewahi kutoa mfanyabiashara yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana tunakwenda kufunga chuo ambacho kinatoa watu *original*, tunaenda kufungua vyuo ambavyo havitoi wafanyabiashara tunaomba sana wenzetu hasa Mheshimiwa Waziri alifikirie sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Kishimba, mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo atakuwa Omar Issa Kombo.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwiningi wa Rehema anayetujalia mpaka sasa hivi tukiwa tuko katika hali ya afya na uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nianze kwa kukupongeza wewe kwa kunipatia fursa ya kuweza kuchangia hotuba ya bajeti kuu ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Aidha, nichukue fursa hii kabisa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kaka yangu Nchemba pamoja na Naibu Waziri kaka yangu Masauni kwa hotuba nzuri ambayo kwa kweli inawagusa Watanzania wote. Vile vile, nichukue fursa hii kuwapongeza sana

Waheshimiwa Mawaziri wote kwa ujumla wao kwa namna wanavyoendelea kujitoa kumsaidia mama yetu Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassain, kwa kweli Waheshimiwa Mawaziri tunawaambia hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona jinsi mnavyofanya kazi ya kuhakikisha kwamba mnawatumikia Watanzania kwa lengo la kulipeleka mbele Taifa letu, lakini vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna anavyoendelea kuwasimamia Mawaziri na kuisimamia Serikali kuhakikisha kutatua kero mbalimbali za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pongezi za pekee nimpongeze sana sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassain, kwa namna anavyoendelea kuiongoza nchi yetu kwa mafanikio na ufanisi mkubwa kwa kweli Mama huyu ametuheshimisha sana Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nampongeza Mheshimiwa Rais wetu siku tunamuaga mpPENDWA wetu Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, pale Jamhuri alituahidi watanzania kwamba hakutoharibika kitu na kwakweli tumeshuhudia hakuna kitu kilichoharibaka wote ni mashahidi tunaona kwamba miradi mbalimbali inaendelea kutekelezwa, hakuna mradi hata mmoja ambao umesimama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile na mpongeza sana Mheshimiwa Rais Samia kwa kutumiza matarajio, matamano ya mtangulizi wake Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Tunaona reli zinaendelea kujengwa, ndege zinaendelea kununuliwa, vituo vya afya vinajengwa, shule zinaendelea kujengwa, mradi wa umeme unaendelea kutelezwa, tunasema kwa kweli Mama yetu anafanya kazi kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii, niwaombe watanzania wenzangu kwa umoja wetu bila kujali tofauti zetu tusimame pamoja kumuunga mkono Rais wetu. Kwani ameonesha nia ya dhati ya kulipeleka mbele Taifa letu,

ameonesha nia ya dhati ya kuwasaidia watanzania kwa hiyo tusimame pamoja kumpa *support* kiongozi wetu Mama Samia Suluhu Hassan. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba sasa nichangie kwenye bajeti hii, kwa kweli nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, bajeti ni bajeti nzuri sana kwa kweli ni bajeti ambayo imegusa maisha ya watanzania na kwakweli ni bajeti ya kwanza watangulizi wetu wanasema hapa, kwamba ni bajeti ambayo imesikiliza vilio vya Wabunge kwa asilimia kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona suala la *TARURA* Wabunge tulismama hapa kwa umoja wetu kuzungumzia Sakata la *TARURA* na kwa kweli *TARURA* ilikuwa ipo katika hali mbaya, kwa sababu barabara za vijijini zilikuwa zipo katika hali mbaya. Ukingatia athari mballimbali zimeelezwa kutokana na ubovu wa barabara za vijijini ikiwemo kina mama kujifungulia njiani, watoto kufariki kutokana na kusombwa na maji kipindi cha mvua, lakini vilevile uzito na kupanda kwa gharama ya kusafirisha mazao yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha amekisikia kilio hiki na kwenda kuweka fedha kwenye mfuko wa *TARURA*. Lakini vilevile Mama yetu Samia Suluhu Hassan amesikia kilio hiki kwa kuweka kila jimbo shilingi milioni 500 tunakupongeza sana Mheshimiwa Rais wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuongoza na kuongeza vianzio vipyta vya mapato kwenye suala la mapato ya simu vilevile yanatokana na miala ya simu, lakini vilevile malipo ya *line*. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri na kwenye tozo za mafuta kwa kweli umefanya jambo muhimu sana na umeandika historia na watanzania wataendelea kukumbuka kwa kazi yako kubwa uliyoifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, tunafahamu kwamba Wizara ya Mawasiliano ni wizara ambayo haipo kwenye

Muongano, lakini kuna sekta ambazo tuna-share pamoja, mfano Sekta ya Mawasiliano kama Posta, lakini vilevile kama TTCL, Air Tanzania na mambo mengine. Sasa kianzio hiki kipyaa cha mapato ambacho kinakwenda kukusanya mapato kutokana na *line* za simu na miamala ya simu, tunafahamu kwamba simu hizi wanaotumia ni watanzania wote wa pande zote mbili upande wa Zanzibar na upande wa Tanzania Bara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini miamala ya simu inafanywa na watanzania wote na sisi upande wa Zanzibar wananchi walio wengi mpaka vijiji wanatumia simu, ni watu wachache sana ambaa hawamiliki simu. Sasa Mheshimiwa Waziri naomba ukija uje utueleze kama Wanzibar na sisi mmetufikiria vipi, tunakwenda kufaidika vipi kutokana na fedha hii ambayo itakusanya kutokana na makusanyo ambayo tunayachangia wote watanzania, tunaombeni sana na sisi kule Zanzibar kusema ukweli hali ni mbaya sana ya barabara zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile nije suala la fedha hizi milioni 500 kama tulivyosema kwamba Mama amefanya jambo zuri sana, lakini kiukweli na sisi Zanzibar barabara zetu za vijiji hali ni mbaya sana. Na tunafahamu hatuna shaka Mama yetu atakisikia kilio hiki.

Nichukue fursa hii kwa niaba ya Wabunge wenzangu wa Zanzibar tunamuomba sana Mama yetu, tunamlilia na sisi atuangalie hali zetu za barabara Zanzibar kwakweli ni mbaya, tunamuomba sana atuangalie ili na sisi aweze kutupatia fedha hizi na wala hatuna shaka kutokana na usikivu wake nina imani yangu kwamba atatufikiria. Waswahili wanasema Mama ni Mama na anaye mdharau Mama hukumbwa na laana, hatupo tayari kukumbwa na laana, tunafahamu sana Mama yetu ni msikivu na ataendelea kutusikiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kumalizia nigusie Sekta ya Uvuvi mara nyngi tumekuwa tukipiga kelele kuhusu Sekta ya Uvuvi hususani kwenye kanuni zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusema kwamba hadi sasa bado Serikali hajataka kuliangalia kwa ukaribu sana kuhusiana na changamoto ya kanuni ya uvuvi inayozuia *ring net* hadi sasa hivi ninavyoongea wavuvi wa Kigamboni na wa Mafia bado hawajapatiwa leseni, wanakaa hivi watu wanafamilia, wanakaa kila wakifika wanapigwa danadana hawapatiwi leseni kisingizio ni kanuni, tuambie, Mheshimiwa Waziri nikucombe au kwa Waziri Mkuu aliingilie kati wavuvi wanapata shida. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi wa *ring net* uliingia nchini mwaka 1984 mpaka 1985 Serikali iliwapatia kibali na ikuhalalisha uvuvi huu kwamba auharibu mazingira. Lakini kama haitoshi uvuvi wa *ring net* duniani nchi kama India, China, Norway, Dubai, Finland, Oman zinatumia uvuvi huu na uvuvi huu hata Shirika la Chakula Duniani unautambua uvuvi huu wa *ring net* kwamba hauharibu mazingira, iweje leo Tanzania tuseme kwamba uvuvi huu unaharibu mazingira. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba sana Serikali ituangalie ndugu zetu wanapata tabu wanategemea Sekta ya Uvuvi na Serikali inapiga kelele kwamba wananchi wajajiri sasa wanapoijajiri tunapokwenda kuwawekea vikwazo tujue tunawasababishia mazingira magumu. Mtu anatoka ameacha watoto nyumbani anakwenda sehemu za Mafia au Kigamboni kufanya shughuli ya uvuvi akifika anazuiwa tuliangalie sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache nasema naunga mkono hoja. Ahsante sana Mwenyekiti kwa kunipatia fursa. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tumefikia mwisho wa kikao chetu cha leo. Ninaomba hapa kuna tangazo maalum kutoka kwa Mheshimiwa Spika, ninaomba nilisome.

Mheshimiwa Spika anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba mujibu wa ratiba ya Mkutano wa Bunge

siku ya Jumanne wiki ijayo tarehe 22 Juni, 2021 ni siku ya upigaji wa kura ya kupitisha bajeti hii ya Serikali ya mwaka 2021/2022. Ambapo kila Mbunge anatakiwa kupiga kura ya wazi kwa mujibu wa Kanuni 126 (2), yaani utaitwa jina lako kwa sauti na utapiga kura yako kwa sauti, hivyo Wabunge wote siku hiyo mnatakiwa kuwepo Bungeni bila kukosa. Nasisitiza siku hiyo ya tarehe 22 Juni, 2021 lazima muwepo wote Bungeni.

Baada ya kukamilisha shughuli zetu Waheshimiwa Wabunge naomba sasa, natamka kwamba naihirisha shughuli za bunge hadi siku ya jumatatu tarehe 21 Juni, 2021 Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 01.35 Usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,  
Tarehe 21 Juni, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*